ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.

12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.

23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais

37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Tisa - Tarehe 3 Februari, 2014

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika: (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora: (Kny: Waziri wa Fedha): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Fedha naomba kuwasilisha mezani hotuba ya Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Baraza yanayotokana na Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika yaani *PAC* ya mwaka 2012/2013.

Mhe. Omar Ali Shehe: (Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*) Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma ya mwaka 2013/2014. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*).

TAARIFA ZA SERIKALI

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi Maji na Nishati: Mhe. Spika, awali ya yote naomba kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutujaalia uzima na afya njema leo hii na kutuwezesha kukutana hapa katika kikao hiki muhimu.

Aidha napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe Mhe. Spika, Naibu Spika, na Wenyekiti wa Baraza pamoja na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa ushupavu na uongozi wenu wa busara,uwajibikaji na uadilifu katika uendeshaji wa Baraza letu hili. Jambo ambalo limepelekea kuwa na mafanikio makubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Baraza letu hili.

Mhe. Spika, vile vile napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati yaMawasiliano na Ujenzi kwa mashirikiano makubwa wanayoipatia wizara yangu pamoja na kuipatia maelekezo na ushari katika utekelezaji wa majukumu yetu.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ilipokea jumla ya ushauri na maagizo 40 kutoka kwa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Mawasiliano na Ujenzi. Maagizo

hayo yamegusa Idara na taasisi mbali mbali zilizomo ndani ya wizara hii. Wizara ilifuatilia kwa karibu maagizo hayo ili kuhakikisha ufanisi wa utekelezaji wake.

Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwa Baraza lako tukufu juu ya utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na kamati kama ifuatavyo:-

Idara ya Ardhi na Usajili

Agizo la kwanza: Mhe. Spika, kamati imeishauri wizara ijitahidi katika utatuzi wa baadhi ya changamoto zilizopo ili kuwezesha idara hiyo ya ardhi kufanya kazi zake kwa umakini.

Mhe. Spika, katika kukabiliana na changamoto za mazingira bora ya kufanyia kazi. Idara imejitahidi kufanya matengenezo ya ofisi za vitengo iliyo chini ya Idara ya Ardhi ambapo kwa Unguja Kitengo cha Hati kimekamilika, na kwa upande wa Pemba cha Ardhi cha Macho Manne jengo linakarabatiwa. Kwa sasa idara inatarajia kuanza matengenezo katika Kiwanda kidogo cha Ukodishwaji wa Ardhi kwa wawekezaji.

Agizo la Pili: Kamati imeishauri wizara izidishe juhudi ya kutoa elimu ya Usajili wa Ardhi na inakubaliana na wazo la Idara la kuwashirikisha wanasiasa katika utoaji wa elimu hiyo.

Mhe. Spika, kuhusu utoaji wa Elimu ya Usajili wa Ardhi. Idara kutipia mradi wa *SMOLE* imefanikiwa kupata fedha kwa ajili ya kuendesha semina na makongamano yenye maudhui ya usajili wa Ardhi, sheria zake, taratibu zake na changamoto zake. Idara imeanza kutekeleza kwa ngazi ya Shehia, Wilaya na Mkoa.

Agizo la Tatu: Mhe. Spika, kamati inashauri kuwa suala la *Master Plan* liendelezwe kwa vitendo na lifuatiliwe kwa umakini zaidi kwa kuyaingiza maeneo ya vijiji katika mpango huo.

Mhe. Spika, kwa kushirikiana na Idara ya Mipango Miji na Vijiji. Idara imeendelea kutoa mashirikiano yenye lengo la kuhakikisha kuwa *Master Plan* inayotengenezwa iwe makini na yenye kuhusisha kikamilifu vijiji vya Unguja na Pemba. Idara inafuatilia suala hili kwa makini sana. Katika utekelezaji wa *Master Plan* ya Mji wa Zanzibar inayofadhiliwa na *World Bank*, idara imeandaa mpango maalumu wa kuwashirikisha wananchi wote kwa kuandaa mikutano mbali mbali inayoanzia katika ngazi ya Masheha wote na Mkoa wa Mjini Magharibi, Taasisi za Serikali na wafanyabiashara na Taasisi zisizo za serikali.

Agizo la Nne: Mhe. Spika, katika ripoti iliyopita kamati ilisisitiza suala la njia ya kutokea katika kituo cha ChakeChake ambapo eneo lilokusudiwa kupitisha njia hiyo kulikuwa na nyumba moja iliyokwamisha mipango hiyo. Kupitia ripoti hii kamati inataka kujua jambo hilo limefikia wapi, ile nyumba iliyokuwa ni kikwazo chenyewe walikubali tathmini ya fidia iliyofanywa na taasisi za serikali.

Mhe. Spika, kwa mtizamo wetu lile jengo liliopo kwenye eneo hilo husika kikwazo sio tathmini kwa utekelezaji huo kama sheria ya ardhi namba 12 ya mwaka 1962 inaelekeza kuwa:

Iwapo serikali itafidia ardhi kwa manufaa ya taifa basi muhusika atahamishiwa atapewa eneo mbadala au fidia.

Agizo la Tano: Kamati inaishauri wizara isaidie mahakama kupata fedha za kutosha kwa ajili ya ukarabati wa majengo ambayo yatatumika kwa shughuli za mahakama. Mhe. Wizara imefanya juhudi kubwa ya kuhakikisha kwamba ukarabati wa majengo hayo unafanikishwa na kwa hatua za hivi karibuni wizara imewasiliana na mradi wa *SMOLE* wao wamekubali kumalizia ujenzi wa Koani na hatua za ujenzi zinaendelea.

Agizo la Sita: Kamati inaiagiza mahakama ishirikiane na taasisi za ardhi katika utoaji wa hukumu zake ili kuepusha kuwadhulumu baadhi wa wamiliki wa ardhi. Ambapo Idara za Ardhi huwa zina ushahidi wa kutosha katika suala la ardhi. Mhe. Spika, Mahakama ya Ardhi ina wajibu wa kushirikiana na taasisi za ardhi pamoja na vyengine vyote vinavyohusiana na madai yaliyowasilishwa mahakamani kwa dhamira ya kulinda, kutoa haki ya kweli kwa kila anayestahiki. Mahakama imeendelea kutekeleza wajibu huo kwa kushirikiana na taasisi zote zinazohusika.

Agizo la Saba: Linashauri wazee wa mahakama waangaliwe kimaslahi kutokana na ugumu wa kazi zao wanazozifanya. Mhe. Spika, wazee wa mahakama wanalipwa ipasavyo kulingana na uingizwaji wa fedha za matumizi wa taasisi.

Idara ya Upimaji wa Ramani

Kamati imesikitishwa sana na taarifa iliyopewa kwa wakati na wafanyakazi wa idara wanapokwenda katika maeneo ya upimaji wanakosa ushirikiano kutoka kwa masheha. Hivyo kamati inashauri wizara isaidie wizara kwa kuitisha kikao na kuwahusisha Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya Masheha na Madiwani na kuwaelimisha umuhimu wa upimaji pamoja na kuwaelimisha sheria za ardhi.

Mhe. Spika, idara inakiri kwamba suala hili kweli lilikuwepo nyuma na idara imechukua juhudi za makusudi kutoa elimu ya upimaji kila inapowezekana. Idara imeweza kuona na kushiriki mikutano inayoendelea katika zoezi la kuwatambua wenye ardhi Unguja na Pemba ambapo imejumuisha Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Masheha madiwani kwa msaada wa *SMOLE*.

Idara pia inaendelea na zoezi la upimaji rasmi kwa mipaka ya wilaya Unguja na Pemba kwa msaada wa mradi huo wa *SMOLE*. Wakuu wa Mikoa na Wilaya pamoja na Masheha wote waliokuwemo kwenye maeneo ya mpaka husika wamehusishwa kikamilifu kwa kufanya kikao cha pamoja na kutoa elimu juu ya umuhimu wa wapimaji na masheha. Upimaji wa sheria za ardhi kabla ya upimaji huo.

Agizo la Tisa: Kamati inaishauri idara iingie gharama kwa kuandaa semina maalumu kwa Wajumbe wa kamati na ikiwezekana Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kuwapatia elimu kuhusiana na umuhimu wa upimaji ili wawe mabalozi katika majimbo yao.

Mhe. Spika, idara ilishindwa kuandaa semina kwa kamati hii kwa kipindi kilichopita kwa bajeti ya idara. Lakini lengo hilo bado lipo na limepangwa kufanyiwa kazi katika kipindi hiki cha bajeti.

Agizo la kumi: Kamati inazidi kukumbusha maoni yake imekuwa ikiyasisitiza kila inapofika kuwa kuna umuhimu wa kuengeza wataalamu wa masuala ya ardhi kutokana na hao waliopo kuwa ni wachache na hawatoshi. Hivyo kamati inaishauri kwa kuliangalia kwa umakini suala hilo.

Mhe. Spika, suala hili tunalikubali na idara imeanza kulishughulikia kwa kuajiri wafanyakazi ambao wanaendana na fani zetu za ardhi na upimaji. Hata hivyo bado mahitaji ni makubwa na tunayashughulikia. Vile vile wafanyakazi wenye fani hizi ni adimu kupatikana katika soko la ajira.

Idara ya Mipango Miji na Vijiji

Agizo la Kumi na Moja: Kamati imeishauri idara inapoandaa mipango yake ijitahidi kuandaa mipango ya kudumu na endelevu. Mhe. Spika, ushauri umepokelewa na hivi sasa mipango inayotayarishwa na Idara itahakikisha kuwa inashirikisha jamii katika utayarishaji na upangaji wake wa miji na vijiji ili iweze kuwa ya kudumu na endelevu.

Idara kwa sasa imeandaa mpango maalumu wa kutoa elimu juu ya matumizi ya ardhi kwa kuandaa mikutano mbali mbali katika ngazi za shehia. Aidha idara imeshatoa nakala ya vipeperushi na magazeti.

Agizo la Kumi na Mbili: Kamati imesikitishwa sana na taarifa iliyopatiwa katika Idara ya Ardhi kuwa bajeti waliyopatiwa kwa awamu ya kwanza ni chache sana, ukizingatia na unyeti wa taasisi hizi. Hivyo kamati inaishauri wizara ijipange kuangalia vianzio vyake vyengine vya mapato na ikitokezea idara hizo zikikwama zisaidiwe ili ziweze kutimiza malengo yale.

Mhe. Spika, ushauri utapokelewa na utafanyiwa kazi kadri itakavyowezekana kulingana na upatikanaji wa fedha za matumizi za wizara kutoka serikalini.

Idara ya Ujenzi

Agizo la kumi na tano: Kamati inashauri serikali inapoamua kuanzisha bodi iwe makini kwa kuziendeleza na kuzipatia mahitaji yote ya msingi ili ziweze kufanyakazi kwa ufanisi. Mhe. Spika, wizara inaendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha ili kuzipatia bodi mahitaji yake.

Agizo la Kumi na Nne: Kamati imeishauri bajeti itayopitishwa kwa idara husika yaani ujenzi iingizwe kwa wakati na ipatikane kwa mujibu wa makisio yaliyowekwa. Mhe. Spika, agizo hili linaendelea kutekelezwa na kwa kipindi kilichopita idara ya ujenzi ilipata fedha zote na kuimaliza kazi ya ujenzi wa nyumba za maendeleo za Mpapa kwa wakati na kukabidhi.

Agizo namba Kumi na Tano: Kama kamati imeishauri wizara kuziangalia bodi za wataalamu na bodi ya ukandarasi kwa kuzitengea fungu lake la bajeti ili bodi hizo ziweze kufanya kazi zake. Mhe. Spika, wizara inaendelea na jitihada za kuomba fedha kwa ajili za bodi zake hizi mbili ili ziweze kutekeleza vyema majukumu yake.

Agizo la Kumi na Sita: Kamati inashauri waajiriwe wafanyakazi ambao wataweza kujaza nafasi za waliostaafu na wataalamu wanaohitajika. Mhe. Spika, wizara tayari imeshapeleka maombi ya kupatiwa watumishi Wizara ya Utumishi na Kazi kwa mazingatio.

Mamlaka ya Mji Mkongwe

Agizo la Kumi na Saba: Kamati imesikitishwa na maelezo iliyopewa kuhusiana na bustani ya Forodhani ambayo baadhi ya wafanyabiasha wanakiuka mikataba waliotiliana na mamlaka na kufanya mambo wanayowataka wao kinyume na mikataba inavyosema.
Hivyo kamati inashauri mamlaka kuwachukulia hatua wafanyabiashara wote wanaokiuka masharti na wasiotaka kulipa kodi.

Mhe. Spika, bustani ya Forodhani inayosimamiwa na Bodi ya Bustani ya Forodhani iliyoundwa na Mamlaka ya Mji Mkongwe *Agakhan Foundation* na Baraza la Manispaa. Bodi ya Bustani ya Forodhani ilikutana mwezi wa Agosti mwaka 2013 na kujadili changamoto zinazokabili bustani hiyo. Sambamba na kikao hicho pia bodi ya bustani ya Forodhani imekutana na wafanyabishara wote wa bustani ya forodhani imekutana na wafanyabiashara wote wa bustani ya Forodhani na kujadili kwa pamoja namna ya kutatua matatizo yanayoikabili bustani ya Forodhani.

Aidha bodi imewaajiri polisi jamii wa Mji Mkongwe kwa ajili ya kuongeza ulinzi wa bustani ya Forodhani na kwa sasa matatizo yanayoikabili bustani hiyo yameanza kupungua. Bodi ya Forodhani imechukua hatua ya kuwasimamisha baadhi ya wafanyakazi wa Forodhani kuendelea na biashara zao kwa kutolipa kama inavyosema mikataba yao.

Agizo la Kumi na Nane: Kamati inaishauri mamlaka ijiwekee utaratibu wa kuwa na siku maalumu za vikao na wafanyabishara wa eneo la bustani ya forodhani ili waweze kujadili na kutatua changamoto mbali mbali zinazojitokeza.

Mhe. Spika, Bodi ya Bustani ya Forodhani imeweka utaratibu wa kukutana na wafanyabiashara wa eneo la bustani ya Forodhani mara mbili kwa mwaka. Vile vile vikao huitishwa mara tu inapotokea jambo muhimu la kuzungumza.

Agizo la Kumi na Tisa: Kamati inashauri mamlaka kuwachukulia hatua za kisheria na za kinidhamu baadhi ya wamiliki wa nyumba katika eneo la Mji Mkongwe ambao nyumba zao hubomoka na baadhi hukimbia kukutana na wataalamu wa mamlaka kwa ajili ya kupatiwa ushauri. Hivyo mamlaka inashauriwa iwachukulie hatua wamiliki hao.

Mhe. Spika, mamlaka inaendelea na zoezi lake la kukagua majengo yaliyo katika hali mbaya na kuwashauri wamiliki wa majengo hayo katika kuyakarabati majengo yao. Mamlaka imepokea barua kwa mujibu wa sheria jengo ambalo linalotaka kufanywa hoteli ya kampuni ya ELEWANA kwa kuwa mkaidi wa kufanya ukarabati wa jengo hilo.

Agizo la Ishirini: Mamlaka inashauriwa kutoa elimu ya kina kwa wamiliki wa nyumba za Mji Mkongwe na wananchi wote kwa jumla ili kulinda hadhi za mji huo. Mhe. Spika, ushauri imechukuliwa na unafanyiwa kazi. Mamlaka inaendelea kutoa elimu kama ni shughuli yake ya kawaida.
Agizo la Ishirini na Moja: Kamati imeshauri mamlaka inapokwama katika baadhi ya mambo yake ambayo yanaweza kutatuliwa endapo ikishirikishwa kamati hii ni vyema kwa mamlaka kushirikiana na kamati kwa lengo la

kuondoa matatizo hayo. Mhe. Spika, ushauri umepokelewa mamlaka tayari imejipanga kwa kushirikiana na kamati hii.

Agizo la Ishirini na Mbili: Kamati inazidi kusisitiza umuhimu wa usafi katika maeneo yote ya Mji Mkongwe. Hivyo kamati inaiagiza mamlaka ishirikiane na Baraza la Manispaa katika kuhakikisha suala la usafi katika maeneo hayo linatekelezwa.

Agizo la Ishirini na Tatu: Kamati inaishauri mamlaka isikubali kwa kulazimishwa kuzipitisha ramani ambazo zinakwenda kinyume na sheria za mamlaka. Mhe. Spika, ushauri umepokelewa na kufanyiwa kazi kama kamati ilivyoagiza.

Agizo la Ishirini na Nne: Kamati inaishauri Mamlaka ya Mji Mkongwe ikutane na Mamlaka ya Maji (ZAWA) ili waweze kukubaliana na kulipatia ufumbuzi tatizo la maji linalowakabili wananchi katika maeneo hayo na wafanyabiashara katika eneo la Bustani ya Forodhani.

Mhe. Spika, Mwenyekiti wa Bodi ya Bustani ya Forodhani amekutana na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maji (ZAWA) na kukubaliana juu ya njia ya kuyapatia ufumbuzi matatizo ya maji yanayowakabili wananchi ndani ya Mji Mkongwe na kwa ajili ya huduma ya maji katika bustani ya Forodhani.

Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Makaazi

Agizo la Ishirini na Tano: Mhe. Spika, wazo la kufuta *Rent Restriction Act* endapo tukianzisha shirika la nyumba. Wazo hili limepewa umuhimu na linafanyiwa kazi.

Agizo la Ishirini na Sita: Kamati imeshauri kuwa iwapo Shirika la nyumba la Zanzibar litaanzishwa ni vyema serikali ili liweze kufikia maazimio yatakayowekwa na maendeleo ya shirika yaweze kuonekana.

Mhe. Spika, ushauri huu umepewa umuhimu katika uundaji wa Rasimu ya Sheria ya Shirika la Nyumba. Rasimu iliyopo ambayo bado inaendelea na mchakato wa kufikia sheria kamili imeainishwa kwa uwazi majukumu ya shirika na mipaka ya maamuzi kiutendaji bila ya kuingiliwa na serikali.

Agizo la Ishirini na Saba: Kamati inashauri kuwa jitihada za makusudi zichukuliwe kwa upande wa Pemba na kupitia ripoti hii kamati inataka kujua agizo lake lililotolewa katika ripoti iliyopita kwa kutafutwa kwa gari ya kunyonyea maji machafu limefikia wapi.

Wizara imechukua jitihada za kutafuta gari ya kufyonzea maji machafu na hivi sasa tayari inaangalia makubaliano na Baraza la Manispaa la kupatiwa gari ili liweze kufyonza maji machafu kila itakapohitajika. Gari hii ipo Baraza la Manispaa.

Mamlaka ya Maji

Agizo la Ishirini na Nane: Kutokana na ziara ya kuitembelea Mamlaka ya maji safi na maji taka jijini Arusha. Kamati inaishauri mamlaka ya serikali kwa ujumla iyafanyie kazi yote ambayo yanawezekana kwa sasa ili kuwezesha mamlaka ili kupiga hatua na kupunguza tatizo la ukosefu wa huduma hapa nchini.

Agizo tumelichukua na tunaahidi ndani ya Baraza lako kwamba yale yote tuliyojifunza kutoka Arusha tutayafanyia kazi kadri ya uwezo wetu na uruhusu ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa kazi zetu na kupunguza tatizo la ukosefu wa maji nchini.

Agizo la Ishirini na Tisa: Kamati imegundua kwamba baadhi ya visima vinashindwa kuendeshwa kutokana na ukofesu wa huduma ya uhakika ya umeme. Hivyo kamati imeishauri Mamlaka ya maji ishirikiane na Shirika la umeme ili kuondoa tatizo hilo ambalo linasababisha baadhi ya maeneo kukosa huduma ya maji kwa uhakika.

Mhe. Spika, tatizo la umeme kwa kiasi kikubwa limepungua kutokana na kuimarika kwa huduma za umeme.

Agizo la Thalathini: Kamati imependelekeza kwamba kila kwenye visima vya maji wanaoshughulikia visima vya maji wapewe vitendea kazi vya uhakika vikiwemo *radio call* kwa ajili ya kurahisisha mawasilino pale linapotokea tatizo lolote katika visima hivyo.

Agizo la Thalathini na Moja: Kamati inaishauri mamlaka ihakikishe kuwa inahifadhi na kuyadhibiti maeneo yote ya vyanzo vya maji hasa katika Kiashangwe ambalo lina maji mengi. Hivyo kamati inashauri eneo hilo lidhibitiwe kwa kujenga uzio ili kuepusha uvamizi.

Kwa upande wa kulinda na kuhifadhi eneo la Maji. Mamlaka ya maji inaendelea na jitihada hizo kwa kupima na kujenga uzio pamoja na kutafutia hatimiliki maeneo mbali mbali ya vyanzo vya maji. Kuhusu eneo la Kiashangwe hilo tumelichukua na kulifanyia kazi kadri hali itakaporuhusu.

Agizo la Thalathini na Mbili: Kamati ilisikitishwa sana na tukio la kuvuja kwa maji katika eneo la Kiashangwe hasa ukizingatia kuwa tatizo hilo halina gharama kubwa ya kutengenezwa. Tatizo hilo kamati imesema kuwa halitajitokeza tena.

Agizo la Thalathini na Tatu: Mamlaka inashauriwa izidishe juhudi za kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi juu ya kulipia huduma ya maji. Aidha kama kuna nafasi za ajira mpya mamlaka na serikali kwa jumla iwaaangalie wale vijana wanaojitolea kulinda katika vituo vya maji. Juhudi ya kutoa elimu kwa wananchi juu ya uchangiaji wa maji inaendelea kupitia redio, magazeti, *Television* pamoja na uhamasishaji wa matumizi bora ya huduma ya maji kwa maeneo mbali mbali Unguja na Pemba.

Shirila la Umeme

Agizo la Thalathini na Nne: Kamati inashauri wizara ilisaidie Shirika la Umeme kuwasimamia wadaiwa sugu sasa taasisi za serikali zenye madeni makubwa ili ziweze kulipa madeni yao.

Agizo la Thalathini na Tano: Kamati inazidi kusisitiza ushauri wake wa mara kwa mara kwa shirika kuviweka karibu vituo vya kuuzia umeme. Mhe. Spika, limeshakamilisha maandalizi ya kufunga kituo cha Gamba na Makunduchi ambapo kwa sasa huduma za kiufundi na ununuzi wa umeme kwa mita za kawaida umeshaanza na hatua za kuviwezesha vituo hivyo kutoa huduma kwa mita za TUKUZA zinaendelea.

Agizo la Thalathini na Sita: Kamati imewashauri kuwa wananchi wote wanaojenga katika maeneo ambayo yamepita nyaya za umeme na maeneo hayo yameshalipiwa fidia wachukuliwe hatua za kisheria ili kuepusha hasara kubwa ambayo inaweza kutoa.

Agizo la Thalathini na Saba: Kamati inalishauri Shirika liwe na utaratibu wa kukutana mara kwa mara na wafanyakazi wake na kusikiliza kero mbali mbali za wafanyakazi wake ili zile zinazoweza kurekebishwa kwa haraka zirekebishwe. Jambo ambalo litapelekea kuwa na uhusiano mzuri baina ya viongozi wa juu na wa ngazi ya chini na hatimaye wafanyakazi hao wafanye kazi kwa ufanisi zaidi. Kamati inasisitiza kuwapatia fursa za masomo hasa wafanyakazi wa kisiwani Pemba jambo ambalo litapelekea wafanyakazi hao kuongeza ufanisi wa kazi.

Idara ya Nishati na Madini

Agizo la Thalathini na Nane: Kamati inaishauri wizara isaidie idara kulipatia jengo la kisasa ikiwezekana ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Tayari Idara ya Nishati na Madini imeshakabidhiwa jengo lililokuwa la Shirila la Umeme. Idara imo katika jitihada ya kulifanyia matengenezo jengo hilo ili liweze kuwa na hadhi ya kiofisi.

Agizo la Thalathini na Tisa: Kamati inatoa ushauri kuwa wataalamu wote wa masuala ya Nishati waenziwe na wapatiwe mishahara ya kuridhisha ili waweze kukaa na kufanya kazi hapa nchini kwa manufaa ya nchi yetu.

Agizo la Arobaini: Kamati inapongeza kwa kukubaliana na wazo la kamati na kushirikiana na Taasisi za *ZASEA* na idara yenyewe imeongezea kwa kushirikisha Chuo cha Karume katika kutekeleza majukumu yake kwa lengo la kuimarisha sekta ya Nishati.

Hitimisho

Baada ya kutoa maelezo hayo naomba kwa mara nyengine tena kukushukuru wewe binafsi pamoja na Wajumbe wote wa Baraza lako hili Tukufu, kwa kunisikiliza kwa umakini na utulivu mkubwa.

Vile vile namshukuru Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Mawasiliano na Ujenzi kwa ushauri na miongozo wanayoendelea kutupatia katika utekelezaji wa majukumu yetu.

Ni matumaini yangu kwamba Wajumbe wameyaelewa maelezo niliyoyatoa kuhusiana na utekelezaji wa maagizo ya kamati ya Mawasiliano na Ujenzi katika ripoti yao ya mwaka 2012/2013. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaendelea kuchangia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano naomba nitoe taarifa kidogo tu.

Jana nilikuwa napigiwa simu na watu mbali mbali wakitaka kujua hali ya afya ya Mhe. Haroun Ali Suleiman Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi ya Umma inaendeleaje. Na katika simu ambazo nilikuwa napigiwa kutaka kujua hali yake ndani yake mlikuwa na taarifa za kutatanisha, kiasi kwamba na mimi ikabidi nijaribu kutafuta taarifa.

Hatimaye tukakubaliana na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ili kabla Waheshimiwa Wajumbe hawajauliza suala hilo basi atoe taarifa rasmi juu ya hali ya ndugu yetu, mwenzetu, Mhe. Haroun Ali Suleiman.

Kwa hivyo, naomba kuchukua nafasi hii kumkaribisha Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ili kutoa taarifa juu ya hali ya maendeleo ya afya ya mwenzetu Mhe. Haroun Ali Suleima. Karibu Mheshimiwa. (*Makofi*).

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kwa dhati kwa kunipa nafasi hii ya kutoa taarifa fupi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Waheshimiwa wa Baraza lako tukufu na wananchi kwa jumla kuhusu hali ya afya ya Mhe. Haroun Ali Suleiman, Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma.

Mhe. Spika, Mhe. Haroun Ali Suleiman alianza kuumwa tarehe 5 Januari, 2014. Baada ya kupimwa katika hospitali yetu ya Mnazi Mmoja ilionekana ahamishiwe *Muhimbili Hospital* kwa kupata vipimo zaidi. Kutokana na baadhi ya vipimo kutopatikana Muhimbili. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliamua kumsafirisha kumpeleka Afrika ya Kusini kwa ajili ya kupata vipimo hivi. Kama kawaida yetu ilikuwa tumsafirishe kumpeleka India, lakini kutokana na maelekezo ya madaktari na kutokana na hali aliyokuwa nayo Mhe. Haroun, asingeweza kumudu masafa marefu ya kutoka Dar es Salaam hadi India. Na hivyo ndivyo Serikali ilipoamua kumsafirisha kumpeleka Afrika ya Kusini kwa ajili ya kupata vipimo hivyo na pia kupata matibabu.

Baada ya kufika Afrika ya Kusini na madaktari kumfanyia vipimo ilionekana kuwa ni lazima afanyiwe upasuaji. Na alifanyiwa upasuaji huo tarehe 14 Januari, 2014. Upasuaji ambao ulikwenda vizuri na wa mafanikio makubwa.

Hivi sasa Mhe. Spika, hali ya Mhe. Haroun Ali Suleiman inakwenda vizuri na tayari ameshaanza kufanya mazoezi. Juzi tarehe 1 Februari, 2014 niliongea na Balozi wetu aliyepo Afrika ya Kusini, Mhe. Radhiya Msuya ambaye alinihakikishia kuwa hali yake ilikuwa inakwenda vizuri. Na jana mimi binafsi tena niliongea na mtoto wake Ndugu Ali Haroun ambaye naye alinihakikishia na huenda leo nikaongea na Maalim Haroun mwenyewe.

Mhe. Spika, ningewaomba sana wananchi waepukane na uvumi ulioenea kuwa Maalim Haroun amefariki. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inawathibitishia wananchi wote kuwa Maalim Haroun ni mzima na mwenye afya njema.

Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Spika: Mhe. Makamu wa Pili wa Rais nakushukuru sana. Na naamini majibu yalikuwa magumu kuweza kuwajibu wananchi waliokuwa wananipigia simu, na wakanipa taarifa za kutatanisha, na wakataka niwathibitishie hali inaendeleaje. Nakushukuru sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza tunamshukuru *Allah* kwa kutupa uhai, uzima na *tawfiyq* ya kufika hapa. La pili, kabla sijaanza napenda nichukue nafasi hii vile vile kuzidi kumuombea dua ndugu yetu Mhe. Haroun Ali Suleiman, Mwenyezi Mungu ampe afya njema, amnyanyue na aweze kuja kufanya kazi pamoja katika kipindi kifupi kijacho tukijaaliwa *inshaallah.*

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba sasa niwasilishe mbele ya Baraza lako tukufu utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Mawasiliano na Ujenzi kutoka Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ya mwaka 2012/13 kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako tutakwenda Idara na Idara na Mashirika kama ambavyo itaoneshwa katika *paper* yetu.

Kwanza tunaanza na Idara ya Usafiri na Leseni. Napenda kutoa shukrani za dhati kwa Kamati iliyofanya kazi hii ambayo bila shaka sasa hivi imebadilika. Na nawashukuru Wajumbe wote ambao wamekwenda katika Kamati mbali mbali. Na pia nawashukuru wale ambao wamebaki katika Kamati hii ikiongozwa na Mwenyekiti sasa Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa.

Mhe. Spika, katika Idara ya Usafiri na Leseni, Kamati imeshauri Wizara kusimamia suala la leseni ili ziweze kutolewa na taasisi moja tu ambayo ni Idara ya Usafiri na Leseni ili kuepusha tatizo la leseni feki na kuwezesha Idara kukusanya mapato.

Katika utekelezaji Wizara imechukua hatua mbali mbali katika kuepusha uwezekano wa kutolewa leseni feki ikiwa ni pamoja na kufanya mazungumzo na *operation* za pamoja na Bodi ya Mapato Zanzibar kufuatilia ufumbuzi wa suala hilo.

Aidha, Wizara inakusudia kuimarisha Idara ya Usafiri na Leseni ili iwe na uwezo wa kutengeneza leseni za kuendesha vyombo vya moto hali ya fedha itakaporuhusu.

Agizo la pili kwa Idara hii ilikuwa Kamati inazidi kusisitiza Wizara kuwa pamoja na mipango yake ya kujenga ofisi za kudumu kwa ajili ya taasisi zake,

lakini inasisitiza umuhimu wa Idara hii kusaidiwa kujenga ofisi za kisasa kwa Unguja na Pemba.

Wizara inaelewa juu ya hali mbaya ya jengo la Makao Makuu ya Idara ya Usafiri na Leseni Mwanakwerekwe. Katika kulitafutia ufumbuzi suala hilo Wizara kwa mwaka huu wa fedha imepanga kutumia jumla ya shilingi milioni 50 katika bajeti ya Idara ya Usafiri na Leseni ili kuanza kulifanyia ukarabati jengo hilo. Lakini tatizo la kuingizwa fedha linakwamisha mchakato huo.

Agizo la tatu ilikuwa Kamati inasisitiza kwa Idara hii kuwa makini sana na suala zima la ukaguzi wa magari na kuwadhibiti baadhi ya watendaji ambao hutumia nafasi zao kupasisha gari kinyume na utaratibu.

Katika utekelezaji; Wizara imekuwa ikiwakumbusha watendaji wake majukumu yao na kutekeleza kazi zao kwa mujibu wa Sheria ya Usafiri Barabarani. Idara itaendelea kuwasimamia na kuwakumbusha watendaji wake taratibu za ukaguzi kama ilivyoshauriwa na Kamati ya Baraza la Wawakilishi, na itawachukulia hatua kali wale wote watakaobainika kukiuka taratibu.

Agizo la nne kwa Idara hii, Kamati ilisikitishwa na malalamiko yaliyotolewa na baadhi ya watendaji wa Idara ya kuwa kuna baadhi ya wakubwa hutumia vyeo vyao isivyotakiwa kwa kuamrisha jamaa zao wapewe leseni au wapasishiwe gari. Hivyo Kamati inaishauri Idara kufanya kazi kwa kufuata taratibu ilizojipangia.

Wizara imekuwa ikikabiliana na changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na baadhi ya viongozi kulazimisha jamaa zao kupatiwa leseni au wapasishiwe gari. Hata hivyo, Wizara itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Nam. 7 ya mwaka 2003 yaani *Road Transport Act* kwa kuhakikisha kuwa kanuni na Sheria za Usafiri Barabarani zinatekelezwa ipasavyo.

Agizo la tano kwa Idara hii, Kamati inazidi kusisitiza na kukumbusha agizo lake la kuitaka Wizara kuiboresha Karakana ili iweze kujiendeleza kutokana na mapato yatakayopatikana. Aidha, Kamati imesikitishwa na taarifa kuwa Wizara chache tu za Serikali ambazo huitumia Karakana ya Chumbuni kwa ajili ya matengenezo ya magari ya Serikali. Hivyo Kamati inaiomba Wizara iziandikie Wizara nyengine kwa maandishi kuwakumbusha umuhimu wa Wizara zao kuitumia Karakana ya Serikali.

Utekelezaji. Karakana Kuu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inakabiliwa na changamoto kadhaa. Hata hivyo, Wizara imo katika mchakato wa kutafuta wawekezaji wa uhakika ambao Serikali itaingia ubia wa kuiendesha Karakana hiyo.

Mhe. Spika, tunaingia Shirika la Meli na Uwakala. Agizo la Kamati namba moja. Kamati ilipotembelea katika Shirika ilipata taarifa kuwa mkataba wa utengenezaji wa meli mpya bado haujasainiwa. Hivyo kupitia ripoti hii Kamati inaiomba kupatiwa maelezo ya kutosha juu ya suala la ununuzi wa meli na hadi sasa suala lilipofikia.

Utekelezaji. Kuhusu suala la meli mpya tayari mkataba umeshatiwa saini tokea tarehe 26 Julai, 2013 huko nchini Korea ya Kusini baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Kampuni ya *DAEWOO*. Hatua za awali za matengenezo ya meli hiyo zinaendelea na inategemewa kukamilika mnamo mwezi wa Februari, 2015.

Agizo namba mbili. Kamati inaunga mkono wazo la Shirika kutotaka kubinafsishwa kwa suala zima la uwakala kutokana na umuhimu wake ikizingatiwa kuwa ndio nguzo moja wapo kubwa ya mapato ya Shirika la Meli. Na uwepo wa Shirika hilo hadi leo unatokana na shughuli za uwakala.

Utekelezaji. Wizara pamoja na Shirika zinakubaliana na maelekezo ya Kamati, na hiyo sasa ndio sababu ya Shirika kukataa kubinafsishwa kwa uwakala. Kwani pia tukijifunza kutokana na wenzetu wa Tanzania Bara *NASACO* baada ya kubinafsishwa Serikali imepoteza fedha nyingi kutokana na kuwa na mawakala wengi wa meli za kigeni ambao miongoni mwao wanasadikiwa walikuwa ni wageni kutoka nchi za nje wakiwa na uhusiano na makampuni ya meli wanayoyafanyia uwakala.

Agizo namba tatu. Kamati inazidi kusisitiza umuhimu wa kujengwa ofisi ya Shirika Tawi la Dar es Salaam kutokana na ushindani wa kibiashara uliopo, ili Shirika lizidi kujitangaza na kujiongezea mapato.

Shirika kwa kushirikiana na Wizara liko mbioni kufuatilia upatikanaji wa eneo jengine la kujenga ofisi baada ya eneo tulilokuwa nalo la ofisi kutakiwa kuvunjwa kwa ajili ya upanuzi wa barabara ya mabasi yaendayo kwa kasi. Na kwa taarifa ni kuwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alipofanya ziara ya kikazi katika Taasisi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar aliahidi kulishughulikia suala la eneo. Kwa sasa tupo katika hatua nzuri ya kulipata.

Kuhusu suala la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Wizara kwa kushirikiana na Shirika tunajiandaa kukutana na uongozi wake ili kuweza kulizungumza kwa kina suala hilo.

Mhe. Spika, Shirika la Bandari. Agizo la mwanzo ilikuwa Kamati inaishauri Wizara kulisaidia Shirika kupata wafadhili watakaosaidia fedha kwa ajili ya

ujenzi wa bandari ya Mpigaduri ambayo ndio itakuwa suluhisho la baadhi ya changamoto zilizopo hivi sasa katika Bandari ya Malindi.

Utekelezaji. Serikali inaendelea na juhudi za kuzungumza na washirika wa maendeleo mbali mbali kwa ajili ya kupata fedha za kugharamia ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri. Juhudi hizo hivi karibuni zilizaa matunda ambapo tayari kampuni moja imejitokeza na kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa bandari hiyo. Ripoti ya upembuzi yakinifu imewasilishwa Serikalini kwa kupitiwa na kutolewa uamuzi. Wizara ina matumaini makubwa kwamba ripoti hiyo itawezesha fedha kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri kupatikana, ili ujenzi uanze na kuipunguzia mzigo bandari yetu ya Malindi.

Agizo la pili. Kamati inaishauri Wizara ilisaidie Shirika la Bandari kufanya makubaliano na taasisi ambazo zinadaiwa na Shirika, ili taasisi hizo na Shirika wawe na makubaliano mapya ambayo yataondoa madeni yaliyopo hivi sasa na taasisi hizo.

Utekelezaji. Wizara kwa kupitia Shirika inaendelea kuyafuatilia madeni inayodai katika taasisi mbali mbali zikiwemo Taasisi za Serikali kama Wizara ya Fedha, KMKM, Shirika la Meli na Uwakala, lililokuwa Shirika la Manukato. Wizara kupitia Shirika inawasiliana na taasisi hizo ambazo bado hazijakubali kulipa madeni yao. Menejimenti ya Shirika imeliwasilisha suala hili katika vikao vya Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika na kutolewa maamuzi kuwa Shirika limuandikie Mwenyekiti wa Tume Maalumu iliyoteuliwa na Serikali kuangalia utendaji mzima wa Shirika la Bandari yakiwemo masuala ya utawala na utumishi, uendeshaji na fedha na masuala mengineyo. Tume hiyo inaongozwa na Makamu wa Pili wa Rais na inajumuisha Mawaziri kadhaa wa Serikali. Uongozi wa Shirika tayari umemuandikia barua Mwenyekiti wa Tume hiyo na hivi sasa kinachosubiriwa ni muongozo wake.

Agizo namba tatu kwa Shirika. Kamati inazidi kusisitiza umuhimu wa Shirika la Bandari kupatiwa eneo la Bwawani kwa ajili ya kuweka makontena na kupunguza mzigo mkubwa wa makontena yanayosongamana katika eneo la Malindi hivi sasa.

Utekelezaji. Shirika la Bandari tayari limeshapatiwa na linaendelea kulitumia eneo la Bwawani kwa ajili ya kuwekea makontena matupu katika jitihada za kupunguza mrundikano wa mizigo bandarini. Shirika limeruhusiwa na Serikali kulitumia eneo hilo kwa muda mpaka hapo eneo hilo litakapohitajika kwa matumizi mengine. Aidha, Shirika limekusudia kuongeza eneo la kuhifadhia makontena bandarini kwa kuyavunja mabanda yanayotumika

kama ofisi hivi sasa baada ya kukamilika ujenzi wa jengo jipya la ofisi bandarini lililokuwa *Duty Free Shop.*

Agizo namba nne. Kamati inaupongeza uamuzi wa mfanyabiashara mzalendo Bakhressa kwa kuweza kuwekeza kwa kujenga katika Bandari ya Malindi jambo ambalo litasaidia kuweka haiba nzuri ya eneo la bandari na kuwavutia watalii. Pia litaingiza fedha katika Shirika zitakazosaidia kukuza uchumi wa taifa.

Wizara inapokea pongezi za Kamati kwa niaba ya mfanyabiashara aliyefanya ukarabati wa majengo ya eneo la bandarini. Aidha, Wizara inawaomba wananchi kupitia Wawakilishi wao kuyatunza mazingira ya maeneo hayo wakati wanapofanya safari zao ili yaendelee kudumu kwa muda mrefu.

Agizo namba tano. Kutokana na kuzuiwa kutumika kwa jengo la Beit el Ajaib hivi sasa, eneo ambalo lililokuwa likitumiwa na Shirika kwa ajili ya kuweka vifaa vya kuongozea meli, Kamati inasisitiza umuhimu wa matumizi ya vifaa hivyo kila wakati. Hivyo Wizara inashauriwa ifanye juhudi za makusudi kulisaidia Shirika kupata eneo la kudumu ili paweze kujengwa jengo litakalotumika kwa shughuli hiyo. Wizara inashauriana na Shirika kuhusiana na kupatikana kwa eneo muafaka kwa ajili ya ujenzi wa kituo kikuu cha mawasiliano *(signal station).* Hata hivyo, Shirika la Bandari limependekeza eneo la bandari mpya ya Mpigaduri liwe eneo muafaka kwa kujengwa kituo hicho kipya.

Agizo namba sita. Kamati inaishauri Wizara kushauriana na Serikali Kuu ili waweze kulisaidia Shirika kupata fedha kwa ajili ya ununuzi wa *tag* kutokana na gharama zake kuwa kubwa na Shirika pekee kushindwa kuzimudu.

Utekelezaji. Shirika la Bandari limekamilisha taratibu za manunuzi ya *tag* mpya itakayokidhi mahitaji ya hivi sasa ambapo tathmini ya zabuni zilizowasilishwa na kampuni mbali mbali za nje na ndani ya nchi inaendelea. Shirika tayari limeanza mazungumzo na Benki ya Watu wa Zanzibar ili kupata mkopo wa fedha za kununulia *tag* hiyo ndani ya mwaka huu 2013/14.

Agizo namba saba. Kamati inatoa agizo kuwa maeneo yote ya Shirika la Bandari ambayo hayana hatimiliki Shirika lifanye juhudi ya kuzipatia hatimiliki za maeneo hayo.

Utekelezaji. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Bandari tayari imeanza utaratibu wa kulifanyia kazi agizo hili la kupata hatimiliki za maeneo hayo. Wizara inayohusika na ardhi tayari imeanza kazi za upimaji wa maeneo hayo na taratibu za utoaji hatimiliki zinaendelea kwa maeneo yote ya Shirika. Hati

za eneo la mnara wa Kigomasha, eneo la jengo lililonunuliwa kutoka *PBZ* na nyumba ya kuishi Mkurugenzi wa Tawi la Shirika Pemba tayari zimepatikana na maeneo yaliyobakia taratibu za kupatiwa hati zinaendelea.

Agizo namba nane. Kamati inaishauri Wizara ishauriane na Wizara ya Afya na taasisi nyengine husika kumbana mfanyabiashara ambaye ameleta unga uliokwishaharibika ambapo uko bandarini kuwa mfanyabiashara huyo auondoe unga wake.

Utekelezaji. Makontena ya unga ulioharibika ambayo yalikuwepo bandarini kwa muda mrefu yameshaondolewa tokea mwezi wa Juni, 2013.

Mamlaka ya Usafiri Baharini. Agizo namba moja. Mamlaka ifuatilie mapato yake ya ndani yanayotokana na meli za kigeni kupitia Shirika la Meli ili fedha hizo ziweze kusaidia kutatua baadhi ya changamoto zinazoikabili mamlaka.

Utekelezaji. Mamlaka iliwasilisha suala hili kwa maandishi na kuambatanisha na ankara, yaani risiti za malipo husika katika Shirika la Meli ambao ndio wakala wa meli za kigeni. Na imefikia hatua kwa Shirika la Meli na mamlaka tukashirikiana kukaa katika kikao cha pamoja na wawakilishi wa meli za kigeni tarehe 10 Septemba, 2013. Na wawakilishi hao wamelichukua suala hili na kulipeleka kwa wamiliki wa meli na wamekubaliana kuwa ankara zote za malipo husika zipelekwe moja kwa moja kwa wawakilishi hao na tayari tumeshaanza kufanya hivyo lakini bado baadhi yao hawajalipa.

Agizo namba mbili. Mamlaka kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano iiombe Wizara ya Fedha ipatiwe Mkurugenzi wa Fedha ili ipatiwe ruhusa ya kuitumia akaunti yake. Wizara kwa kushirikiana na mamlaka ililifuatilia suala hili na tayari Mkurugenzi wa Fedha na Utawala amepatikana tangu mwezi Machi, 2013 pamoja na kukabidhiwa hesabu za fedha za kigeni kutoka Wizara ya Fedha tangu Juni, 2013.

Agizo namba tatu. Kamati inaungana na wazo la mamlaka kujaribu kuliondoa tatizo la ulanguzi wa tiketi kwa kushirikisha Polisi Jamii katika zoezi hilo. Kamati inaziomba taasisi zote zishirikiane kikamilifu katika kupiga marufuku ulanguzi wa tiketi.

Utekelezaji. Mamlaka imewashirikisha Polisi Jamii katika kupiga vita ulanguzi wa tiketi. Hata hivyo, imeshindikana kulikomesha suala hilo kwa sababu linajumuisha wadau wengi. Ili kulipatia tiba ya kudumu tatizo hilo mamlaka imeanza kufanya yafuatayo.

Agizo namba moja. Kuzungumza na Manispaa ili kuweza kuviondoa vibanda au miamvuli iliyomo maeneo ya bandarini Malindi.

Agizo namba mbili. Kuwatambua rasmi mawakala wanaouza tiketi kwa masharti kwamba wawe na jengo la ofisi na wapate leseni kutoka mamlaka.

Agizo namba tatu. Kufanya mazungumzo na Mahkama ili kuweza kuitumia Mahkama ya Mwanzo iliopo Manispaa kwa ajili ya kesi za walanguzi wa tiketi.

Agizo namba nne. Kutokana na umuhimu wa mamlaka na unyeti wa shughuli zake ambazo nyingi zinahitaji wataalamu. Kamati imesikitishwa na taarifa kuwa hadi sasa mamlaka katika ulipaji wa mishahara haitumii *scheme of service* iliyojipangia. Hivyo, Kamati inaiomba Wizara iliangalie tena suala hilo.

Utekelezaji. Tangu kuanzishwa kwake hadi sasa mamlaka inatumia *scheme of service* ya Wizara. Hata hivyo, tarehe 6 Septemba, 2013 mamlaka iliingia katika mkataba na Mshauri Mwelekezi kwa kutayarisha muundo wa utumishi kwa ajili ya mamlaka. Kwa sasa tayari Mshauri ameshafanya mahojiano na wafanyakazi wa kada zote akiwemo Mkurugenzi Mkuu. Kazi ya kutayarisha muundo wa utumishi tayari rasimu ya pili imeshawasilishwa kwa uongozi wa mamlaka. Baada ya kukamilika itawasilishwa kwenye Bodi na hatimaye kwa Waziri kwa ajili ya kuidhinishwa na kuanza kutumika. Tunategemea itatumika rasmi kuanzia mwezi wa Februari, 2014.

Agizo namba tano. Kamati inaishauri Wizara izidishe juhudi za kusaidia mamlaka kutengeneza kanuni za uendeshaji pamoja na jitihada zilizokwishachukuliwa.

Utekelezaji. Wizara inashirikiana kwa karibu na mamlaka katika kutayarisha kanuni mbali mbali. Hata hivyo, tatizo la ufinyu wa bajeti linadhorotesha utayarishaji wa kanuni. Hivi sasa kanuni tano zimeshapitiwa na Mhe. Waziri kwa mara ya mwanzo, kanuni mbili ziko hatua ya mwisho ya mapitio, na kanuni moja yaani *Zanzibar Maritime Transport Training and Certification Regulation* ambayo itaiwezesha mamlaka kutoa leseni kwa vyuo vya ubaharia na kuthibitisha vyeti vya mabaharia iko katika hatua za awali. Tunategemea kuwa kukamilika kwa kanuni hii kutatoa fursa kwa vijana wa Kizanzibari kujisomea elimu ya ubaharia hapa Zanzibar na kwa gharama nafuu zaidi.

Agizo namba sita. Mamlaka iweke utaratibu maalumu wa kuwaongoza wamiliki wa meli juu ya kuitunza mizigo ya abiria sehemu maalumu na mwenye meli atakuwa na dhamana iwapo kutapotea mzigo wa abiria.

Utekelezaji. Mamlaka imewawekea wenye meli utaratibu maalumu wa upakiaji wa abiria, pamoja na upakiaji na uhifadhi wa mizigo. Na huwa inawakumbusha wenye meli kwa kuwaandikia barua na kuwaita katika vikao vya pamoja.

Agizo namba saba. Kamati inaiomba Wizara kwa kushirikiana na mamlaka ilifuatilie suala linalofanyika katika Bandari ya Dar es Salaam kuwalipisha abiria pesa zaidi kwa ambao wamechukua mizigo mingi.

Utekelezaji. Kanuni za usalama wa vyombo zinatoa fursa kwa abiria kuchukua mizigo *baggage* miwili yenye uzito wa kilo 10 hadi 15 kwa kila mmoja, na mzigo mmoja mpaka miwili yaani *luggage* usiozidi kilo 40 bila ya kulipa. Iwapo mizigo itazidi uzito uliotajwa hapo juu abiria atalazimika kulipa mzigo huo kutokana na kanuni iliyopo.

Agizo namba nane. Mamlaka itoe elimu kwa wananchi kuhusiana na kazi zake pamoja na abiria kujiepusha kununua tiketi kutoka kwa walanguzi, vile vile kuangalia uwezekano wa kuwepo tiketi za moja kwa moja DAR/ZNZ/PEMBA na kusimamia uundaji wa kamati ndogo ya kudhibiti ulanguzi wa tiketi.

Mamlaka imeshaandaa vipindi mbali mbali kwenye vyombo vya habari vinavyotoa elimu kwa wananchi juu ya taratibu bora za kukata tiketi kwa kitambulisho ili kuepusha ununuzi wa tiketi kutoka kwa walanguzi. Na tayari wenye meli wameshaweka tiketi za moja kwa moja DAR/ZNZ/PEMBA.

Agizo namba tisa. Kamati inaipongeza kwa dhati Kampuni ya Azam kwa uamuzi makini wa kuamua kushirikiana na Serikali na kuifanyia matengenezo Bandari ya Malindi. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa kampuni inakabiliwa na ufinyu wa ofisi, hivyo wameomba wapatiwe eneo la kujenga ofisi hapa Zanzibar. Kamati inaliafiki wazo hilo na imeshauri kuwa eneo lipo basi kampuni hiyo ipatiwe. Wizara imepokea kwa niaba ya Kampuni ya Azam akiwa ni mdai wetu.

Mhe. Spika, sasa tunakuja Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Agizo namba moja, Kamati inaishauri Wizara isaidie mamlaka kupata vifaa vya kuangalia usalama wa abiria na mizigo yaani *x-ray machine.* Mashine hizo ziwe tatu ambazo mbili zitatumika kwa ajili ya kuwakagua abiria wanaosafiri na moja kwa ajili ya mizigo.

Utekelezaji. Wizara inaendelea na juhudi za kupata fedha za ununuzi wa vifaa vya uchunguzi wa mizigo na abiria kwa ajili ya kuimarisha usalama katika Kiwanja cha Ndege cha Abeid Amani Karume. Aidha, Wizara imewasilisha

maombi rasmi Serikalini kwa ajili ya kupatiwa fedha za kuimarisha huduma mbali mbali za kiwanja cha ndege ikiwemo ununuzi wa mashine za *x-ray.* Pia kwa kuzingatia umuhimu wa usalama katika viwanja vya ndege Wizara imejumuisha gharama za mashine za *x-ray* katika ujenzi wake wa jengo jipya la abiria unaoendelea yaani *Terminal II.*

Agizo namba mbili. Kamati ilipotembelea katika mamlaka ilipewa taarifa kuwa ujenzi wa *terminal* mpya ya Uwanja wa Ndege imesimama kutokana na matatizo yaliyojitokeza. Hivyo kupitia ripoti hii Kamati inaomba kupatiwa maelezo ya Wizara kuhusiana na suala hilo na lilipofikia kwa sasa.

Mhe. Spika, ni kweli kuwa wakati Kamati ilipotembelea jengo hilo ujenzi wake ulikuwa umesita kwa muda kutokana na matatizo yaliyojitokeza, yakiwemo tofauti ya ukubwa baina ya jengo na sehemu ya maegesho inavyoendelea kujengwa na Kampuni ya *SOGEA.* Pia jengo kujengwa karibu na njia ya kutulia na kurukia ndege. Serikali baada ya kubaini tatizo hilo ilimuajiri mtaalamu kwa ajili ya kupata ushauri. Ushauri uliotolewa ni kuwa jengo hilo lingeweza kubakia hapo hapo ikiwa yatafanyika marekebisho kwa mfumo wa maegesho ya ndege kwa kuweka ndege kubwa upande wa kusini wa jengo, na zile ndogo kuegeshwa mbele ya jengo. Ushauri huu ndio Wizara imeuchukua na kumtaka Mkandarasi kuutekeleza. Kwa sasa tayari Mkandarasi anaendelea na kazi ya ujenzi wa jengo hilo.

Agizo namba tatu. Kamati inazidi kusisitiza Wizara ilisimamie suala la *airport service charges* irudishwe katika mamlaka yenyewe ili fedha hizo ziweze kuisaidia mamlaka kujiendesha na kutatua matatizo mbali mbali yaliyopo hivi sasa.

Utekelezaji. Wizara imefuatilia madai ya Kamati lakini kutokana na ukweli kuwa mapato ya *service charge* ni sehemu ya mapato yanayotumika kuendesha shughuli za serikali haikuwezekana mapato hayo kupewa mamlaka. Hata hivyo, serikali imeiruhusu mamlaka kukusanya mapato mengine yaliyobakia kwa ajili ya shughuli zao za kuendeshea mamlaka hiyo.

Agizo namba nne

Kamati inakubaliana na ushauri uliotolewa na mamlaka kuwa serikali katika bajeti yake itenge fedha kwa ajili ya *scholarships* kuwasomesha wataalamu wa mambo ya *airport.*

Utekelezaji

Mafunzo ya wafanyakazi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege hufanywa na mamlaka yenyewe. Hata hivyo, pale ambapo panaonekana mahitaji maalum, wizara kupitia mipango yake ya mafunzo kazini huwajengea uwezo zaidi, hivi karibuni mamlaka imewapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi 33 nje na ndani ya nchi.

Aidha, wafanyakazi 2 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya *diploma* na *master degree*.

Agizo Na. 5

Kamati inazidi kusisitiza umuhimu wa kufanya ukarabati uwanja wa ndege wa Pemba. Aidha, kamati inasisitiza mamlaka na wizara kwa jumla wajitahidi kuziondoa changamoto ziliopo katika uwanja wa Pemba ambazo nyengine zimekuwa ni changamoto za muda mrefu.

Utekelezaji

Wizara kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imeendelea na juhudi zake za kufanya ukarabati mdogo mdogo katika kiwanja cha ndege cha Pemba, hadi hapo mradi mkubwa wa kuimarisha kiwanja hicho utakapoanza.

Kwa upande wa uwekaji wa taa Pemba, wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar iliwasilisha serikalini maombi ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya uwekaji wa taa za sehemu ya kurukia ndege ili ziweze kutumika muda wote. Serikali imeshatoa maamuzi ya kuweka taa hizo ndani ya kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014.

Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara (UUB)

Agizo Nam. 1

Katika miradi ya ujenzi wa barabara ambao serikali inapata mikopo, kamati inashauri kuwa gharama za fidia ziingizwe moja kwa moja au kwa njia nyengine yoyote katika thamani ya jumla ya mkopo, ili iwe ni sehemu ya mkopo huo kwa ajili ya kufanya utekelezaji wa mradi, ujenzi usichelewe kutokana na kukosekana kwa malipo ya fidia.

Utekelezaji

Kwa kawaida wafadhili wetu wengi ukitoa changamoto ya *millenium* ya Marekani wamekuwa wakitoa masharti ya kuitaka serikali kulipa fidia za vipando, nyumba na kuondosha huduma za kijamii zilizokuwepo pembezoni mwa barabara. Hali hii imepelekea miradi kuchelewa kumalizika na kuongezeka gharama za ujenzi, kwa vile serikali inakuwa haina uwezo wa kulipa fidia hizi kwa wakati mmoja.

Kwa kuzingatia umuhimu wa suala hili, wizara imeanza kuwaomba wafadhili kuangalia uwezekano wa kuingiza gharama za fidia ndani ya mikopo au ruzuku wanazotoa ili kuepusha ucheleweshaji wa ujenzi na muongezeko wa gharama. Benki ya Maendeleo ya Afrika walitueleza kuwa sera na sheria zao zinazuia kuingiza fedha za fidia kwenye mikopo wanayotoa.

Serikali inachukua ushauri huu mzuri na kuahidi kuwa tutaendelea kuwashauri washirika wa maendeleo kulikubali suala hili.

Agizo Nam. 2

Kamati inashauri kuwa serikali iwe na usimamizi madhubuti katika miradi ya ujenzi utakaowakilisha vyema maslahi ya serikali kwa lengo la kuifanya miradi hiyo ya ujenzi imalizike kwa wakati na kwa kiwango kinachohitajika kwa mujibu wa mkataba baina ya mjenzi na serikali.

Utekelezaji

Wizara inaupokea ushauri wa kamati, hata hivyo tayari wizara imekuwa na utaratibu ambapo miradi yote ya ujenzi wa barabara kabla ya kuanza kwake, wizara huajiri mshauri kwa ajili ya kusimamia ujenzi wake.

Aidha, wizara inateuwa mhandisi yaani *engineer* mkaazi wake mmoja kuwa ni mratibu wa mradi husika.Washauri hawa pamoja na mtaalamu wetu wanakuwepo kwa muda wote wa ujenzi kwa ajili ya kumsimamia mkandarasi kuhakikisha kuwa kazi wanazozifanya ni kwa mujibu wa mikataba inayosainiwa.

Mshauri anatakiwa kuzingatia maslahi ya muajiri wake ambapo moja ya maslahi hayo ni kuona kazi ya ujenzi wa barabara zinamalizika kwa wakati na kwa gharama ndogo iwezekanavyo.

Agizo Nam. 3

Kamati inaishauri idara iandae mkakati madhubuti ya kuzilinda barabara zake kwa kuwachukulia hatua kali wale wote wanaoharibu miundombinu ya barabara, wakiwemo wale wote wanaolipwa fidia na wanarudi tena kujenga pembezoni mwa barabara.

Aidha, kamati imesikitishwa na hatua zinazochukuliwa na baadhi ya wananchi wanaojenga matuta kiholela pasi na kufuata ushauri wa kitaalamu kutoka kwa idara. Hivyo, kamati inaiagiza idara itoe elimu kwa wananchi juu ya uwekaji wa matuta wunaofanywa na vigezo vinavyotumika kuweka matuta kitaalamu.

Utekelezaji

Wizara tayari imechukua hatua ya kuirekebisha sheria yake ya barabara kwa kuainisha maeneo ya hifadhi ya barabara pamoja na kurekebisha viwango vya adhabu kwa makosa mbali mbali ya uharibifu wa barabara. Mara tu sheria hiyo itakapoanza kutumika ambapo imeshapitishwa na Baraza letu la Wawakilishi, tunaamini kuwa makosa ya aina hiyo yatapungua kwa kiasi kikubwa.

Idara imepokea ushauri huo. Aidha, kwa taarifa ni kwamba hivi sasa wananchi wengi tayari wameanza kuelewa utaratibu mzima wa masuala ya uwekaji matuta. Hivi sasa wananchi wengi kupitia viongozi wao wa majimbo na Shehia wamekuwa wakifika idarani wanapokuwa na tatizo la kutaka kuweka matuta maeneo yao kwa kupatiwa ushauri wa kitaalamu.

Agizo la 4

Kamati inazidi kusisitiza kuwa *road reserve* wakati inapojenga barabara zake, jambo ambalo linasaidia sana kuzilinda barabara.

Utekelezaji

Tayari wizara imeanza kuchukua hatua kwa kutenga bajeti maalum kwa ajili ya kuweka *road reserve poles*, yaani vipigi au viguzo vya kuonesha maeneo ya barabara ya akiba. Aidha, zipo barabara ambazo tayari nguzo hizo zimeshawekwa kwenye mradi wa barabara Kaskazini Pemba. Utaratibu huo utaendelea kwa barabara zilizobakia.

Agizo Nam. 5

Kamati inashauri kuwa wakandarasi wanapopewa tenda ya ujenzi wasisitizwe kuwa wanapomaliza wahakikishe wanaweka mazingira mazuri kwa kuyafukia au kuweka sawa maeneo yote wanayotumia kwa ajili ya uchimbaji wa vifusi. Wizara imepokea ushauri na itaongeza jitihada za kusimamia jambo hilo.

Kuhusu maagizo na maoni yaliyoelekezwa kwa mashirika, mamlaka na kampuni zilizo chini ya usimamizi wa moja kwa moja ya Serikali ya Muungano wa Tanzania, ninapenda kuliarifu Baraza hili kuwa maagizo hayo na ushauri waliotoa kamati tumewasilisha kwa wahusika wote na wameupokea. Ni matumaini ya wizara kuwa maagizo yaliyotolewa na kamati watayatekeleza na yale maoni watayazingatia kwa nia ya kutoa huduma bora hapa nchini.

Kuhusu maoni yaliyotolewa kuhusu *ZANTEL*, ninapenda kuliarifu Baraza lako kuwa maoni na maagizo hayo pia yamewasilishwa kwa kampuni hiyo kwa kuyafanyiwa kazi.

Mhe. Spika, baada ya hayo ninapenda nitoe shukurani zangu za dhati tena kwa usikivu wa Wajumbe wote na niishukuru sana kamati iliyopita ambayo ilitayarisha maagizo haya na kuipokea kamati iliopo na maagizo yao, na utekelezaji utaendelea.

Ninakushukuru sana Mhe. Spika. (*Makofi*).

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba wa mbingu na ardhi kwa kutuwezesha siku hii ya leo kuendelea kufika hapa kuendelea na taratibu zetu ambazo tumejipangia.

Lakini kabla ya hapo Mhe. Spika, na mimi niungane na taarifa ambayo Makamu wa Pili wa Rais ameisoma hapa juu ya hali ya Maalim wetu, mzee wetu na waziri wetu Mhe. Haroun Ali Suleiman na *Inshaallah* huko aliko Mwenyezi Mungu amjaalie apate afya zaidi na aweze kurudi, ili kushirikiana kwa pamoja tuendeleze gurudumu la maendeleo la nchi yetu.

La pili, ninapenda kuchukua fursa hii kutoa pongezi maalum na pongezi za kipekee kutokana na ushindi alioupata ndugu yetu Mahmoud Thabit Kombo Jecha katika uchaguzi uliofanyika jana maeneo ya Kiembesamaki. Uchaguzi ule unaendelea kudhihirisha jinsi ya wananchi, wanachama na wapenzi wote

wa Zanzibar wanavyoendelea kukubaliana na sera za Chama cha Mapinduzi katika kuongoza taifa hili. (*Makofi*).

Baada ya hayo sasa Mhe. Spika, naomba niendelee na kazi ambayo imenileta hapa.

Mhe. Spika, nianze kwa salamu kwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu ambao kwa rehma na ukarimu mkubwa wa Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha sote kwa pamoja kukutana hapa leo, tukiwa wazima na afya tele ili kuonesha kuthamini hili, ninasema *alhamdullah*.

Mhe. Spika, baada ya kumshukuru *Allah* ninaomba sasa nikushukuru wewe kwa mashirikiano na ushauri mwema unaonipatia mimi pamoja na Wajumbe wenzangu wa kamati. Ushauri ambao umetuwezesha na kuniwezesha mimi kuongoza kamati hii vyema kabisa na kufanya nifikie malengo yaliyokusudiwa na kuwezesha kufanya majukumu yake yaliyowekwa kwa mujibu wa Kanuni ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, pia ninapenda nichukue nafasi hii ya kipekee kuwapa pole wale wote Waheshimiwa waliopoteza vipenzi vyao ambavyo vimetangulia mbele ya haki. *Allah* atawapa subra na moyo katika kipindi hiki kigumu cha majonzi lakini wakumbuke kwamba wao wametangulia na sisi tupo nyuma yao.

Mhe. Spika, rambirambi za pekee pia ninazipeleka kwa wananchi wa Zanzibar ambao wamefikwa na maafa ya kupoteza jamaa zao kutokana na ajali ya boti ya Kilimanjaro iliyotokea katika visiwa vyetu hivi karibuni. Ninawaombea wote waliotangulia mbele ya haki *Allah* awape mapumziko mema na ndugu zao na jamaa wote awape subra kwa mitihani iliyowafika.

Mhe. Spika, haitokuwa ubinadamu kusimama hapa leo nikatoa maelezo yangu kwa niaba ya kamati bila ya kueleza masikitiko niliyonayo kutokana na maafa ya moto waliyopata wananchi wa Wilaya ya Micheweni Pemba, hasa kwa kuwa kamati yangu ilikwenda kujionea hali halisi ilivyokuwa. Hivyo basi, ninachukua nafasi hii kuwafariji na kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu awape subra na uvumilivu.

Mhe. Spika, baada ya kutoa shukurani na pole kwa wanaostahiki, sasa naomba nielekee katika lengo ambalo limenifanya nisimame mbele ya hadhara hii tukufu ambayo ni kusoma muhtasari wa ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi. Hivyo basi, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Wajumbe wa kamati hiyo naomba kuusoma muhtasari huo kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi iliopo sasa imeanza na ziara yake ya mwanzo tarehe 13 May, 2013 baada ya kuteuliwa na wewe Spika baada ya kamati iliyokuwepo kumaliza muda wake.

Mhe. Spika, uteuzi wa Wajumbe wa kamati hiyo uliufanya kwa mujibu wa Kanuni Nam. 107 (1) na (2) ya Kanuni ya Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2012. Uteuzi ambao umepelekea kupatiwa kamati yenye Wajumbe 7, ambao naomba niwataje pamoja na makatibu wake kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Mahmoud Muhamed Mussa	-	Mwenyekiti
2. Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Ismail Jussa Ladhu	-	Mjumbe
4. Mhe. Marina Joel Thomas	-	Mjumbe
5. Mhe. Mahamed Haji Khalid	-	Mjumbe
6. Mhe. Salma Mohamed Ali	-	Mjumbe
7. Mhe. Hussein Ibrahim Makundu	-	Mjumbe
8.Ndg. Latifa Saleh Suleiman	-	Katibu
9.Ndg. Saad Othman Saad	-	Katibu

Mhe. Spika, itakumbukwa kwamba Kanuni za Baraza la Wawakilishi zinaeleza kwamba Wajumbe wa kamati watamudu katika kamati waliyoteuliwa kwa muda wa miaka miwili na miezi sita kuanzia siku ya uteuzi wao. Hivyo basi, baada ya kupita muda na kamati iliyopita kumaliza muda wake, kamati iliopo ilianza utekelezaji wa majukumu yake kama ilivyoainishwa katika Kanuni ya 111 (a) mpaka (h) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2012.

Mhe. Spika, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi inatekeleza majukumu yake hasa kwa kusimamia wizara mbili za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambazo ni Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Spika, kwa kuwa kamati hii ni mpya katika kusimamia wizara hizi ililazimu kutembelea taasisi, idara na maeneo yote ambayo yapo chini ya wizara hizi mbili kwa malengo ya kuvitambua. Hivyo basi, inaaminika nikitamka kwamba kamati ilikuwa na kazi nzito ya kuhakikisha kwamba inapata maelezo na ufafanuzi wa kina kila shughuli inayokusudiwa kufanywa na wizara hizi mbili kwa lengo la kutoa ushauri na maelekezo yanayofaa.

Mhe. Spika, kwa muda nilionao kusoma muhtasari huu ni mchache, sasa naomba nianze maelezo yangu kwa ufafanuzi wa mambo muhimu ambayo kamati inaona katika wizara zake ilizoanza mwezi wa Mei, 2013 na kumaliza mwezi wa Januari, 2014 kama ifuatavyo:-

WIZARA YA ARDHI, MAKAAZI, MAJI NA NISHATI

Mhe. Spika, Kamati ilipata nafasi ya kuzikagua na kupata maelezo ya shughuli zinazofanywa na taasisi mbali mbali zilizopo chini ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Kiujumla wizara inahusika na usimamizi wa utoaji wa huduma katika sekta ya ardhi, sekta ya makaazi, sekta ya maji na sekta ya nishati.

Mhe. Spika, katika kutekeleza majukumu yake Kamati imegundua mambo yafuatayo ambayo iliyatolea ushauri na maagizo mbali mbali kama ifuatavyo:-

Shirika la Umeme

Mhe.Spika, katika kusimamia Shirika la Umeme (*ZECO*), Kamati imegundua kuwepo kwa changamoto kubwa zinazoziandama shirika hilo, hali inayopelekea shirika kukosa maelezo na maendeleo ya kujiendesha na vile vile kuweza kujiendesha kwa hasara. Changamoto kubwa inayoipa wakati mgumu kamati ni madeni inayodaiwa Shirika la Umeme la *ZECO* na *TANESCO* kwa mauzo ya umeme unaoletwa Zanzibar.

Mhe. Spika, deni ni kubwa sana kiasi cha kufikia hatua ya *TANESCO* kutoa indhari kwamba italazimika kuuzima umeme unaoletwa Zanzibar, ili kuishindikiza Serikali kulipa madeni hayo. Mhe.Spika, kumekuwa na maelezo mengi kuhusiana na ukubwa wa deni hilo ambapo kila mmoja anatoa kauli yake.

Hivyo basi katika hili, kamati inaiomba serikali kutoa kauli ya uhakika mbele ya chombo chako hiki kitukufu kuhusiana na taarifa zilizopo ambapo zinaleta utata kwamba deni linalodaiwa *ZECO* na *TANESCO* ni bilioni 70 kama inavyoelezwa na *TANESCO* au ni bilioni 44 kama inavyoelezwa na *ZECO*. Na utaratibu gani serikali imefikia katika kuamua namna ya kuweza kulilipa deni hilo.

Mhe. Spika, kamati pia imegundua kwamba mzigo mkubwa uliolielemea Shirika la *ZECO* ni madeni yanayotokana na taasisi nyingi za serikali kuwa hazilipi umeme unaotumika katika shirika, licha ya Baraza hili kuidhinisha bajeti ya umeme kwa wizara hizo kwa malipo yanayostahiki kwa kila mwaka.
Mhe. Spika, katika hili kamati imeliagiza Shirika la Umeme *ZECO*, kuhakikisha kwamba kila taasisi iwe ya serikali au ya mtu binafsi au maeneo mengine ambayo hayalipii umeme, yakatiwe umeme. Zaidi ya hilo ni kuhakikisha kwamba taasisi zote hizo zinaekewa mita za *LUKU* ili kuwalazimisha kulipia umeme kabla ya matumizi.

Vituo vya Kuuzia Umeme

Mhe. Spika, kamati katika ziara zake imegundua kuwepo kwa vituo kidogo vya kuuzia umeme hasa kwa upande wa Pemba ambapo kuna vituo vitatu kwa Pemba nzima. Kamati inaamini kwamba huu ni usumbufu mkubwa unaowapata wananchi hasa ukizingatia kwamba vituo hivyo vipo mbali sana na wananchi, yaani Chake Chake, Mkoani na Wete.

Hivyo kamati inaiomba serikali kuongeza vituo hivi ili kuja na njia mbadala ya kuuzia umeme kama vile njia ya kununua umeme na kutumia simu za mkononi, ambapo kamati inaamini kwamba itarahisisha shughuli hiyo. Katika hili naomba niongeze pia kuhusu suala la kuzibadilisha mita za TAKUZA ambazo zinatumia pesa na kuweka mita zile za TAKUZA ambazo zinatumia *unit*.

Hii itasaidia kupata uhakika wa matumizi ya umeme na gharama zake. Mhe. Spika, hili linatokana na mtafautiano wa bei za umeme kwa wateja wenye mita za pesa na zile zinazotumia *unit* ambapo inasadikiwa kwamba bei mpya ya umeme inatumika kwa wananchi wenye mita za *units* tu, hali hii inapelekea shirika kukosa mapato lakini pia kuwaweka wananchi katika tabaka mbili tofauti; yaani wanaolipa bei kubwa na wale wanaolipa bei ndogo, jambo ambalo si utaratibu mzuri.

Chanzo mbadala cha umeme

Mhe.Spika, Kamati inapenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jitihada zake za kuwapatia wananchi huduma ya umeme na ya uhakika katika visiwa vya Unguja na Pemba. Hata hivyo, Kamati imeshawishika kuishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufikiria kwa umakini suala la kuja na mpango mbadala utakaowezesha kuwa na chanzo cha umeme kitakachomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenyewe. Kamati inaamini kwamba, kwa kuwa na chanzo chetu cha umeme kutasaidia sana kuwa na umeme wa uhakika, kupunguza madeni ya umeme yanayodaiwa kwa *ZECO* na kupata mapato mengine zaidi kwa nchi yetu kutokana na mauzo ya umeme huo.

Mhe.Spika, Kamati inazidi kuishauri serikali ikiwa kwa sasa ni gharama sana kuwa na chanzo chetu wenyewe cha umeme, basi itafute uwezekano wa kununua umeme katika nchi nyengine za jirani kuliko kutegemea chanzo kimoja cha *TANESCO* ambacho kikipata athari nchi itakosa njia ya mbadala ya kupata umeme kama ambavyo imetokea hivi karibuni, ambapo maeneo yanayozalisha gesi huko Songosongo yalikuwa yakifanyiwa ukarabati na kusababisha nchi kukosa umeme kwa siku kadhaa. (*Makofi*).

Maendeleo ya sekta ya nishati

Mhe. Spika, kumekuwa na maelezo mengi katika jamii ya watu wa Zanzibar kwamba visiwa vya Unguja na Pemba kuna uwezekano mkubwa wa kuwepo kwa nishati ya mafuta na gesi. Tafiti zimekuwa zikifanyika kila siku lakini bado hakujawa na maelezo yakinifu yanayotoa taswira halisi ya nini kilichokuwepo.

Mhe. Spika, katika kulifuatilia hili Kamati imefikia hatua ya kuzitembelea Idara za Nishati zilizopo Unguja na Pemba na pia kutembelea Shirika la Maendeleo ya Mafuta la Tanzania (*TPDC*) na kupata maelezo ya kina yanayohusu masuala ya mafuta na gesi, kuanzia utafutaji, uendelezaji, uchimbaji na uuzaji. Mhe. Spika, baada ya Kamati kupata maelezo ya kina kuhusu suala la mafuta na gesi, Kamati inaishauri serikali kujipanga na kujitayarisha katika mambo yafuatavyo:-

1. Katika uandaaji wa sera ya mafuta, Kamati inashauri uangaliwe uzoefu wa nchi za wenzetu ambao wamewahi kupitia mambo mbali mbali yanayohusiana na uzoefu ya uchimbaji wa mafuta, ili kuepusha nchi yetu kuingia katika migogoro na mapigano yanayosababishwa na uchimbaji wa mafuta na kuweza kuhakikisha kwamba nchi yetu inapata faida zaidi na sio hasara katika raslimali hii.
2. Serikali ianze kuekeza sasa katika kuwasomesha wanafunzi kwenye fani zinazohusu masuala ya mafuta na gesi kwa kuwapatia mikopo wanafunzi waliopo vyuoni ambao wanaotaka kusomea masomo hayo. Lakini pia kwa kuwashajihisha wanafunzi kusoma masomo hayo kwa kuwaeleza faida zake na kuwapa maelezo ya uwezo wa soko kubwa la ajira katika masuala hayo.
3. Kuimarisha Idara ya Nishati kwa kuipatia jengo la kisasa, vitendea kazi vitakavyoendana na kazi yenyewe, kuwapa elimu na mafunzo na kuwajengea uwezo watendaji wake, kuwapatia maslahi mazuri wataalamu waliopo sasa, ili kuendana na kazi watakayoifanya na wanayoifanya na kuwaepusha na vishawishi vya kuja kukimbia na kutafuta maslahi makubwa huko nchi za nje.
4. Serikali kuanzisha mpango mahasusi wa kutoa elimu ya kina kwa wananchi kuhusiana na masuala ya mafuta na gesi, faida na hasara zake, hii itasaidia kuepusha hasara kubwa watakayoweza kuwa nayo wananchi juu ya suala hili, hali inayoweza kupelekea migogoro isiyokuwa ya lazima.

Suala la miji *(master plan)*

Mhe. Spika, Kamati inatoa pongezi zake za dhati kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hasa kwa juhudi inazozichukua katika kutafuta muafaka wa kuupanga mji wa Zanzibar, ili uwe katika maandalizi mazuri yanayopangika na yanayovutia wenyeji wake na wageni. Mhe. Spika, Kamati imewahi kuhudhuria semina ya uwasilishaji wa ripoti ya awali ya utayarishaji wa mji wa Zanzibar na kupata fursa ya kutoa michango yake juu ya ripoti hiyo. Hata hivyo, Kamati inaiomba serikali kwa kipindi hiki ambapo mradi huo haujakamilika hatua za haraka zichukuliwe ili kuepusha vitendo vya ujenzi holela unaoendelea siku hadi siku katika miji na vijiji vya nchi yetu.

Mhe. Spika, Kamati inatoa masikitiko yake kwa Baraza hili kuwa kile inachokishudia kikiendelea siku hadi siku ambapo watu na wananchi wanauza viwanja katika maeneo mbali mbali bila ya kufuata taratibu. Mamlaka zinazohusika na utoaji wa vibali vya ujenzi, zinatoa vibali bila ya kuzingatia kwamba maene hayo hayaruhusiwi kujenga na kadhalika. Hali hii ni dhahiri isipodhibitiwa itapelekea nchi yetu kukaa pabaya.

Mhe. Spika, katika hili Kamati inazitaka mamlaka husika zikiwemo Idara ya Ardhi na Usajili, Mipango Miji na Vijiji, Idara ya Ujenzi, Idara ya Nyumba na kadhalika kusimamia vyema kwa uadilifu majukumu yao ya kazi inavyotakiwa na serikali.

Mhe. Spika, Kamati inapenda kutoa tahadhari kwa kile ilichokishuhudia wakati ilipokwenda kukagua kiwanda cha matofali cha Kwarara ambapo kilitumika kuzalishia matofali yaliyotumika kujengea nyumba zote za maendeleo zilizopo Zanzibar. Kiwanda hicho kimevamiwa kwa kiasi kikubwa na wananchi kwa kujenga maeneo ya karibu na kiwanda hicho. Ni dhahiri kwamba kiwanda hicho kwa sasa hakifanyi kazi tena lakini ni vyema kikatunzwa kwa lengo la kukifufua wakati serikali itakapoanzisha Shirika la Nyumba la Zanzibar, kikawa kinatumika kwa kuzalisha matofali ambayo yatatumika kujenga nyumba za serikali.

Mhe. Spika, hali ilivyo kwa sasa ni kwamba njia ya kuelekea katika kiwanda hicho ni ya taabu kutokana na ujenzi holela unaofanyika kuelekea njia inayoelekea kwenye kiwanda hicho. Vile vile Kamati inaiagiza wizara kusimamia upatikanaji wa baadhi ya sehemu za mashine ya kufyatulia matofali zilizokuwa zimeibiwa, ili ziweze kurudishwa kwani hiyo bado ni mali ya serikali na wananchi wanahitaji kujua namna inavyotumika.
Mahakama ya Ardhi

Mhe. Spika, uamuzi wa serikali kuanzisha Mahakama ya Ardhi ni kuwawezesha wananchi wa Zanzibar kuweza kupata haki zao zinazohusu masuala ya ardhi kwa kufuata utaratibu wa kisheria. Lengo la Mahakama hizi ilikuwa ni kumaliza migogoro ya ardhi ambayo imeonekana kukua siku hadi siku.

Mhe. Spika, Kamati inaamini kwamba utoaji wa haki za wananchi unakwenda sambamba na uwepo wa mazingira mazuri katika maeneo yanayotarajiwa kutoa haki hizo. Kamati inasisitiza kuendeleza hali iliyoiona katika Mahakama za Ardhi za Unguja na Pemba za majengo kuwa ni madogo sana kiasi cha kufikia chumba kimoja cha ofisi ambacho ni kidogo kutumiwa na watu zaidi ya sita.

Majengo yanavuja na maji yanaingia katika ofisi wakati shughuli zinaendelea. Hali iliomo ndani ya majengo hayo ni hatarishi kwa maisha ya binadamu. Chumba kinachotumiwa na Hakimu anayehukumu kesi hizo ni kidogo sana, hakina hadhi ya kutumiwa na Hakimu. Choo kipo karibu sana na chumba cha ofisi, hali inayopelekea usumbufu mkubwa kwa watendaji na kadhalika.

Mhe. Spika, Kamati inajiuliza ikiwa majengo hayatoshelezi kwa ajili ya watendaji wa Mahakama tu, vipi majengo hayo yanaweza kubeba watu waliokuja kusikiliza kesi zao pamoja na kutendewa haki. Mhe. Spika, hii inaonesha dhahiri kwamba mazingira ya haki yatakuwa yana utata kupatikana kama vile inavyopaswa.

Mhe. Spika, Kamati inaitaka serikali kuhakikisha kwamba Mahakama za Ardhi zinaimarishwa Unguja na Pemba kwa kuzipatia vitendea kazi na majengo yaliyo na nafasi na hadhi inayostahiki. Hivyo Kamati inaiomba wizara kulitengeneza jengo la Mahakama ya Unguja na kuipatia vifaa vya kutendea kazi ili kazi za utoaji haki ziweze kufanikishwa. Pia Kamati inaitaka mahakama kuzingatia idadi ya kesi anazopangiwa hakimu kwa siku, ambapo kwa sasa ni kesi 15 kwa siku ambazo ni idadi kubwa inayoweza kupelekea haki kukosekana.

Ukarabati wa Nyumba ya Kengeja

Mhe. Spika, Kamati ilipata nafasi ya kwenda kukagua jengo la nyumba za Kengeja na kuona hali halisi ilivyo, kiukweli ni nyumba ambazo hazistahiki kuishi binadamu tena, kwa sababu ni mbovu sana na ni hatari kwa maisha ya binaadamu. Itakumbukwa kwamba Baraza la Wawakilishi katika bajeti ya 2013/2014 liliidhinisha jumla ya shilingi 200,000,000, ambazo zitatumika kwa ajili ya ukarabati wa jengo hilo, na kuelezwa kwamba fedha hizo

zitatumika kuezekea kwa hatua ya awali ili kuliepusha na athari za mvua wakati zitakaponyesha.

Mhe. Spika, kwa kuwa hadi kufikia mwezi wa Disemba, 2013, fedha hizo hazijaingizwa kutoka Wizara ya Fedha na hivyo kupelekea jengo hilo kutokufanyiwa ukarabati wa aina yeyote. Kamati inaiomba serikali kabla ya kumalizika kwa mwaka huu wa fedha kuipatia wizara pesa hizo ili kuweza kulinusuru jengo hilo kuja kuanguka moja kwa moja. Hali inayoweza kupelekea maafa makubwa, na kupoteza kumbukumbu ya serikali kwa upande wa Kengeja.

Suala la Kiwanja cha Mhe. Kamal Basha Pandu

Mhe. Spika, itakumbukwa kwamba, suala la kiwanja cha Mhe. Kamal Basha Pandu ni miongoni mwa mambo ambayo yalizusha mjadala mkubwa katika kikao cha kujadili bajeti ya Serikali ya mwaka 2013/2014, ambapo baadhi ya waheshimiwa akiwemo Mhe. Hamza Hassan Juma, wakidai kwamba serikali ifikirie suala la kumpatia Mhe. Kamal Basha Pandu kiwanja chake ambacho kipo Darajani karibu na uwaja wa Malindi, ili aweze kukitumia kwa matumizi yake aliyokusudia.

Mhe. Spika, suala hili lilifuatiliwa na kamati yako kwa kuonana na Uongozi wa Mamlaka ya Mji Mkongwe, na kupata ufafanuzi wa kina juu ya suala hili. Mhe. Spika, kamati ilipata kuona ramani ya kiwanja na kuelezwa sababu zinazoleta ugumu kwa kiwanja hicho kupewa mtu kwa ajili ya ujenzi.

Kwanza kiwanja hicho kipo katika maeneo yanayotambulika kisheria kuwa ni maeneo ya wazi hayaruhusiwi kujegwa, lakini pia kiwanja kipo karibu sana na kituo chenye mashine ya umeme (*power station*). Lakini zaidi ni kwamba kiwanja hicho kinaingia sana katika maeneo ambayo tayari serikali imeshakuwa na mpango wa kupitisha barabara, wakati wa utanuzi wa baraba ya *creek road* ya kuelekea Malindi.

Mhe. Spika, kutokana na sababu zote hizo, mamlaka inapata ugumu wa kuamua kumpatia eneo hilo mheshimiwa huyo, kwa kuwa ni kinyume na utaratibu.

Mhe. Spika, Kamati baada ya kupata maelezo hayo, na kutoshelezeka kwamba kuna sababu za msingi za kuzuia utoaji wa kiwanja hicho, inaiagiza mamlaka kumpatia mheshimiwa huyo kiwanja mbadala ambacho kitamuwezesha kukitumia kwa shughuli za kimaendeleo, badala ya kumpatia hicho ambacho tayari kina vikwazo vingi.

WIZARA YA MIUNDOMBINU NA MAWASILIANO

Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ni wizara nyengine inayosimamiwa na Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, ambayo inahusika na usimamizi wa sekta ya usafiri wa baharini, nchi kavu na anga, lakini pia inahusika na sekta ya mawasiliano Zanzibar.

Mhe. Spika, naomba nianze na pongezi za dhati kwa serikali kupitia wizara hii, kwa juhudi inazochukua kuwaletea wananchi maendeleo katika sekta ya usafiri na mawasiliano, kwa kuimarisha Miundombinu ya barabara, bandari, viwanja vya ndege na kadhalika.

Pongezi za dhati nazipeleka kwa wizara kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara kwa hatua ya kuondoa matuta yaliyojengwa na wananchi, bila ya viwango vilivyowekwa kisheria katika barabara nyingi za Kaskazini Unguja, ambayo yalisababisha usumbufu mkubwa kwa wasafiri lakini pia ajali za mara kwa mara.

Vile vile, kamati inaipongeza wizara kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kwa hatua ya kusikiliza maagizo ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa kuifanyia mapitio na kuirekebisha mishahara ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege vya Zanzibar, na kuanza taratibu za kuandaa muundo wa utumishi wa mamlaka ili kuhakikisha maswala yote yanayohusu watumishi yanatekelezwa kwa kufuata taratibu za kisheria.

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo, sasa naomba kutoa ufafanuzi wa mambo mbali mbali ambayo kamati iliyafuatilia na kuyatolea miongozo inayostahiki na yenye lengo la kuboresha utendaji wa wizara, yakiwemo yale yaliyozungumzwa na kujadiliwa sana katika Baraza hili tukufu na kupitia wajumbe wako.

Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara

Mhe. Spika, idara hii ni miongoni mwa idara muhimu za wizara hii ambayo inashughulika na ujenzi na ukarabati wa barabara zetu. Hata hivyo, katika kufuatilia utekelezaji wa kazi za kawaida za idara hii kamati imebaini kwamba inakabiliwa na changamoto kubwa ya uchakavu na uhaba wa vitendea kazi vya ujenzi wa barabara, hali inayopelekea miradi mingi kukwama.

Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba vifaa vya ujenzi wa barabara vina gharama kubwa, hivyo idara pekee haitoshi kugharamia ununuzi na ukarabati wa vifaa hivyo. Hivyo basi, Kamati inaiomba serikali kuja na mpango mahsusi, ambao

utakuwa na lengo la kutenga fedha maalum, kwa ajili ya ununuzi na ukarabati wa vifaa vya mamlaka hiyo.

Mradi wa Barabara tatu (Kaskazini Pemba)

Mhe. Spika, mradi huu unajumuisha ujenzi wa barabara za Wete - Konde, Wete – Gando na Wete – Chake ambazo kimsingi ujenzi wake umesita kwa muda mrefu sasa. Hali inayopelekea wananchi kupata usumbufu mkubwa hasa kwa kuwa njia hizo zimebaki bila ya kuendelezwa kwa muda mrefu.

Kamati ilibaini kwamba mkandarasi na mshauri muelekezi waliamua kuondoka eneo la mradi baada ya kutokupata malipo yao kwa muda mrefu ambayo wameifanya kazi hiyo.

Kamati hii ilifuatilia suala hili na iliamua kuzikagua barabara zote na kutaka maelezo ya kina kutoka kwa wizara. Maelezo yaliyotolewa kwa kamati yalibainisha kwamba ni kweli Mkandarasi na Mshauri waliondoka kwa madeni waliyokuwa wakidai, hali iliyopelekea miradi hio kusita. Hata hivyo, wakati wa ziara ya mwisho ya Kamati kisiwani Pemba, wizara iliipatia maelezo Kamati kwamba fedha zinazodaiwa na Mkandarasi na Mshauri Muelekezi, zimeshalipwa zote na kinachosubiriwa sasa ni kuanza kazi hiyo, ambapo tayari wote wawili wameshafika eneo la mradi kukagua, na ifikapo mwezi wa Januari kazi hiyo itaanza.

Mhe. Spika, Kamati inaishauri wizara kuhakikisha kwamba mara baada ya Mkandarasi kuanza kazi ya ujenzi, ni jukumu la wizara kumsimamia na kuhakikisha kwamba mradi huo unamalizika na kuwaondolea wananchi usumbufu walioupata kwa muda mrefu. Mhe. Spika, maelezo kwa urefu yanayohusiana na mradi huu yanaonekana katika ripoti kuu ya Kamati kwa mwaka 2013/ 2014.

Uvunjaji Mkubwa wa Sheria za Barabarani

Mhe. Spika, **s**isi sote ni mashahidi wa namna uvunjaji wa sheria za barabarani ulivyokithiri katika maeneo mbali mbali ya mji wetu wa Zanzibar. Vitendo hivyo ni kama magari yasiyokuwa na namba kutembea nyakati zote, hususan nyakati za usiku ambapo Kamati inaamini kwamba magari hayo yanaweza kutumika kufanya uhalifu wa aina yoyote bila ya kujulikana. Kamati pia inaamini kuwa magari ya abiria kupakia kupita kiwango kilichokusudiwa kisheria, ni moja kati ya kadhia ya uvunjwaji wa sheria. Madereva wanaoendesha magari bila ya kuwa na leseni hasa wanaotumia vyombo vya matairi mawili, kutembea bila ya utaratibu wa kisheria n.k.

Kamati inaiagiza idara hii kufanya kikao cha pamoja na taasisi nyengine zinazohusika na usimamizi wa usalama barabarani, likiwemo Jeshi la Polisi, kwa lengo la kuweka mikakati ya kuzuia uvunjaji huu wa sheria za barabarani na kukumbushana wajibu wa kila mmoja katika hili.

Mhe. Spika, kwa kuwa kikao kilifanyika na maazimio kufikiwa, Kamati inaiagiza Idara pamoja na Jeshi la Polisi kusimamia ipasavyo maazimio hayo kwa lengo la kupunguza ajali na uvunjwaji wa sheria katika mabarabara yetu, ili kuongeza kiwango cha uheshimu wa sheria za barabarani.

Mhe. Spika, kamati pia inakumbushia Serikali kutekeleza ahadi yake iliyoitoa katika Baraza hili kwamba gari zitatafutiwa utaratibu wa kusajiliwa na kupatiwa namba maalum, mara baada zitakapoteremshwa hapo bandarini, hatua ambayo itasaidia kutatua tatizo la magari kuendeshwa bila ya leseni na bila ya namba.

Mkonga wa Taifa

Mhe. Spika, itakumbukwa kwamba harakati za kuweka miundombinu ya Mkonga wa Taifa zimekamilika kwa kiasi kikubwa sana na kupelekea mkonga huo kukabidhiwa kwa Idara ya Mawasiliano iliyo chini ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa hatua za utekelezaji.

Hata hivyo, kamati inapata mashaka na uwekaji wa mkonga huo katika maeneo mbali mbali, ambapo inaonekana dhahiri kwamba mkonga huo umelazwa futi kidogo kwenda chini ya ardhi, lakini pia uko karibu sana na barabara.

Mhe. Spika, Kamati inapata ujasiri mkubwa wa kuwa na mashaka hayo, kwa kile ilichoshuhudia Pemba kwamba mkonga umeanza kupata athari ya kukatwa na kampuni ya Kichina ya *Cinohydrate* walipokuwa katika harakati za kuchimba barabara.

Mhe. Spika, Kamati inaitaka serikali kuhakikisha kwamba mkonga huo unalindwa na kuzingatia viwango vya kimataifa wakati wa uwekaji wa miundombinu kama hiyo.

Vile vile, Kamati inaitaka serikali kuzihusisha taasisi husika kwa pamoja, wakati wa kuanzisha miradi ya maendeleo, hii itapelekea kuwa na mipango ya muda mrefu itakayoepusha mradi mmoja kuathiri maendeleo ya mradi mwengine, ambapo yote ipo kwa faida ya wananchi.

Usimamizi wa Vyombo vya Baharini

Mhe. Spika, usimamizi wa vyombo vya usafiri wa baharini kwa Zanzibar unasimamiwa na Mamlaka ya Usafiri Baharini (*ZMA*), ambayo ni taasisi muhimu kwa kusimamia na kuhakikisha kwamba sheria za usalama wa baharini zinafuatwa kama zilivyoainishwa katika maazimio mbali mbali ya kitaifa na kimataifa.

Mhe. Spika, sote tutakuwa ni mashahidi kwa ajali za vyombo vya baharini zinazotokea mara kwa mara katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba na kusababisha vifo na upotevu wa watu wengi ambao ni nguvu kazi ya Taifa kwa ujumla.

Mhe. Spika, Kamati imebaini kuwa licha ya taasisi hii ya kusimamia dhamana ya usalama wa watu na mali zao, kwa kuhakikisha kwamba wanatoa taarifa kwenye vyombo husika, lakini pia kwa vyombo vinavyotaka kubeba abiria vinakaguliwa na kuhakikisha kwamba vimefikia viwango vya kimataifa katika kupakia abiria hao.

Hata hivyo, kamati imebaini kwamba taasisi hii haijawezeshwa ipasavyo ili kuweza kusaidia utekelezaji wa majukumu yake ipasavyo. Kwa mfano, taasisi haina vifaa vya uokozi, haina ofisi ya kudumu, haina ofisi katika bandari tofauti za Zanzibar, haina kanuni kamili za kuwezesha utekelezaji wa sheria yake n.k

Hivyo basi, Mhe. Spika, Kamati inaiomba serikali kuweka kipaumbele kwa kuiwezesha taasisi hii, hali itakayopelekea kufanya kazi vizuri na kupunguza majanga yanayojitokeza mara kwa mara.

Ujenzi wa Terminal Katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Zanzibar

Mhe. Spika, Mradi huu una lengo la kujenga jengo kubwa na la kisasa la abiria katika Uwanja wa ndege wa Zanzibar, ili uwanja huo uweze kupokea ndege kubwa na kubeba abiria wengi zaidi wasiopungua milioni moja kwa mwaka. Hata hivyo, wakati wa utekelezaji wa mradi huo, makosa ya kiufundi yalijitokeza hali iliyopelekea serikali kuchukua hatua ya kuusitisha kwa muda mradi huo, kwa lengo la kumtafuta Mshauri Mwelekezi, ili aweze kufanya utafiti wa kina na kutoa ripoti itakayotoa ushauri kwa serikali utakaowezesha kujua tatizo na hatua za kuchukua ili kuendeleza mradi huo.

Baada ya kumaliza kazi yake Mshauri Mwelekezi (*ADPI* kutoka Ufaransa) alikuja na ripoti yake kwa serikali, na kupendekeza hatua za kuchukuliwa ambazo kimsingi, ziliitaka serikali kuchagua hatua ya kulirekebisha jengo hilo

au kulivunja jengo na la kulisogeza nyuma, ili kufikia eneo ambalo lilikusudiwa kujengwa hapo awali.

Mhe. Spika, serikali kwa sababu tofauti, zikiwemo gharama ya ujenzi, muda wa ujenzi pamoja na mkopo na ushirikiano wa kimataifa kati ya Zanzibar na China, iliamua kufuata ushauri wa kuliacha jengo hilo hapo lilipo na badala yake kulifanyia ukarabati ikiwemo kuzihamishia ndege kuweza kupaki pembeni upande wa Kusini wa *Terminal* hiyo, badala ya mbele ya *Terminal* kama ilivyokuwa awali.

Mhe. Spika, kwa ujumla kamati haipingani na maamuzi ya serikali yaliyofikiwa ya kuendelea na ukarabati wa jengo, kwa kuwa inaamini kwamba imezingatia mambo muhimu na ya kimsingi. Hata hivyo, kamati inaamini kwamba serikali ingekuwa na maamuzi mazuri zaidi iwapo ingeuzingatia kwa makini sana ushauri wa Bodi ya Mamlaka ambao ulitolewa kwa barua kwenda kwa waziri. Ushauri ambao kamati baada ya kupata ufafanuzi wa kina inaona ni ushauri wenye nia nzuri ya kuundeleza uwanja huo na kuuwezesha kuongeza mapato yake ya ziada.

Baadhi ya ushauri huo ni huu ufuatao:-

1. Jengo litaweza kukidhi mahitaji yanayotakiwa kutokana na taratibu za *ICAO* na *IATA.*
2. Usanifu wa jengo utakuwa unaendana na hali halisi ya mazingira ya nchi.
3. Gharama za uendeshaji wa huduma katika jengo zitapungua, hususan katika matumizi ya umeme.
4. Uwezekano wa kupanua huduma za kiwanja baadae utakuwepo.
5. Uwezo wa kupokea abiria zaidi hadi kufikia milioni mbili kwa mwaka unawezekana.
6. Mamlaka itakuwa na uwezo wa kuingiza mapato zaidi kutokana na mfumo na mpangilio mpya wa biashara.

Kwa ujumla, Bodi ya Mamlaka iliishauri serikali kufuata pendekezo namba 2A ambalo hata mshauri mwelekezi amelitilia mkazo zaidi, pamoja na kuwa pendekezo hili linahitaji gharama zaidi zinazokadiriwa kufikia dola milioni 10, ukilinganisha na pendekezo namba 1B ambalo serikali imeamua kulifuata.

Lakini kutokana na faida zilizoainishwa hapo juu gharama hizo zinaweza kujirudia ndani ya miaka mitano ya kazi, lakini gharama ndogo inayohitajika kwa kufuata pendekezo namba 1B zitapelekea serikali na mamlaka hasara

kubwa zaidi ya uendeshaji hapo baadae, na kusabaisha shughuli za maendeleo ya mamlaka kuzorota.

Upatikanaji wa Kampuni ya Kutoa Huduma Katika Viwanja vya Ndege – Zanzibar

Mhe. Spika, ni utaratibu wa viwanja vyote vya ndege duniani, kwamba ni lazima kuwe na utaratibu wa utoaji wa huduma mbali mbali, kama ukaguzi wa mizigo, upakiaji, upakuaji, usimamizi wa kutoa huduma wakati wa utuaji na urukaji wa ndege, kusaidia abiria kupata mizigo yao, na kuwasaidia abiria wasiojiweza kufika eneo lenye ndege n.k.

Kwa muda mrefu sasa viwanja vyetu vya ndege vimekuwa na kampuni moja tu ya kutoa huduma hizo katika viwanja hivyo. Kampuni ya *ZAT* ndiyo inayohusika na shughuli hizo, ambayo kwa muda mrefu sasa kampuni hiyo imekuwa ikilalamikiwa na abiria pamoja na uongozi wa mamlaka wa viwanja hivyo, kutokana na huduma zake zilizo chini ya kiwango kinachotakiwa.

Mhe. Spika, serikali iliagiza kufanyika taratibu za kuipata kampuni nyengine ya kutoa huduma hizo uwanjani hapo. Taratibu zilifanyika, lakini kabla ya kufikia hatua ya kuitangaza kampuni iliyoshinda, Mamlaka ilipata maagizo kutoka serikalini, kwamba utaratibu huo wa kuitisha tenda ufutwe na tenda hiyo itangazwe upya, ingawa ile ya mwanzo ilifikia hatua za mwisho.

Mhe. Spika, Kamati imetaarifiwa kwamba baada ya serikali kutoa maagizo ya kufuta tenda hiyo, iliamua kusimamia suala hilo na kuhakikisha kwamba kampuni hiyo itapatikana na kuanza kazi zake karibuni.

Mhe. Spika, jambo ambalo linaishangaza Kamati ni kwa nini serikali iingilie utaratibu huo na kwa nini hadi sasa kampuni hiyo haijaanza kazi, hali inayopelekea mamlaka kuendelea kutegemea kampuni moja ambayo utendaji wake sio mzuri.

Madeni ya Kampuni ya *ZAT*

Mhe. Spika, Kampuni ya *ZAT* imeanza kutoa huduma za viwanja vya ndege kwa takribani miaka 18 sasa, lakini kitu cha kushangaza ni kwamba kampuni hiyo haina mkataba *(consession agreement*), mbali na kuwepo jitihada za makusudi zinazofanywa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege vya Zanzibar kuitaka kampuni hiyo kusaini mkataba huo kama sheria zinavyotaka.

Mhe. Spika, kamati imebaini kuwa mbali na kampuni hii kukosa mkataba wa kazi, lakini pia haijawahi kulipa fedha za uendeshaji ambayo inapatikana

kutokana na makusanyo ya mwaka ya kampuni hiyo, ambayo kampuni hiyo inayakusanya kutoka kwa kampuni za ndege zinazopata huduma kutoka kwa *ZAT*.

Taarifa ilizozipata Kamati kutoka kwa uongozi wa Mamlaka na Bodi yake kwamba serikali kupitia Wizara ya Fedha iliwahi kumwita mmiliki wa kampuni hiyo, na kumtaka alipe fedha hizo ambazo si chini ya Shilingi milioni 400. Fedha ambazo Kamati inaamini kwamba zingeisaidia sana mamlaka katika shughuli zake, na akaahidi kulipa. Kamati inasikitishwa kwamba hadi Kamati inaandaa ripoti hii fedha hizo hazijalipwa.

Mhe. Spika, Kamati ilitaka kupata maelezo kutoka kwa kampuni hiyo, kuhusiana na tuhuma hizo, lakini haikuwezekana kutokana na taarifa iliyojibiwa kwa maandishi, kwamba viongozi wa kampuni hiyo wote wana dharura na wengine ni wagonjwa. Hivyo, hawataweza kukutana na kamati.

Mhe. Spika, Kamati inaitaka serikali kuhakikisha kwamba fedha hizo zinalipwa, lakini pia kuhakikisha kwamba kampuni hiyo inasaini mkataba wa kufanya kazi katika viwanja vya ndege, kama ilivyo kisheria, na inaamini kwamba serikali haijashindwa wala haitoshindwa kuifanya kampuni hiyo kufuata taratibu zilizowekwa kisheria.

Katika kutilia msisitizo suala hili, Kamati inaitaka serikali kumaliza taratibu za kuipata kampuni nyengine ya kutoa huduma kiwanjani hapo. Kamati inaamini kwamba kutokuwepo kwa kampuni nyengine ya kutoa huduma, ni kikwazo kinachoifanya mamlaka isiweze kuiwajibisha kampuni ya *ZAT*, hatua ambayo inaweza kusababisha uwanja huo kukosa huduma hasa katika sheria za kimataifa.

Suala la Kuipatia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Fedha Zinazokusanywa Kutokana na Huduma Inazozitoa Mamlaka Kwa Abiria (*Airport Service Charges*)

Mhe. Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 19 (1) (b) cha Sheria ya Mamlaka ya Viwanja vya ndege nam. 8 ya mwaka 2011**,** inataja kwamba fedha zinazokusanywa kutokana na huduma zinazotolewa na Uwanja wa Ndege zitakuwa ni sehemu ya vyanzo vya mapato vya mamlaka, na huu ndio utaratibu wa viwanja vya ndege vingi duniani. Mhe. Spika, lengo la kuweka tozo hii kutoka kwa abiria ni kwa sababu viwanja vya ndege vinagharamika kutoa huduma kwa abiria wanaoingia na kutoka kiwanjani hapo.

Mhe. Spika, katika hali ya kushangaza licha ya kuwepo utaratibu huo uliowekwa na sheria, lakini fedha zote zinazokusanywa kama ni tozo ya

huduma, zinazotolewa kwa wananchi na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, zinakwenda katika hazina ya serikali, bila hata ya kuipatia Mamlaka asilimia fulani ya kurudisha gharama inazotoa kwa huduma inazowapatia abiria.

Kamati imepokea malalamiko hayo kutoka kwa uongozi na kuamua kuyafikisha mbele ya serikali kupitia Wizara ya Fedha. Kamati ilipokutana na Waziri wa Fedha ilijibiwa kwamba serikali haiwezi kutoa chanzo hicho cha fedha, kuwa sehemu ya mapato ya mamlaka kwa sababu mamlaka ina vyanzo vyengine na pia ipunguze gharama zake za uendeshaji wa ndani kama kupunguza mishahara n.k.

Mhe. Spika**,** kamati haikuridhishwa na majibu hayo, na kwa kupitia ripoti hii inaishauri serikali kulifikiria upya suala la kuipatia mamlaka japo sehemu ya mapato hayo ili iweze kusaidia kuendeleza shughuli za kawaida za mamlaka, hasa ukizingatia kwamba Mamlaka haipatiwi fedha za maendeleo.

Vile vile Kamati inashawishika kuamini kwamba fedha hizi zitaisaidia mamlaka kutatua matatizo yake mengi ambayo yanaikabili kwa sasa, kama ukosefu wa *X-Ray machine*, mashine za kukagulia mizigo, hali inayopelekea mizigo kukaguliwa kwa mikono, shughuli inayochukua muda mwingi na ni uchovu kwa watendaji, pia ukosefu wa usafiri kwa wafanyakazi wa mamlaka ambao hutakiwa kuwepo kazini hadi muda wa usiku, n.k

Mhe. Spika, Kamati haikatai kwamba, inawezekana kwamba matumizi ya mamlaka yakawa ni makubwa sana, lakini haikubaliani na hoja ya kupunguza mishahara ya watendaji kwa kuwa maisha ni magumu sana, na kila siku wajumbe wa Baraza lako hili tukufu wamekuwa wakilizungumzia sana suala la kuboresha maslahi ya watendaji ili wapate kujikimu na kujitosheleza na wafanye kazi kwa moyo safi.

Mhe. Spika, Kamati kupitia kikao hiki, inapenda kuiomba serikali kufikiria upya suala la kuipatia mamlaka japo asilimia fulani ya mapato hayo. Kwa kuwa serikali inakitegemea chanzo hichi kwa matumizi ya shughuli za kimaendeleo. Kamati inashauri basi, mapto hayo yagaiwe sehemu tatu, ambapo thuluthi moja iende katika mfuko wa hazina, thuluthi ya pili iende katika miradi ya kuendeleza viwanja na thuluthi ya tatu ibakie kwa mamlaka ili kufidia gharama za kuendesha kiwanja hicho.

Changamoto za Kiwanja cha Ndege cha Pemba

Mhe. Spika, Uwanja wa Ndege wa Pemba ni uwanja wa ndege ambao upo chini ya uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege vya Zanzibar.

Mhe. Spika, Kamati ilipotembelea kiwanja hiki mara mbili tofauti, iligundua changamoto nyingi ambazo baadhi ya hizo zimeshazungumziwa sana katika Baraza hili tukufu. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatazo:-

i. Ukosefu wa Taa za kuongozea ndege

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza awali kwamba changamoto hii ni ya muda mrefu, na serikali kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasailiano imeshatoa ahadi nyingi sana kwa Kamati lakini pia kwa Baraza hili kwa ujumla. Jambo la kusikitisha kwamba licha ya Baraza hili kuidhinisha fedha kwa ajili ya utatuzi wa changamoto hii, mpaka ripoti hii inasomwa leo mbele yako na mimi Mhe. Mwenyekiti wa kamati hiyo katika Baraza hili, hakuna fedha iliyoingizwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Mhe. Spika, kamati inaelekeza malalamiko yake kwa Wizara ya Fedha ambayo imeshindwa kuipatia fedha wizara, kwa lengo la kutekeleza kazi ya uwekaji wa taa hizo. Hivyo basi, kamati inahitaji kupata maelezo ya kina kutoka kwa Waziri wa Fedha ni kwa nini agizo hilo halijatekelezwa hadi leo hii.

ii. Ukosefu wa Huduma za Zimamoto

Mhe. Spika, huduma za zimamoto ni miongoni mwa huduma muhimu sana zinazotakiwa ziwepo kwa wakati wote katika maeneo ya viwanja vya ndege, hasa kutokana na ukweli kwamba moto ni jambo ambalo linaweza kuzuka wakati wowote katika maeneo hayo.

Mhe. Spika, kiwanja cha ndege cha Pemba hakina njia maalumu ya kupitishia gari ya zimamoto kufikia ilipo ndege (*Perimeter road*), hali inayoipa ugumu gari hilo kufika maeneo hayo. Lakini pia mazingira wanayoishi askari wa zimamoto hayaridhishi, magodoro wanayolalia hayaridhishi, nguo maalum za kuzimia moto hawana na mambo mengine yanayohusiana na wao. Kwa hivyo, tunaishauri serikali kuiangalia taasisi ya zimamoto huko Pemba.

Mhe. Spika, tatizo hili halipo tu katika kiwanja cha ndege cha Pemba, lakini pia kwa kiwanja cha ndege cha Unguja ambapo inadaiwa kwamba huduma hizo hazijafikia kiwango cha kimataifa.

(iii) Ukosefu wa Huduma Muhimu

Mhe. Spika, kama inavyeleweka kwamba katika viwanja vya ndege vyote duniani kunahitajika baadhi ya huduma muhimu ziwepo masaa 24, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba usalama wa kiwanja pamoja na abiria unapatikana wakati wote. Mhe. Spika, Kamati imebaini kutokuwepo kwa huduma katika baadhi ya taasisi muhimu kiwanjani hapo, licha ya maagizo yaliyotolewa na kamati ilipotembelea kwa mara ya mwanzo katika mwezi wa Machi, 2013, kuitaka mamlaka kuwaandikia wahusika wa taasisi hizo, ili waweze kuweka huduma hizo muhimu katika viwanja hivyo.

Licha ya jitihada za uongozi wa mamlaka kuzikarabati ofisi hizo, na kuwataka wahusika kuweka huduma hizo ambazo ni huduma za afya, huduma za watu wa kilimo, huduma za watu wa kutoza ushuru wa forodha na kadhalika. Lakini bado kamati ilipotembelea tena katika mwezi wa Januari 2014 imekuta huduma hizo bado zinakosekana katika viwanja hivyo vya ndege hususan Pemba.

Mhe. Spika, zaidi ya hilo, kamati imeshtushwa na taarifa ilizopata kutoka kwa uongozi wa Uwanja huo, kwamba hakuna askari anayevaa sare kwa wakati wote wa mchana katika kiwanja hicho, askari waliopo ni askari kanzu pekee, na badala yake askari hao huja kiwanjani hapo wakati wa usiku kwa lengo la kulinda tu. Hili linatokana na kukosekana kwa kituo cha polisi katika viwanja hivyo. Kamati inajiuliza iwapo patatokea tatizo lolote la kiusalama kiwanjani hapo wakati wa mchana nini kitafanyika na nini kitakachotokea kwa wananchi wakati ulizni haupo?

Mhe. Spika, Kamati inaitaka serikali kupitia wizara inayohusika na usimamizi wa Jeshi la Polisi kuwatafutia utaratibu wa kujengewa kituo cha polisi katika maeneo ya uwanja wa ndege wa Pemba ili askari hao waweze kufanya kazi zao mchana na usiku.

Uimarishaji wa Bandari

Mhe. Spika, Bandari ni miongoni mwa vyanzo vikubwa vinavyotegemewa na serikali yetu katika kukuza mapato yake ili kujiletea maendeleo endelevu. Kwa kulijua hilo, tumekuwa tukishuhudia harakati mbali mbali za serikali na watu binafsi kujitolea kwa lengo la kuziimarisha Bandari zetu, Kamati inatoa pongezi za dhati kwa hilo.

Mhe. Spika, **S**hirika la Bandari ndiyo taasisi pekee iliyokabidhiwa dhamana ya kuzisimamia Bandari zote zilizopo nchini, ikiwemo bandari ya Malindi, Mkoani, Mkokotoni, Wete na Wesha. Pia, kumekuwa na jitihada mbali mbali

za kuziimarisha Bandari hizi kwa kuzipatia vifaa vya kisasa vya kufanyia kazi kwa lengo la kufikia ufanisi wa kiwango cha juu.

Mhe. Spika, Kamati kwa kuzingatia kwamba inahakikisha kwamba huduma za kibandari zinaimarishwa ipasavyo, inapenda kuishauri serikali mambo yafuatayo:-

1. Kuipatia eneo Shirika la Bandari karibu na bandari hiyo ili iweze kujenga jengo la kisasa litakalokuwa na mnara wa kuongozea meli na kuachana na utaratibu wa sasa wa kuazima majengo. Shirika hili limekuwa likiazima ofisi katika jumba la *Beit el Ajaib*, ili kuweza kufanya shughuli za kuongozea meli. Kwa sasa ambapo jengo hilo limepata athari Shirika linaendelea kuhangaika kuazima majengo mengine. Hivyo, ili kuondokana na kadhia hii ni vyema wakapatiwa eneo hilo mbadala.

2. Kamati inaishauri serikali pia, kuangalia utaratibu wa kuikarabati minara ya kuongozea meli ambayo ni minara inayotambulika kimataifa, kwa kuwa Kamati ilipata nafasi ya kukagua minara yote ya Unguja na Pemba na kujionea hali halisi ilivyo, inapendekeza kwamba minara hiyo ifanyiwe ukarabati, hasa kwa kuwa mingi ya minara hiyo imejengwa zamani sana (kabla ya Mapinduzi ya Zanzibar), ukarabati huo upendekezwe zaidi katika ngazi za kupandia minara hiyo, ambazo nyingi zao ni za mbao na zimeshaanza kulika, hatua hii itasaidia kuiweka minara hiyo katika hali nzuri.

3. Kamati pia inaishauri serikali kulifikiria suala la kuiimarisha bandari ya Mkoani kwa kuipatia vifaa ikiwemo *crane* ya kushushia mizigo mikubwa, lakini pia kuiwekea kipaa cha kuwakinga abiria na mvua na jua linapokuwa kali wanapokaa kwa kushughuli zao za kupanda na kushuka kwa meli. Kamati inatoa pendekezo la kuitumia gati ya zamani ya Mkoani, kutumika kuwa ni sehemu ya kupakia na kushukia kwa meli za abiria na gati ya sasa ibakie kuwa ya kushushia mizigo tu. Hii itasaidia kuondoa ugumu na mchanganyano wa abiria na shughuli za kiutendaji pale bandarini.

4. Kamati pia inaitaka serikali kuzikarabati bandari ambazo bado haziko katika kiwango kizuri, hali inayopelekea kutumiwa kinyume na utaratibu na kuikosesha serikali mapato, kutokana na kutokuwa na ofisi zinazosimamia harakati za kila siku za Bandari hizo, Mfano Bandari ya Mkokotoni, bandari hiyo kwa sasa imekuwa na inaingiza

bidhaa nyingi, lakini kwa kuwa haijawa bandari iliyoendelezwa mapato hayo yanapotea katika mikono ya watu wachache.

5. Kamati inaishauri serikali kufikiria uwezekano wa kuanzisha bandari ndogo katika maeneo ya Nungwi, ambayo itasaidia kupunguza masafa ya safari baina ya visiwa hivi viwili, lakini pia itatumika kurahisisha shughuli za uokozi wakati wa majanga ya meli yanapotokea, bandari hiyo pia itaweza kutumika kujenga vituo vya maafa ambavyo vitasaidia kutoa huduma za dharura kwa wahanga wa maafa ya ajali za baharini, ambayo yanaonekana kuindama nchi yetu siku hadi siku.

6. Kamati pia inapendekeza kwa serikali kufikiria kuifanyia marekebisho sheria ya Shirika la Bandari ili iweze kutoa mamlaka kwa Shirika hilo, kusimamia maswala yote yanayohusu bandari, ikiwemo kuiwezesha zabuni au kutoa mapendekezo kwa serikali kuhusiana na uanzishaji wa bandari mpya katika maeneo tofauti, kuliko ilivyo sasa kwamba Shirika hilo limepewa Mamlaka ya kusimamia bandari zilizopo sasa za mjini tu.

Kwa ujumla Kamati inaitaka serikali kuharakisha ujenzi wa Bandari ya Mpiga duri, ambayo kwa sasa hakuna taarifa za kuanza kwa harakati za ujenzi wa bandari hiyo, bali kilichopo ni mazungumzo tu.

KAMPUNI YA ZANTEL

Mhe. Spika, Kampuni ya *Zantel* ni kampuni binafsi inayotoa huduma za simu kwa hapa Tanzania, wamiliki wa hisa za kamapuni ni *Etisalat* 65%, *MEECO* 17% na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni 18%. Kwa ujumla kampuni hii inajihusisha kutoa huduma za simu, *internet* n.k.

Mhe. Spika, kinadharia makao makuu ya Kampuni hii yapo Zanzibar, lakini kihuduma na uimarishaji wa utendaji uko Tanzania Bara, Kamati yako ilipata nafasi ya kutembelea ofisi za Kampuni hii kwa upande wa Zanzibar na Tanzania Bara na kuona tofauti kubwa iliyopo.Vile vile, Kamati ilipata nafasi ya kukutana na wafanyakazi wa kampuni kwa upande wa Zanzibar na kusikiliza matatizo yao.

Kutokana na Kamati kukosa majibu ya kuridhisha juu ya malalamiko hayo kwa upande wa Zanzibar, hasa ukizingatia kwamba viongozi wote wa juu wa kampuni hii wamehamia Tanzania Bara, Kamati ilikwenda kuonana na uongozi huo kwa upande wa Tanzania Bara na kuyawasilisha malalamiko hayo kwa uongozi, ambapo miongoni mwa matatizo hayo ni; ukosefu wa

Muundo wa Utumishi (*scheme of service*), hali inayopelekea kutokuwa na utaratibu maalum wa kushugulikia maslahi ya wafanyakazi kwa mujibu wa sheria.Pia, kuwepo kwa utofauti mkubwa wa maslahi baina ya wafanyakazi wa Zanzibar na wale wa Tanzania Bara, kwa kazi za aina moja, ukosefu wa mikataba ya kazi, n.k.

Ni vyema kwamba, uongozi uliopo ulikubali na kuzungumza na Kamati na kuahidi kuyafanyia kazi na kuyapatia ufumbuzi matatizo yaliyopo haraka iwezekanvyo.

Mhe. Spika, itakumbukwa kwamba mjadala mkubwa ulijitokeza wakati wa kujadili bajeti ya Wizara hii, hasa kuhusiana na suala la Kampuni ya *Zantel*, kuwepo kwa tetesi zinazoelezea kwamba Kampuni hiyo inatarajia kuhamisha makao makuu yake kwenda Tanzania Bara. Kamati ililifuatilia hilo na kwa mujibu wa uongozi wa juu wa Kampuni hiyo, ambao uko Tanzania Bara una kuiahidi Kamati kwamba, hawana lengo la kuihamisha Kampuni hiyo, lakini kuhusu hoja ya kuimarisha huduma zaidi kwa upande wa Tanzania Bara, Kampuni ilieleza kwamba kwa kuwa upande wa Tanzania Bara kuna makampuni mengi ya simu, hivyo, wanajaribu kuboresha huduma ili kuweza kumudu ushindani mkubwa wa kibiashara uliopo.

Mhe. Spika, Kamati imefarijika na kauli ya kwamba makao makuu ya Kampuni hiyo hayatohamishwa kutoka Zanzibar, lakini inapenda kutoa ushauri kwa serikali kuliangalia upya suala la kuzitoza kodi Kampuni za simu zinazotoa huduma hapa Zanzibar ambazo kwa sasa zinalipia kodi kwa Tanzania Bara tu, kinyume na Kampuni ya *Zantel* ambayo inalipia kodi Tanzania Bara na Zanzibar.

TAASISI ZA MUUNGANO

Mhe. Spika, Kamati yako ilipata nafasi ya kutembelea taasisi mbali mbali za muungano ambazo uratibu wake kwa upande wa Zanzibar, uko chini ya Wizara hizi mbili zinazosimamiwa na Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, zikiwemo Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*), Shirika la Maendeleo ya Mafuta na Petroli (*TPDC*) na *TCAA.* Lengo la Kamati kuzitembelea taasisi hizo, ni kuona namna wanavyotekeleza majukumu yao na namna gani ambavyo ushiriki wa Zanzibar katika kutatua na kugundua kadhia mbali mbali katika taasisi hiyo, zaidi ya hilo, Mhe. Spika, ilikuwa ni kutaka kujua ni kwa namna gani Mgawanyo wa mapato baina ya Zanzibar na Tanzania Bara unafikiwa katika taasisi hizo.

Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa, Kamati yako inapenda kulitaarifu Baraza hili tukufu kwamba, taasisi ambayo Kamati iliulizia taarifa hizo

haikuwa na majibu ya kuridhisha juu ya maswala hayo. Majibu zaidi yalikuwa ni kwamba fedha hizo baada ya kukusanywa hupelekwa hazina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na huko ndiko mgawanyo unakotakiwa ufanyike.

Baada ya kusema hayo, Mhe. Spika, napenda kulitaarifu Baraza lako tukufu kwamba hoja zinazohusu Wizara hizi mbili ni nyingi na zina maelezo marefu na ufafanuzi mkubwa.Kwa hivyo, maelezo hayo kwa urefu yanapatikana katika ripoti kubwa ya Kamati ambayo naamini wajumbe wote wa Baraza hili wameshapatiwa. Hivyo basi, nawaomba wajumbe waitumie vyema ripoti hiyo kwa kuisoma ili wapate kuijadili ripoti hii na kuiboresha na hatimae kuikubali.

Mhe. Spika, baada ya kuwaomba wajumbe kuichangia kwa kina ripoti hii, nataka nichukue nafasi hii kuzishukuru Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano pamoja na watendaji wake kwa ujumla pamoja na makatibu wetu wanaofanya kazi muda wote bila kuchoka kwa ushirikiano wao ulioutukuka kwa Kamati yetu wakati wote wa kazi, ili kufanikisha majukumu haya.

Hivyo basi, kwa niaba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi, naunga mkono ripoti hii na nawaomba wajumbe wenzangu wote waiunge mkono ripoti hii.

Mwisho kabisa, shukurani zangu za dhati nazipeleka kwa ofisi ya Baraza la Wawakilishi, hususan kwa mtendaji mkuu Katibu wetu mpendwa Yahya Khamis Hamad kwa kazi kubwa na ushauri mkubwa anaotupa kwa kushirikiana na wewe Mhe. Spika, kwa msaada na kuitaka Kamati hii ili iweze kufanikisha majukumu yake.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Mhe. Mwenyekiti, tunakushukuru kwa kuwasilisha ripoti hiyo ya kamati ambayo ni refu kidogo. Wajumbe sasa tuchangie ripoti hizo.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, niende moja kwa moja ili kuweza kuokoa muda kwanza naunga mkono ripoti. Lakini la pili, Mheshimiwa katika kuchangia kwangu hivi karibuni nilionesha baadhi ya mambo ambayo yanakwaza kwa mujibu wa taratibu au kwa mujibu wa sheria nikaona bora leo nizidi kumuhimiza Mheshimiwa wangu Waziri ili azidi kuweza kukamilia na hii hatua iweze kufika.

Mheshimiwa kuna tatizo ambalo nilieleza na kwa bahati nzuri Mheshimiwa wangu waziri nimempelekea barua na Mhe. Waziri, alimtuma Mkurugenzi wake kwenda kuifanya ile hatua na kaifanya na akaweza kutoa barua ya kusimamisha. Lakini kuna tatizo zililojitokeza na ambalo mimi nimeshangaa sana hata hawa ndugu zetu wa Polisi, jamani hatukusudii kuwasema Mhe. Spika, kwa ubaya, lakini waangalie zile sekta ambazo au Wizara husika zinapotoa maagizo na wao wa-*action* ile.

Mkurugenzi amesema kuwazuia kiwanja hiki, kuna matatizo kwa maana hiyo mantiki yake ni kuwa tayari nakala kapeleka kwa wahusika wote ambao wanaoweza kuwa kwenye eneo lile na kuweza kusimamia. Lakini la kushangaza mtu huyu anaendelea kujenga kwa jeuri. Sasa natoa vielelezao.

Mheshimiwa kiwanja hicho 547 kilitolewa tarehe 17 Januari, 2008, lakini kiwanja hicho kuna mtu mwengine, vile vile, kimetolewa tarehe 27 Oktoba, 2008. Lakini kuna na mtu mwengine huyo huyo kiwanja kimoja kimetolewa hati tatu. Mhe. Spika, mimi cha kushangaza huyu mtu ambaye wa mwisho, mwenye kiwanja cha mwanzo anaitwa Mohammed Ussi Kheri, lakini mstaarabu yeye kakataa hakufanya fujo na ndio wa mwanzo huyo mwenye haki yake. Lakini wa pili, anaitwa Amina Juma yeye huyu ndie mkali, ndie anayetuletea pale msongomano hata matajiri waweze kuondoka na hizo fedha za kujenga skuli.

Mhe. Spika, ninamuomba sana Mhe. Waziri, sasa akafute kwa hamaki kwa sababu huyu mtu kakudharauni, mmetoa barua kwa heshima na taadhima ili kutafuta ufumbuzi, hii *double occation* tayari *automatically* sheria, nani mwenye hati ya kiwanja hiki, hajulikani sheria iko wazi. Mhe. Waziri naomba sana ukiondoka leo kafute kakudharau sana. Kwa sababu wewe umemtuma Mkurugenzi wako na amefanya kazi ya kuzuia, yeye anaendelea kujenga ana maana gani.

Halafu Mwanasheria wake anasema kuwa wewe anakwambia huna haki ya kuweza kumzuia yeye, mimi nilishangaa sana na halafu Polisi naye kakubali barua ile, anaona Mwanasheria au Wakili ana sheria zaidi, naomba sana Mhe. Waziri, hili suala tumeshachoka. Wananchi wanataka kujenga skuli ya kisasa yeye anakwenda kutuzuia. Mhe. Waziri, hilo ninakuomba sana nisaidie na lifanyie kazi.

Jambo jengine Mhe. Spika, ninaomba kuna watu ambao sasa hivi hizi eka wanajifanya wao ndio wababe, naomba sana Mheshimiwa unikabidhi Ofisa wako wa eka, tena leo hii jua lisitue. Kuna mtu eka tatu kenda kuongeza na nyengine kwa mwenzake ambazo zipo Kitope. Naomba sana Mheshimiwa hili suala liende tukalisawazishe mara moja. Naomba sana Mheshimiwa hili suala

unisaidie mimi, niko tayari kutoa mafuta kama kuna mafuta, lakini suala Mheshimiwa twende.

Mheshimiwa tangu juzi mimi nilikuwa nimenyamaza kimya, nilikuwa natafakari jinsi gani vya kusema. Mhe. Spika, watu wengi juzi walizungumzia suala la Nyanjale, mimi ndio mwenye Nyanjale sasa, naomba leo nitoe ufafanuzi mzuri wenye busara, wenye hekima na mawazo ndio Mwenyezi Mungu katupa akili sisi na sisi tunaongoza tuongoze kiakili.

Mheshimiwa suala hili niliitwa na niliwakuta kinamama siku hiyo walikuwa 15 na Diwani tukenda. Wakatwambia Mheshimiwa tumeambiwa hapa tunaondoshwa, na nani na Mwekezaji. Mimi kawaida yangu ninakuwa sina pupa kwa sababu natafuta njia za sheria na za usalama na zenye ubora, hata kama ukiniona nimekuja tena, njia zikikosana ninakuja kuripua hapa.

Mhe. Spika, nikenda kwa mwekezaji, mwekezaji akasema kweli tunataka kuwaondoa pale hatutaki kuona bandari pale, nikamwambia haya kama hutaki kuona bandari unawapeleka wapi, kule Mikokoni, mimi nikamwambia kwa hilo sikubaliani na wewe, wale binaadamu na ile bandari lazima pale wafanye shughuli zao wenye bandari. Lakini Mhe. Spika, hapa watu hawajui kutofautisha, kuna wanunuzi na watumiaji wa bandari, sasa ndio hapa mvutano ndio ulivyokuwepo.

Narudia tena Mhe. Spika, samahani sana kwa kuvunja kanuni, kuna wenye bandari ambao wenye vyombo vya bandari wanaoegesha pale na kufanya shughuli zao na kuna hawa wanunuzi ni vitu tofauti Mheshimiwa, ndio ugomvi wenyewe ulipo hapa.

Sasa ikafika pahali tumekubaliana na wale wawekezaji, kama ni hivyo sawa, bandari tunatoa tunaiacha, lakini njia hatuwapi, watakwenda kule mikokoni, nikawambia *no* bado hujanambia, mimi mpaka sasa hivi sikubaliani njia uiweke kule Mikokoni, sasa vipi, nikawambia twende kwenye bandari asilia. Tumekwenda mimi na wao nikawambia njia hii ndio itakayokuwa wanapita kwenda kule kufanya shughuli zao.

Jamaa hakufanya tabu akasema *okay* nimekubali, lakini na mimi nina maombi, hawa waanikaji naomba Mheshimiwa basi wakaanike sehemu ambayo nitawajengea Mhe. Spika, nisikilize vizuri. Hawa waanikaji sio wale watumiaji bandari, nataka ufahamu Kiswahili cha kizanzibari, ninazungumza safi. Hawa wanakijiji mimi naomba sana niwatafutie sehemu nzuri niwajengee, nikamwambia utawajengea *model* gani, nataka nijuwe, nikenda nao kule ili niwafahamishe.

Akanambia nitatoa eneo lenye kukaa wao au lenye kuweza kukaushia madagaa yao, nikamwaambi kivipi, akasema nina njia mbili naweza nikawasaidia tukikubaliana nao. Nitatoa mashine ambazo zitakausha hao dagaa wenyewe au nitawaachia wenyewe kitu ambacho wataona wenyewe kinafaa, nikamwambia maji, akasema maji nitatia *pipe* mpaka baharini mimi, nitavutia maji nitawajengea *tank* juu kubwa watashusha wenyewe kwenye hodhi halafu wataweza kuchota kwa kwenda kupikia.

Mimi nikakubaliana nae na halafu isitoshe kuna barua ambazo wale wenye bandari wamekubaliana mambo ya kuweka shughuli zao. Nikawambia kama ni hivyo, sina tatizo nalo, hawa kuchukua dagaa kule mpaka kuleta huku juu utafanya nini, akasema nitatoa gari, nitatoa na liko *tank* fulani wenyewe wanasema ni *open tank* la kuweza kupakia madagaa kuwapeleka kule.

Nikawambia hiyo mikataba si mikataba, hizi ni karatasi tu, nitatoa na gari pamoja na boti, nikamwambia bado hujazungumza, lakini ninachokwambia fanya utaratibu kwenye njia za sheria, uwatengenezee *agreement* kama mahoteli mengine yanavyofanya kwa wananchi. Hapo mimi nitajua kama hii sheria, lakini ukisema kwa mdomo itakuwa ni sawa sawa kama umeimba tu.

Mheshimiwa hiyo ndio hatua tuliyofikiana, lakini huku kukawa na zogo, mimi ninawaomba sana wananchi hiyo ndio lugha yangu ambayo ni ya uhakika hivi sasa. Mheshimiwa, niko katika harakati za kwenda mbio ili watupe hati ile ya wenyewe na lile diko lenyewe, kwa kuwa lile diko tumekubaliana kuwa itolewe hati, hakuna tatizo lolote na wale wenyewe wawekezaji *forever* kabisa pale wataendelea kukaa pale na wafanye maisha kwenda kurudi.

Mhe. Spika, nimeona nitoe ufafanuzi huo ili watu waelewe tatizo lililokuwepo kati ya mnunuaji, sio wenye bandari. Kwa sababu mnunuaji ni sawa sawa kununua samaki ukasema unampara, unakwenda kukaanga nyumbani, ndio namna yenyewe ilivyo, lakini *still* bandari iko pale pale, hawatoondoshwa bandarini, wataendelea na shughuli zao wavuvi kama kawaida yao. Naomba nitoe ushauri wa bure.

Mhe. Spika, nikiendelea na ufafanuzi wa mwisho kwa kulilia ardhi, nilisema juzi kuna mama mmoja maskini ya Mungu alijitolea yeye bure, akaitoa hati ili kuikabidhi skuli pale Regeza mwendo, lakini kuna sehemu huyu hakupewa. Naomba sana Mhe. Waziri, mama huyu asaidiwe sehemu iliyobaki aweze kufanya shughuli zao za kimaisha.

Naomba sana Mheshimiwa asaidiwe. Kwa sababu amejitolea kutoa eneo la eka kwa kufanya skuli, lakini kuna sehemu ambazo bado ninamuomba sana

Mhe. Waziri, mtume Mkuregenzi wako ende akaangalie sehemu iliyobakia tumpe na huyu mama angalau ile sehemu yenye makaburi yake alinde, yale makaburi kuwatilia *fat-ha* wazee wake. Mimi naomba sana Mhe. Spika, kwa ushauri huo, najua Mheshimiwa wangu ushatikisha kichwa, ninajua Mheshimiwa wangu utalifanyia kazi hili suala.

Mhe. Spika, niingie katika suala la mawasiliano, Mheshimiwa nina mambo madogo madogo wala sina makubwa sana. Kwanza niwashukuru sana kamati, kuna mambo ambayo tulikuwa tukiyaona na tukiyasema na nyinyi mlikuwa tayari kwenye ripoti yako unaeleza. Mheshimiwa nilisikitika sana, jengo limetafutwa mshauri muelekezi na amelipwa *foreigner* pesa chungunzima na ushauri wenyewe basi ni miwili tu katoa, hata mimi ningeitwa ningesema pale, lile jengo livunjwe au lile jengo livutwe nyuma kutokana na *run way* iweze kufanya kazi yake vizuri mikonge iingie katika *sight* iliyokubalika tunakwenda kutupa pesa nyingi Mhe. Spika, kwa tatizo hili, mshauri muelekezi katolewa nje huko kalipwa ma-f*oreign* kutoka Ufaransa na Mshimba yupo hapa hapa Jimbo la Kitope, nani atakaekubali, si kasema tu. Ni lazima Mheshimiwa tufikirie tuokoe pesa za wavusha jasho, ni kitu *very simple* kabisa. Mheshimiwa *wallahi* unafikiri mimi niseme nini panataka utaalam gani, pana *technician* pale vunja rudi nyuma, mchezo umekwisha.

Mhe. Spika, hilo suala linasikitisha sana, ninaomba sana hii kauli ifutwe sasa, tupo wazalendo humu tunatoa ushauri wenyewe huo, ili mtu alete ushauri huo kama kuna mafuta au hakuna mafuta ndio akatafute mshauri muelekezi,wakati mafuta yapo au hakuna chimba twenzetuni. Ningeomba Mheshimiwa hili suala lifikiriwe tusipoteze pesa bwana, wapo watu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, niseme tatizo letu tuangalie juzi kumetokea ajali za boti, Mheshimiwa boti zetu wanafanya tamaa hilo ukweli tuseme kuna sehemu ambazo hazihusiki kuongeza viti, lakini tunaongeza viti kwa nini hizi sheria hazifanyi kazi Mamlaka husika, jamani tusifanye mchezo zile roho za binaadamu. Tunaongeza viti kwa makusudi tofauti na umbile ambalo tumetoka nalo kuja nalo hapa sisi, ndio tunajifanya wataalam zaidi tusifike pahala hapo. Ninaomba sana hili suala .

Jengine nilizungumza siku moja suala la boti kubwa lile. Mheshimiwa hebu tuangalieni utaratibu kule kwao kulikuwa na abiria wangapi, nimesikia yaumu shaka, kwa sasa hivi kakubaliwa aongeze 1450 kama ni kweli mnahatarisha maisha ya watu, kama ni kweli ninaomba njoo Mhe. Waziri, leo uje kunijibu hili suala kweli au uongo, sio wanaongeza tu watu jamani tusikubaliane kwa tamaa ya fedha, haiwezekani. Ingekuwa inapakia hata wanyama, mimi

nisingekubali seuze binaadamu. Mimi naomba sana hili suala tuliangalie kwa mantiki nzuri tu.

Halafu Mheshimiwa siku zote mnapigania ajira za vijana, jamani gari zinatoka huko zinakuja kuchukua mizigo huku, ni njia moja ya kuhatarisha kuwa sasa hivi unga upakiwe kwa urahisi, mna *security* gani, mnatumia gari zile, zikishachukua mizigo huku uraiani, zinaingia kule ndani bandarini. Tumekaa na akili yetu tumefikiri, lakini wale maskini ya mungu wanaokaa pale wakabeba mizigo, mmewaekea vipi mnawalipa nyinyi pale wakikosa kazi.

Ninaomba sana Mheshimiwa kutokana na hali halisi hiyo kuwa hawa vijana tuwafikirie bandarini jamani tutawekeza wimbi kubwa la vijana wetu kukosa ajira. Muambieni na mshaurini, mwambieni bwana hizi gari sasa *stop* watabeba mizigo hawa, rizki yote jamani achukuwe mtu mmoja haifai. Mheshimiwa, salama leo kile kitabu chenye aya nimekisahau. Lakini kulikuwa na aya ambayo inawasaidia sana wanyonge waliokuwa wajuzi watajua aya hiyo iko wapi. Sasa leo tunakiuka aya hiyo Mheshimiwa.

Mheshimiwa leo nilisikia Mhe. Waziri, anasema kuwa watu wasijenge matuta, wende serikalini wapewe *plan*, mimi nimeshakwenda na barua yangu nimeandika ili kuwaokoa watu pale wa Mgambo, vitoto vinapondwa ovyo, vitoto vinakufa ovyo, mpaka leo sijapewa ushauri huo. Ninaomba sana kama kweli tutakuja tuone hali halisi.

Lakini Mheshimiwa, nilizungumzia suala la usafiri wa makontena, tabia yetu mpaka tuue ndio sheria itakuwepo, ndio udhibiti utakuwepo, hili suala sitolisahau maisha, jamani wanaoendesha magari haya wanakwenda mbio tuekewe utaratibu wa kusafirisha mizigo yao, tusikie jamani, tulivyoambiwa hii ni hatari.

Kwa kuendelea Mheshimiwa, *UUB* nataka niwaambie kitu kimoja, Mheshimiwa, huwa ninapita njia hii sehemu za katikati kwa Mhe. Rais, Mhe. Rais wetu hata njia tunashindwa kumtilia pale kwake kutoka pale Mchina barabarani mpaka kuingia ndani mwake, tunasahau kumtilia lami Mhe. Rais, lakini si hayo tu hata kule kwake anakokaa Rais, jasi tupu, naomba sana tumfikirie na huyu Rais wetu, tumuwekee angalau lami. Rais wetu wenyewe jamani tunashindwa kumuenzi. Barabara zake za vumbi hapo kwake vumbi na kule kwake anakokaa, vumbi tunamuweka wapi Mhe. Rais. Ninaomba sana Mkurugenzi wangu mtiifu, najua mimi nikiondoka hapa lami atakwenda kuiweka, ninaamini hivyo. Ninashukuru sana hilo.

Mhe. Spika, niwashukuru sana Shirika la Meli, nataka nijue meli zetu zinakuja lini, wanakweda vizuri, hicho tulichokuwa nacho kinasua sua, lakini nataka kujua meli zetu lini zitaanza kukabidhiwa Shirika lifanye kazi yake vizuri, ninaomba hivyo.

Kwa kumalizia nimshukuru sana Mkurugenzi wangu wa Mamlaka ya Uwanja wa Ndege, kila siku ikacha anabuni mambo mapya, lakini suala la tenda mpaka leo sijalisikia, nani aliyepewa. Ninamuomba Mhe. Waziri, leo uje kunijibu lile suala la tenda, nani sasa hivi ambaye kakubalika na serikali kupewa na kwa nini mpaka leo hii hajaanza kazi zake? Tena uje kunijibu vizuri kwa sababu hilo nakwenda nalo juu juu huko mpaka mbele ya safari, siliachi, mimi naomba sana hilo Mhe. Spika, ninakushukuru sana.

Mhe. samahani kuna moja nimelisahau ninaomba tena katika Idara ya Upimaji wa ardhi, kuna mtu amepanda midimu yake anaitwa Haji Juma, lakini alipokwenda kudai ikageuzwa kibao kenda kapewa mtu mwengine, naomba na hii mnyonge maskini ya Mungu nipewe mpimaji akaangalie Mhe. Waziri, akupe ripoti na uone mimea aliyokuwa keshaikeza pale, ninaomba Mheshimiwa apewe haki yake na ninavyokujua Mheshimiwa mambo mengi sana umefuta kwa wanyonge kuwasaidia na wae wanyonge uliowafutia wapewe wenyewe Mheshimiwa, ninakuomba sana Mhe. Waziri, *inshaalla* Mwenyezi Mungu akujaalie baada ya maka ya kwanza uende na maka ya pili, naomba sana Mheshimiwa.

Mhe. Spika, naunga mkono. Ahsante sana.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, kabla ya yote nichukuwe nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kuwa katika hali ya afya na uzima ndani ya Baraza lako hili tukufu. Lakini pia, nikushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii.

Mhe. Spika, niungane na wenzangu wale ambao wamemtakia kheri Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma na mimi niseme namtakia kila la kheri, Mwenyezi Mungu amjaalie apate nafuu na afya njema ili aweze kuja kushirikiana nasi katika shughuli zetu hizi za kitaifa.

Pia, nitakuwa mwinzi wa fadhila hasa nikiwa mimi ni mwanachama wa Chama cha Mapinduzi kama sikutoa pongezi za dhati kwa Chama changu cha Mapinduzi kwa kuweza kuhakikisha kwamba, ushindi wa Jimbo la Kiembesamaki wanachukua Chama cha Mapinduzi. Pia, nimpongeze mtoto wetu Mahmoud Thabit Kombo, niseme tu msimamo huo huo wa Chama cha Mapinduzi majimbo yote yao. Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, sasa nije katika uchangiaji.

Mhe. Spika, mimi bado namwambia Mhe. Waziri, nitamganda mpaka dakika ya mwisho kuhusu uwanja wa ndege wa Pemba. Mhe. Spika, uwanja wa ndege wa Pemba nimeuona kuwa angalau umepelekewa *bulldozer* umesafishwa safishwa, umetiwa uzio, pia nashukuru kwa wizara kufanya hivyo. Lakini hiyo si moja wapo ya maendeleo kwa uwanja wa ndege wa Pemba.

Mhe. Spika, kila nikisimama hapa si wakati wa bajeti, wala wakati wa kuchangia hizi ripoti, mimi namshika Mhe. Waziri, kuhusu uwanja wa ndege wa Pemba kwa malengo, kwamba imefika wakati tubadilike, hebu ule uwanja wa Pemba tuutupie jicho Mhe. Spika. Kwa kweli ni aibu naweza kusema.

Mhe. Waziri, nilichangia wakati wa bajeti hapa kuhusu habari ya jengo na mambo yake yote yanayohusiana na jengo, akanambia maneno mengi, maana waziri akiondoka akikaa mwengine mambo yote anakamata yule aliyekuwepo kwa wakati ule. Lakini pia, nikazungumza kuhusu habari ya taa, jamani kweli wakati huu wa sayansi na teknolojia ule uwanja wa Pemba tunashindwa kuzitia hizi taa, kulikoni. Kule wanakwenda viongozi, si viongozi tu hata wananchi wanasafiri na siku hizi *Alhamdulillah* ndege kwa wingi, linaweza likatokea tatizo lolote lile kwa kweli tukashindwa kuokoa roho za wananchi.

Mhe. Spika, namwambia Mhe. Waziri, kwa sababu hizi ni ripoti, lakini wakati wa bajeti nitachukua shilingi katika mshahara wake, kama sikupata ufumbuzi wa uwanja wa ndege kuhusu habari ya taa pamoja na matengenezo ya jengo kwa kweli nitachukua shilingi, sasa atakuwa na hiari yake nikiichukua shilingi na yeye hapati mshahara. Hilo nalitahadharisha na mapema.

Niendelee Mhe. Spika, kuhusu mambo ya vyombo vya moto. Mhe. Spika, hivi karibuni tulipotembelea na kamati yangu tulikuwa tunakwenda Makunduchi, tulimuona mtoto wa miaka minane anaendesha gari. Bahati nzuri kule mbele kulikuwa na watoto wetu wa usalama barabarani, lakini sisi ndio tulikuwa tunaelekea Makunduchi hatukujua wakati wa kwenda kama walisimamishwa na usalama barabarani au vipi, tukashangaa kwamba mtoto yule kapewa gari anaendesha. Hilo moja.

Jengine ni kwamba sasa hivi utoaji wa leseni za uendeshaji wa gari Mhe. Spika, watoto ni wadogo sana, sijui tunatoa kigezo gani kuwapa watoto wadogo, maana tunajua kwamba watu wanafoji umri humu ili kuonekana mtoto ameshatimia umri wa miaka 18 au 21. Sasa namuomba Mhe. Waziri na hili aliangalie vizuri, ashirikiane na vyombo husika waliangalie.

Mhe. Spika, kubwa zaidi sasa hivi kuna uendeshaji wa vespa, watu wanakaa tako moja na toka ilipoanza tabia hiyo, vespa zimeshauwa watoto wengi tu,

tunavyoarifiwa ni kwamba ukishakuwa una mashindano ya vespa ya tako moja, unaambiwa utoe *break*, ukishakutoa *break*, wewe ndio unafukuzana tena lolote unalokumbana nalo huko wewe na Mungu wako na ndio maana vijana wetu wengi wameshakufa hivi sasa.

Hata na mahonda haya makubwa makubwa nimuombe Mhe. Waziri na vyombo ambavyo vinashirikiana na yeye na niwaombe watu wa usalama barabarani suala hili kwa kweli lizingatiwe kwa makini, si hivyo, tutapoteza vijana wetu nguvu kazi ambao wataweza kuja kusaidia taifa hili.

Nikiondoka hapo Mheshimiwa, niende kwenye Bandari. Kwanza nisiwe mwinzi wa fadhila bandari yetu sasa hivi kwa upande wa abiria wanaopanda hivi vyombo vya kwenda Dar-es-Salaam ni bandari nzuri na nimpongeze sana ndugu yetu Said Bakhresa, ambaye amefanya mambo mazuri. Kwa sababu kilikuwa kilio cha siku nyingi, lakini kutokana na uzalendo wake amejitahidi na ataendelea kujitahidi, naomba tumpe fursa pale ambapo tunahisi hapa kwa upande wa bandari, basi tumpe fursa ambazo anaweza kuzikamilisha. Kwa sababu huyu ni mzalendo bora ajenge kwao na kwa wenzao, lakini kwao bora zaidi.

Nimuulize Mhe. Waziri, sijui katembelea bandari yote, sio pale palipotengenezwa vizuri tu na Bakhresa, kaitembelea bandari yote mpaka huku Malindi kuona hali halisi ilivyo? Mhe. Spika, nataka aje anipe maelezo mazuri, kwa sababu ukija katika sehemu ile ya wauza samaki, kwa kweli wakati mwengine bandari ile inatumiwa vibaya. Nimuombe sana Mhe. Waziri, kama katembelea sina matatizo, atakuja kunipa maelezo, kama hajatembelea, basi aizunguke bandari yote ili kuhakikisha kwamba kweli matumizi ya bandari yanafanyika kwa mujibu wa taratibu na sheria zilizowekwa, hapo ndio nitaridhika.

Pia, Mhe. Spika, nije katika ile ile sehemu ya usafiri, *parking* bado haijawa madhubuti, bado haijaridhisha Mheshimiwa, hebu tufanyeni utaratibu wa kuhakikisha *parking* ile ya watu wanaotoka Dar-es-Salaam na magari yale wasaidieni. Kwa sababu wakati mwengine boti inakuja unachukua saa nzima unataka kutoka hii sehemu ya Mji Mkongwe huku kuja zako bandarini, basi unashindwa, unakaa nusu saa nzima hujapata nafasi ya kupita. Naomba tuangalie uwezekano ni upi wa kuhakikisha kwamba pale penye *parking* panapakiwa vizuri ili watu wajiridhishe, wasafiri na wale wanaotoka maofisini maana na wao tunawapa shida.

Nikiondoka hapo kwa sababu mazungumzo mengi, nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati hii kwa kweli ameeleza hali halisi ilivyo, lakini na mimi nilisema nitupie hapa na pale nije katika suala la ardhi.

Kwanza nimshukuru Mhe. Waziri, kwa jitihada yake, kwa sababu amesimamia mambo mengi katika yale maagizo ambayo tunayatoa. Lakini nimwambie bado Mhe. Waziri, ajifunge tena mkaja, bado matatizo ya ardhi yapo. Mimi ningesema tunakosa kujipanga, lazima tujipange. Sisi tuna mikoa hebu tujipange kimikoa tuangalie ardhi yetu ikoje, mwisho Mhe. Spika, tutakuja kushindwa hata kuweka kisiki cha muhogo jinsi tunavyoivamia ardhi. Ukiangalia ukiweko angani ile minazi, mana sifa ya Unguja ilikuwa minazi mingi, sifa ya Pemba karafuu nyingi.

Leo ukitembea angani ukiangalia minazi iliyokwishaangamizwa ni mingi sana, leo Kisiwa cha Unguja minazi iliyopo tunauziwa nazi shilingi 1,000. Mhe. Spika, si maajabu hayo. Pamoja na kwamba mambo yamepanda, lakini si kuuziwa nazi shilingi 1,000. Mwananchi wa Unguja ananunua nazi shilingi 1,000. Namuomba sana Mhe. Waziri, tuangalie *plans* zetu, tusiangalie *plans* ya mji tu, tuangalie pia na *plans* za mikoa tunafanyafanyaje ili kuhakikisha kwamba tunaokoa ardhi ili wakulima wetu wapate kulima kwa busara na waweze kuzalisha chakula ili kuweza kuendesha maisha yao vizuri. Namuomba sana Mhe. Waziri, tufanye *survey* katika mikoa yetu.

Mimi jana nilikwenda pahala basi nilikaa hivi juu ya kilima, nikaona majumba hayo na kulikuwa hata kwenda kwa miguu hufiki, lakini niliona majumba tena majumba. Sasa pia naishukuru hii Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mhe. Spika, maana watu wanasema umasikini, tunakufa njaa, tunafanyaje, hee, jamani nyee!

Tumuombe Mwenyezi Mungu asije akatuelekeza huko, tumuombe atuendeleze na mambo yetu kwa sababu sasa hivi nchi hii iko huru toka mwaka 1964 watu wanafanya wanavyotaka, wanajenga, wanafungua maduka, Mwenyezi Mungu awazidishie tumuombe twende hivi hivi, lakini tusijiombee shari Mhe. Spika. Mwenyezi Mungu atupe kila la kheri, atupe amani, atuletee busara tuongozane katika amani hii hii tuliyonayo. Niwaombe wananchi kwa sababu wamepewa uhuru wa kufanya wanavyotaka, isipokuwa tu ufuate taratibu na sheria.

Kwa hivyo, niseme Mhe. Spika, kwamba namuomba Mhe. Wazir, bado aendelee na kufanya *survey* kwa kila mkoa.

La mwisho, Mhe. Spika, wakati tunapotembelea sehemu mbali mbali katika kamati, tukenda maeneo ya ukanda wa pwani *Wallahi* wawekezaji wengine wamepewa maeneo maana utajiuliza na mengine hata kujengwa hayajaanza na yanaweza kufika wengine wamepewa maeneo haya hata miaka kumi hawajafanya chochote. Sasa unajiuliza hakuna sheria na sheria tunazipitisha sisi wenyewe humu. Lakini mimi niseme ni maeneo makubwa sana Mhe.

Spika, sisemi kwamba nchi hii wawekezaji wasije, waje lakini wafuate taratibu na sheria.

Ukienda upande huu wa Uroa, ukitoka ukuta huu unaingia ukuta mwengine, ukitoka ukuta mwengine, unaingia mwengine na ukienda humo hamjajengwa Mhe. Spika, hebu Mhe. Waziri, aje atwambie na hawa wenzake anaohusika nao wanaokaribisha vitegauchumi hao, aje atwambie kulikoni, yale maeneo yatajengwa lini.

Kwa sababu watu wanakuja hapa wanawalevyalevya wananchi wetu na mtu masikini akioneshwa shilingi milioni tatu, milioni nne, anaziona nyingi, lakini toka wakati alipouziwa yeye, huyo sasa hivi huwezi kupata eneo lile kwa shilingi milioni tatu, labda kwa shilingi bilioni mbili, bilioni mbili kwa maeneo yaliyowekezwa eneo la mtu mmoja tu.

Kwa hivyo, mimi namuomba sana Mhe. Waziri, alifuatilie na wenzake hili tuhakikishe kwamba yale maeneo aidha yanafanyiwa kazi au watizame ni kitu gani ambacho kinasababisha. Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, na mimi niseme naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja, lakini naomba tu wizara husika hizi tunazozielezea mambo haya, ziweze kuchukua mkondo wake na waweze kuhakikisha kwamba mambo yanakwenda sawia ili kuwaridhisha na wao wananchi matakwa yao.

Baada ya kusema hayo, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Asha Bakari Makame, inaonekana jana kazi ilikuwa kubwa sana, watu wengi wamechoka mno. Nadhani watajitahidi ili tuweze kwenda na kazi zetu vizuri pamoja na machofu ya kazi ya jana, maana wengine wamelala kabisa ndani ya ukumbi huu. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kunipa nafasi hii kuzungumza machache katika ripoti hii aliyoisoma Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. Lakini vile vile, na majibu ya Waheshimiwa Mawaziri wa Miundombinu na Mawasiliano na Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Spika, kwanza na mimi kama walivyoanza wenzangu, nataka niwapongeze wananchi wote wa Zanzibar kwa mshikamano wao, lakini vile vile, wananchi wa Jimbo la Kiembesamaki kwa kuweza kufanya uchaguzi bila ya matukio ya aina yoyote ya kuathiriana kimaisha, lakini vile vile, bila ya vurugu zozote.

Mhe. Spika, hii kwa kweli inaonesha kwamba pamoja na matatizo madogo madogo tunayotofautiana kisiasa, lakini bado kila siku zikienda Wazanzibari tunazidi kuvumiliana. Kwa hivyo, tunawapongeza sana wananchi wa Jimbo la Kiembesamaki, lakini na wananchi wote wa Zanzibar kwa kuweza kipindi chote hichi cha uchaguzi na jana imefikia hatima kwamba hakuna aliyepata madhara yoyote. Tunawapongeza kwa hilo tunaomba waendelee.

Lakini vile vile, nimpongeze aliyeshinda na tunamuomba Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema, aje hapa Barazani ili aweze kuapishwa na kuweza kushirikiana naye katika kujenga Zanzibar. Lakini vile vile, kuweza kutoa huduma kwa wananchi wa Jimbo la Kiembesamaki. Baada ya hayo sasa nataka niende moja kwa moja katika ripoti.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze moja kwa moja katika ufafanuzi alioanza kuutoa Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, alipokuwa akitoa ufafanuzi katika maagizo ya kamati ya mwaka uliopita. Kidogo nina masikitiko kuwa ile *statement* ya Mhe. Waziri, kwamba agizo lilitoka tangu mwaka jana kuwa Mamlaka ya Mji Mkongwe wakae na watu wa Mamlaka ya Maji ili kuweza kutatua tatizo la maji pale katika bustani ya Forodhani. Sasa labda pengine sikufahamu vizuri, lakini kama mpaka sasa hivi bado mazungumzo yanaendelea baina ya taasisi hizo mbili ambazo zimo ndani ya wizara moja, mimi nahisi *speed* ya utendaji wa serikali kwa hali hii tutachelewa sana kufika. Sasa naomba maelezo ya ziada hayo mazungumzo yamefikia wapi, tatizo la ufumbuzi wa maji limeshapatikana pale kwenye bustani ya Mji Mkongwe au vipi.

La pili, Mhe. Spika, katika wizara hii hii ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati pia naendelea kuwa na masikitiko hasa kwa wananchi wanaofutiwa maeneo yao na kupewa watu wengine au taasisi nyengine bila ya ridhaa yao.

Mhe. Spika, bado tunaendelea kupata malalamiko wananchi wanazo hati zao, lakini serikali inakuwa inatoa hati nyengine. Kwa hivyo, wale wananchi bado wanaendelea kunung'unika. Sasa mimi kama kawaida yangu Mhe. Spika, nitarudi tena kwa Mhe. Waziri, ili akae na watu hawa kuweza kupata ufumbuzi. Kwa sababu wananchi kuendelea kulalamika hasa katika masuala ya ardhi kwa kweli haituletei taswira nzuri. Lakini moja nataka nilieleze *specific* la Nungwi.

Mhe. Spika, wananchi wa Nungwi walilalamika kwa muda mrefu na walifika hapa Barazani ikafika pahala wakaonana na Kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Kwa sababu walikwenda mpaka kwa Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa. Kwa hivyo, kamati yangu ikahusika moja kwa moja katika kushughulikia mgogoro ule.

Tulikaa nao wale wazee tukajaribu kuwaambia watuletee *documents* zao, wanazo *documents* halali kabisa ambazo wamepewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini eneo lao amepewa mtu mwengine mashuhuri. Sasa sipendi kutaja majina ya watu, lakini mimi nikisema mashuhuri nadhani Mhe. Waziri, atakuwa anafahamu.

Mimi naomba, kwa kuwa kipindi hiki Mhe. Waziri, amefanya kazi kubwa sana tena nzuri ambayo ya kuipongeza kuwaita watu pale anapowapa hati, anamwita mtu *physical* amuone sura yake kama kweli yule mtu anayempa lile eneo ni yeye mwenyewe mhusika. Kwa sababu zamani watu walikuwa wanapewa hati mtu hewa, manaake mtu akitafutwa haonekani, lakini sasa hivi utaratibu umekuwa mzuri.

Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri, kipindi hiki kuna baadhi ya maeneo aliyafuta ambayo yalikiuka taratibu za kisheria. Sasa mimi naomba sana ili kuondoa mgogoro kwa wananchi wale wanyonge wa Jimbo la Nungwi, wazee washahangaika sana kila siku hawaondoki Barazani na kila tunavyoangalia bado wana haki yao ya msingi katika ardhi waliyorithi kwa wazee wao na serikali imewapa *document,* naomba sana Mhe. Waziri, huyu mtu ambaye alipewa lile eneo la wananchi, basi katika hayo maeneo yaliyofutwa aweze kubadilishiwa hati akapewe eneo jengine, lile eneo lile wapewe wale wananchi. Mimi nafikiri huo ni ushauri ambao najaribu kumsaidia Mhe. Waziri, ili kuweza kuondoa mgogoro. Kwa sababu vyenginevyo wale wananchi wameshahangaika sana na kushatokea purukushani nyingi kwa yule mtu aliyepewa. Kwa hivyo, nafikiri si jambo la busara kuendeleza mgogoro ambao hauna faida. Kwa sababu ni mtu ambaye hakai Nungwi, lakini wale wananchi wa Nungwi wao ndio wana hati.

Sasa kwa nini asiondolewe yule mtu ambaye si mtu wa Nungwi akapewa eneo jengine, lile eneo wakaendelea kupewa wenyewe watu wa Nungwi wakaliendeleza ili kuwasaidia katika maisha yao. Kama tunavyosema utalii wetu tunataka zaidi uwafaidishe wananchi wawekezaji wafaidike, lakini na wananchi wawezekufaidika. Sasa hili kwa kuwa nilikwishakuzungumza na Mhe. Waziri, nilikuwa najaribu kumkumbusha ili *hansard* ionekane kwamba naendelea kumkumbusha. Mimi naomba sana Mhe. Waziri, hili najaribu kumpa ushauri huo naamini ataufikiria ili wale wananchi wa Nungwi waweze kupata haki yao.

Mhe. Spika, nikiendelea katika wizara hii, mimi kidogo sikubaliani na ripoti ya Mwenyekiti wa Kamati aliyosema lile eneo la pale Malindi la yule mzee wetu Mhe. Naibu Spika, Mstaafu kwamba afutiwe apewe eneo jengine. Mheshimiwa, ardhi inategemea eneo, ile ardhi amepewa ana hati zake za kisheria na Mhe. Spika, mtu unapomuondoa eneo moja kumpeleka katika

eneo jengine, vile vile, angalia na thamani ya ardhi na eneo iliyokuwepo hiyo ardhi.

Leo ukimuondoa pale ukienda kumpeleka Tunguu au wapi huko, nafikiri tunazidi kumuumiza yule mzee wetu. Mzee wetu yule amewatumikia wananchi wa Jimbo la Rahaleo kwa muda mrefu na katika kipindi chote kwa kweli wananchi walimpenda sana, hata sisi hapa Barazani alituongoza kwa kipindi kirefu tunamshukuru sana, lakini sasa tusimuumize katika hali ya maisha ya baadae.

Mhe. Spika, wenzetu nchi zilizoendelea wanatengeneza sheria ambazo zitawafanya wanapokuwa uzeeni waweze kuishi vizuri. Sasa sisi si busara kwamba leo mwenzetu yule alipokuwa na nguvu zake, leo nguvu zimeshaanza kupungua tunamuumiza. Mhe. Spika, mimi namuomba sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati katika ile ripoti yake kwa hili atustahamilie. Mzee wetu yule hali yake tunamujua na namuomba apate siku moja aende akamuangalie, amuone ile hali yak, halafu atizame na hayo maneno aliyoandika katika ripoti yatalingana? Kwa hivyo, mimi nadhani Mhe. Spika, Mhe. Mwenyekiti wa Kamati mahiri kabisa na pia Mwenyekiti wa Baraza, basi tunaomba shufaa kwa mwenzetu huyu aweze kutumia ardhi yake ile ili iweze kumsaidia katika maisha ya baadae yanayokuja.

Mhe. Spika, nikiendelea, vile vile, nakuja sasa katika Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu. Bado mimi nataka niseme kilio changu kiko pale pale kwa suala la *VIP* kwa Waheshimiwa kupita kwa utaratibu wa heshima waliopewa na wananchi. Hili tutaendelea kulisema. Mhe. Spika, kama mamlaka wanataka kujenga *VIP* ya kutoza kodi, basi wajenge nyengine ile ni *VIP* ya wananchi, *otherwise* serikali, basi na sisi ituruhusu tupite ule uwanja wa zamani wanaopita wakubwa, maana katika wakubwa nchi hii na sisi tumo.

Sasa nadhani Mhe. Spika, katika suala la malipo kwa Waheshimiwa *VIP* bado tunaendelea kusema Mhe. Waziri, hii ni mamlaka yake yeye, sio mamlaka ya mtu mwengine yoyote.

Kama tunavyojua uwanja wetu pamoja na kwamba tunauita *International*, lakini bado hatujakuwa na zile *local airport*, kama tungekuwa tuna *local airport* hiyo, *international* sisi wala tusingepita tungekuwa tunasafiria huko. Kwa sababu leo ukiangalia sisi Unguja na Pemba hatuna muungano ni nchi moja.Kwa hivyo, leo mtu anapotoka Pemba anakuja na familia yake au anapotoka Unguja anakwenda na familia yake Pemba, leo ukamtoze kod, mimi nafikiri hiki kitu si kizuri sana.

Kwa hivyo, naomba sana katika eneo hili Mhe. Spika,bado Mhe. Waziri, atumie mamlaka yake ya uwaziri huo uwaziri amepewa kwa mamlaka tena kisheria kabisa, atumie nafasi yake ili kurejesha heshima ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, nikiendelea katika hii hii Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano najaribu kuzungumzia suala la bandarini. Bandarini namuomba sana Mhe. Waziri pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ hayupo, lakini najua mawaziri wengine wapo na serikali ipo, eneo lile la bandarini pale hasa kwenye madagaa huku, Mhe. Spika, kuna wizi unakuwa unafanyika. Kuna wizi wa mafuta unafanyika tena kwa madumu bila ya kificho wazi wazi.

Sasa sisi tunajiuliza madumu yale ya mafuta yanakuwa yanatokea wapi? Mhe. Spika, tunaomba eneo lile la bandari ya madagaa kule nyuma na ile sehemu iliyokuwa *fisheries* zamani palikuwa na upenyo pale, kama ukikaa hufiki siku tatu utawakamata watu na madumu ya mafuta.

Mhe. Spika, hili mimi naomba sana Mhe. Waziri, na lile ni eneo mtambuka kwa sababu waziri yeye bandari yake, lakini vile vile kuna waziri mwengine anayeshughulikia masuala ya ulinzi wa maeneo yetu ajaribu kuliangalia hili.

Vile vile Mhe. Spika, na hili nitaendelea tena kusema suala la Umiliki wa Meli kuendelea kutoa mizigo wao wenyewe bandarini wakaipeleka mpaka kwenye maduka ya watu au kwenye maghala ya watu.

Mhe. Spika, hii ni moja katika njia ya uingizaji wa madawa ya kulevya. Suala hili mimi sitolikubali na namshauri Mhe. Waziri bandari ni yako hata mtu kajenga itakuwa kajenga kwa matakwa yake kwa mapenzi yake tunampongeza, lakini bado mamlaka ya matumizi ya Bandari serikali ndio iwe ina nguvu kwa ajili ya matumizi ya bandari.

Kwa sababu hili Mhe. Spika, leo mtu anaweza akalizungumza labda anaweza akahisi ana chuki na mtu falani, lakini siku itakayoonekana gari yake imepakia madawa ya kulevya hapo ndipo atakapokuja kukumbuka kumbe yule kijana alisema alikuwa ananitakia mema.

Kwa hivyo, mimi naomba sana huu utaratibu bado kama inavyokaguliwa mizigo mengine, mizigo yote inapotoka bandarini ikaguliwe ili baadae wenye mizigo yao wachukue waipeleke wanakotaka.

Mhe. Spika, hivi juzi tu tulishuhudia hapo Uwanja wa Ndege kuna mabegi pale yaliachwa na hayana mwenyewe, mabegi siku hizi yanatembea wenyewe

yamefika mpaka Uwanja wa Ndege mwenyewe hakuna. Sasa na hili nilikuwa najaribu kulizungumza tena ili uonekane umuhimu wake. Hatuna chuki na mtu, tunapenda maendeleo lakini vile vile tunaomba utaratibu wa mizigo bandarini ufanywe kama wanavyofanyiwa wengine.

Chengine najaribu kuzungumza na wenzangu wamelizungumza na mimi nitaligusia kidogo suala la machine ya *x-ray* pale Uwanja wa Ndege wa Zanzibar. Mhe. Spika, katika hali ya kawaida zile *x-ray machine* tunajua zinaongozwa na binadamu lakini bado na uaminifu wa wale watu wetu tunaomba sana uendelee. Mashine zinunuliwe lakini na suala la *CCTV camera*. Tuliuliza tukaambiwa kuwa sasa hivi Uwanja wa Ndege ipo. Lakini bado katika tukio la juzi la Uwanja wa ndege hatuna uhakika, lakini tuliambiwa kuwa *CCTV camera* eneo lile aliyeleta mabegi haikumuona.

Sasa mimi naomba Mhe. Waziri hili bado ni jukumu lako uangalie anavyofanya mwezako Mhe. Mwakyembe kule anaingia mwenyewe katika suala la kupambana na madawa ya kulevya. Tunataka huyu aliyekabidhiwa *CCTV camera* atwambie kwa nini *CCTV camera* haikumuonesha mtu aliyeleta mabegi ya madawa ya kulevya uwanja wa ndege. Na kama haijamuonesha kazi haimfai wala haijui aondoke mara moja.

Mhe. Spika, lazima tuwe wakali, makini Mhe. Waziri ukisema kwamba mimi niko ofisini mambo yamefanyika Uwanja wa ndege mwenzetu Mhe. Mwakyembe yuko ofisini lakini na uwanja wa ndege anakwenda vile vile, tunaomba ufuate nyayo zake.

Mhe. Spika, tulileta ripoti hapa ya Kamati Teule siku nyingi. Serikali ikaleta jawabu na tukawaambia kuwa kuna maeneo hatukuridhika. Pale kuna uwekezaji mkubwa kuna *hangar* waliyopewa wale *Tropical. Hangar* lile lilikaa zaidi ya miaka 20 lilikuwa halilipiwi kodi. Lakini ndege pale zinakwenda zinatengenezwa wanafundisha marubani fedha nyingi sana hatujui zilikuwa zinaenda wapi. Maelezo mpaka leo hatukupata.

Kuna *hangar* jengine ambalo alikodishwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Uwanja wa Ndege. Bado yeye ndiye Mkurugenzi na yeye ndiye mwenye *hangar*. Mhe. Spika, *hangar* lile tulisema tulipokwenda sisi kamati miaka mitatu halikulipiwa ada. Lakini vile vile Mhe. Spika, tulieleza hata hiyo kodi ambayo amekodishwa ni U$ 220 kwa mwaka ilikuwa U$ elfu 2400. *Hangar* lile sasa hivi karibu U$ elfu 20 kwa mwaka serikali imemkodisha kwa U$ elfu 2400. Sasa Mhe. Spika, tuko makini kweli leo tunazungumza *OC* tumepata shilingi ngapi sijui mashine za *X-ray* hakuna. Mapesa yapo lakini mnayaangamiza.

Sasa mimi nilikuwa naomba Mhe. Spika, kwa sababu huyu anayedaiwa yeye mwenyewe anajidai atajilipa huyu. Sasa hebu tufike pahali serikali iwe makini sana. Jamani mimi naomba sana na hapa ndipo tulipozungumza haya maadili ya uongozi hayakubaliani na hili tunaendelea kulisema. Kwamba mwekezaji abakie kama mwekezaji mtu aliyepewa dhamana ya kutumikia umma abakie kutumikia umma. Huwezi ukawa na Mkurugenzi halafu hapo hapo anaendesha *hangar* katika Mamlaka ya Uwanja wa Ndege. Hilo suala hatuwezi kukubaliana nalo, na hili ndio litakalosababisha safari hii Mhe. Spika, mwezako kaondoka na wewe utakuja kuondoka kwa masuala ya *hangar* la Uwanja wa Ndege hapa lazima tujue moja. Sisi kwanza tunataka *hangar* letu lirudi serikalini halafu mambo ya makubaliano na mapatano tutajua baadae. Vyengine Mhe. Spika, safari ile bajeti uliipitisha wewe lakini safari hii tutakuzuia.

Mhe. Spika, namalizia hapo hapo Uwanja wa Ndege bado naomba sana ule unyanyasaji uondoke kuwalipisha ada shilingi mia tano mpaka wale wafanyakazi wanaofanya kazi Uwanja wa Ndege. Akienda kunywa chai akirudi na gari yake mia tano jamani hii tunakwenda wapi.

Mhe. Spika, tulishauri wapewe stika walipewa stika mwezi mmoja ili Baraza lioneshwe kwamba stika zimetolewa. Siku ya pili utaratibu uko pale pale. Leo watu wanazuiliwa mpaka vibali vya kuingilia mle uwanja wa ndege wakati wao wamewekeza ndani ya Uwanja wa Ndege. Ndio maana tukasema jamani Uwanja wa Ndege wa Mtu. Mimi nilishauri ubadilishwe jina. Lakini mpaka leo sijui mnaogopa kitu gani.

Jengine kubwa zaidi na tumelizungumza sana pale Uwanja wa Ndege kuna mapato ya *visa* yanapotea. *Visa* zinalipwa pesa mkononi na tukashauri pale Benki ya Watu wa Zanzibar ifungue kijitawi kidogo cha Benki. Leo watu binafsi wamekwenda pale wamepewa nafasi na wale walikuwa hawalipi kodi. Leo Benki ya Watu wa Zanzibar kuweka pale kijiofisi chao yakaweza malipo ya *visa* kulipiwa kwa njia ya benki. Mpaka leo mtu anakataa. Sasa huu uwanja wa serikali au wa nani? Mhe. Spika, mimi namuomba sana rafiki yangu, swahibu wangu yeye alikuwa akiuliza sana serikali *are we serious*? sasa na yeye tunamuuliza *are you serious*?

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, naunga mkono ripoti ya kamati lakini vile vile bado nitahitaji maelezo ya zaida kwa mawaziri.

Mhe. Spika, samahani kidogo kuna moja namkumbusha tu Mhe. Waziri pamoja na Mhe. Waziri wa Ardhi suala la muwekezaji yule anayefundisha marubani wa *Air strip* ametaka eneo la kujenga kiwanja cha ndege kidogo kwa ajili ya kufundishia marubani. Mpaka leo Mhe. Spika, serikali inampiga

danadana. Tunajiuliza leo tunakwenda Ulaya, Marekani, China kutafuta wawekezaji, wawekezaji wamekuja tunawasumbua. Twambieni kuna tatizo gani? Kwa sababu serikali tatizo lenyewe haina majibu huyu ukienda huku waziri mwengine anakwambia hivi hebu tunataka majibu ya serikali.

Je, yule mwekezaji aliyekuja kuwekeza katika kufundisha marubani lile eneo lake ataweza kuwekeza au hawezi? Na kama hawezi kwa sababu gani? Mhe. Spika, tumeshaona mwenzetu Dar-es Salam helikopta zinatua katika viwanja vya kawaida kabisa tena wawekezaji binafsi. Yule mwekezaji Mhe. Spika, ndege zake zile zina uwezo wa kutua mpaka baharini. Juzi nilizungumza kuhusu maafa zina uwezo wa kutua mpaka baharini, maafa yanayotokezea haya wangetusaidia sana. Mpaka leo wanawasumbuasumbua.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache nakushukuru sana. Kama ingelikuwa ripoti ya wizara nisingeuka mkono. Lakini kwa kuwa ripoti ya kamati kwa kweli Mhe. Mwenyekiti nakuunga mkono, lakini lile moja naomba turuhusu sisi, lile la mwenzetu swahibu wetu. Mhe. Spika, nakushukuru. (*Makofi*).

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kupata nafasi asubuhi hii kutoa machache juu ya kamati ya mawasiliano na ujenzi.

Mhe. Spika, mimi ni Mjumbe wa kamati hii kwa hivyo sitokuwa na mengi ya kuzungumza kwa sababu tumeipata na wenzangu katika taasisi za wizara ambazo ziko chini ya kamati hii. Tumepata maelezo mbali mbali na mengi ya maelezo tuliyopata kwa kweli tuliridhika nayo.Lakini juu ya hivyo mimi nitaanza kwenye Shirika la Umeme. Hapa nilikuwa nataka nizungumzie jambo moja tu deni lake kwa *Tanesco*.

Mhe. Spika, tulipokwenda *Tanesco* tulipata maelezo ya kupewa indhari, kama ingelikuwa ni mchezo wa mpira basi tayari tumepewa *yellow card*. Mhe. Spika, na kama deni hili halitolipwa basi iko siku *Tanesco* itaipa *ZECO red card* na wakitoa *red card* ni kutuzuilia umeme wao wanaotuuzia ambao wanatudai sana.

Mhe. Spika ingawaje deni lina utata; wao wanatudai wanatudai bilioni 70 sisi tunasema 40. Kwa vyovyote kesi ilivyo tuna deni tena kubwa na deni hili linapaswa lilipwe. Lakini Mhe. Spika, kama itafika hatua ya sisi kuzimiwa umeme itakuwa serikali yenyewe ndio iliyokubali huu umeme ukatwe. Kwa sababu Taasisi za Serikali nazo zinadaiwa na *ZECO* na hazitaki kulipa. Hasa hapo wakija kukata wenyewe ndio tutajua tufanye nini.

Juzi tu hapa kwenye Shirika la *ZBC* tuliona kuwa wana deni la milioni 489 peke yao hawajalipa na wengine. Sasa mkusanyiko wa madeni haya wanaifanya *ZECO* kushindwa kwenda kwa ufanisi kama walivyojipangia.

Mhe. Spika, ikifika hatua ya Zanzibar kukatiwa umeme ningeishauri serikali ihakikishe kuwa inalipa madeni yake kwa *ZECO* ili kuifanya *ZECO* ifanye zake kwa ufanisi. Itafika wakati hawa watashindwa kutuvumilia kiasi kwa sababu wanatuenga enga kiasi, tunafanya mambo halafu ikatuacha kati kati wakarudi nyuma. Iko siku watakuja kuweka siasa upande waweke uchumi wao mbele. Ningeomba taasisi za Serikali zinazodaiwa zilipe madeni yao. Kama tulisema mgao sasa basi utarudi upya na tutakuwa hatuji mwisho wake lini. Ningeomba taasisi za Serikali zinazodaiwa zilipe madeni yao.

Mhe. Spika, ripoti yetu imesema kwamba kuondoa matatizo haya tufunge umeme wa LUKU ili mtumiaji akitumia ukimaliza ni hiari yake. Hili ni zuri isipokuwa kwenye vituo vya afya zaidi Hospitali kubwa naomba hili tusifanye kwa sababu ya wagonjwa waliokuwepo kule tunawatarajia wapoe na waweze kuleta huduma katika nchi, lakini taasisi nyengine zote za kawaida ni vyema wakafungiwa umeme huo na ukimalizika uwe umemalizika kama hawakununua mwengine ni hiari zao.

Mhe. Spika, nije katika vituo vya kuuzia umeme zaidi kule Pemba. Kwa sababu taratibu nyengine hazijakamilika. Ni vyema vituo vya umeme kuongezwa Pemba pamoja na matatizo yote yaliyokuwepo hasa Wilaya yangu ya Mkoani. Ningeomba pale Mtambile ni kama *center* ya Wilaya ya Mkoani kikawekwa hiki kituo cha kuuzia umeme ili wakawapunguzia matatizo watu wa Chambani, Muwambe, Kiwani, Kangani na kadhalika.

Mhe. Spika, nije kwenye hii Mahakama ya ardhi inayoshughulikia matatizo ya ardhi ambayo katika nchi hii ardhi imechukua sehemu kubwa ya mizozo iliyopo kuliko sekta nyengine yoyote. Mhe. Spika, ushauri wangu kwenye mahakama hii ili iweze kufanya kazi iwe na ofisi nzuri ya wafanyakazi wazuri wanaoweza kujitosheleza kwa kazi zao. Tuanzishe ofisi tutafute pahala pazuri pa kufanyia kazi sio kituturi.

Mhe. Spika, nije katika nyumba ya Kengeja kama yuko aliyeiona na akawa na uwezo kidogo licha ya kukaa mwanaadamu hata ya kuweka kuku wake angelikuwa hataki, angelihofia kuwa wale kuku wangu wataangukiwa na lile jumba, kutokana na unyonge bado watu wanaishi katika nyumba ambayo ni mbovu kweli kweli. Serikali iliombwa angalau ifanyie marekebisho madogo madogo hivi vijipesa kidogo vilivyoombwa nayo hata senti moja hazijaingizwa. Mimi nina wasi wasi serikali inakuja kungojea kuweka bendera nusu mlingoti baada ya watu kadhaa kuja kuangukiwa na jengo lile,

lakini nyumba iko hatarini na kuna haja ya kufanyiwa matengenezo ili watu waweze kuishi vizuri.

Mhe. Spika, kuna mtindo hizi gari ambazo hazina *plate number* wala hawana khofu hawachagui usiku wala mchana, wanatembea wakati wowote bila ya khofu yoyote kama gari iliyokuwa na kila kitu kuna nini wanatembea kuzimu kweupe? Mhe. Spika, jambo hili nalo kuna haja ya kutizamwa kwa undani wake.

Mhe. Spika, kuna suala la Deni la *ZAT* milioni 400 ambazo kulipa hawataki wala hawana nia kufunga mkataba mpya hawataki wala hawana nia. Inawezekana kuna watu wamejificha ndani yake hawataki wajulikane na ndio maana wanamuacha anafanya anavyotaka. Mhe. Spika, iko siku uwanja ule utakwama kufanya kazi. Hasa ile kutangaza kuwa ni *International Airport* sijui itakuwaje. Mhe. Spika, leo sisi Uwanja wa Ndege hauna kipaza sauti anakuja mtangazaji kama yuko kwenye daladala wanaokwenda Pemba kwa *ZAN* Air halafu hiyo ndio *International Airport*.

Mhe. Spika, sijui nyie ndio watembezi ndio mnavyoona hivyo? Mie sijui baada ya Chokochoko. Lakini nyie mnakwenda kila pembe ya dunia hivi ndivyo mnavyoona kuwa kiwanja cha ndege cha kimataifa watu wakiondoka wanapigiwa kofi . Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*).

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia nafasi hii ya kuzungumza machache kuhusiana na hoja ilioko mbele yetu.

Leo tuna taarifa ya hii Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi pamoja na utekelezaji wa maagizo waliyopewa kamati ambao waziri ametusomea hapa.

Wakati Mheshimiwa anawasilisha taarifa yake kwetu alizungumzia suala zima la kiwanja cha Mhe. Kamal Basha Pandu kilichopo hapo Darajani. Mimi nadhani Mhe. Spika, kiwanja kile si ajenda tena, kwa sababu katika Mabaraza yaliyopita tulimuomba waziri kwa sababu yule bwana ametumikia sana vyombo mbalimbali basi kile kiwanja aachiwe afanye shughuli zake. Kwa kweli Mhe. Waziri alitamka rasmi kuwa kamuachia isipokua asijenge sheli, lakini anaweza akajenga mambo mengine pale.

Kwa hivyo, nadhani katika hili kama tutakuwa na kumbukumbu nzuri Barazani suala la kile kiwanja limemaliza. Kwa sababu hata mimi niliwahi kuchangia katika lile. Kwa hivyo, nadhani mimi nimsifu Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban kwa kuweza kusimamia vizuri majukumu yake na hatimaye

kumrudishia kile kiwanja Mhe. Kamal Basha Pandu ambaye anakiendeleza sasa hivi kwa taarifa nilizonazo.

Wakati alipokuwa anawasilisha Mhe. Mwenyekiti pale yeye alitumia fursa ile ya kuwasilisha mada yake pale kumpongeza Mheshimiwa huyu Mgombea wa Chama cha Mapinduzi katika uchaguzi wa jana. Mimi Mhe. Spika, katika hili sitaki nimpongeze mgombea yeyote wala sitaki nimpe pole mgombea yeyote. Ilikuwa naiomba tu serikali katika hili kwa kushirikiana na Chama cha Mapinduzi itusaidie wananchi wa Zanzibar.

Itusaidie serikali hii moja katika kufanya mambo mawili ili sisi wananchi tuwe salama katika nchi. Wala isione haya kufanya kwa sababu haya mambo yako ulimwenguni. Mhe. Spika, ningeomba serikali itutangazie Usultani katika nchi, itakapotangaza usultani katika nchi. Mimi nitakuwa kazi yangu ni kutunga mashairi ya kumsifu Mfalme ndio kazi nitakayofanya.

Mhe. Spika, na kumpigia matarumbeta mfalme wakati wa usiku tutafanya hivyo Mhe. Spika, na tutaitii na tutakuwa chini ya twaa ya Mfalme. Jambo moja naiomba serikali ni hili.
Lakini kwa kuja kuendeleza na chaguzi...

UTARATIBU

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kutokana na kanuni ya 59. 3 kwamba Mjumbe yeyote anapokuwa akisema Barazani atawajibika kuna sababu za msingi kwa maelezo anayoyatoa ni sahihi na si mambo ya kubuni au ya kubahatisha tu. Na Spika, anaweza kumtaka Mjumbe huyu anayesema atoe uthibitisho wa usemi wake.

Mhe. Spika, kwa kuwa nchi yetu iliondoa rasmi Usultani kwa msingi huo huo kwa kufanya Mapinduzi mwaka 1964 na ndio maana tukawa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa msingi huo Mhe. Spika, serikali hii haiwezi kutangaza usultani, hili jambo haliwezi kutokea na wala halitofanyika. Kwa maana hiyo nilikuwa namuomba tu Mheshimiwa aseme mambo mengine baada ya kuzungumzia suala hili. (*Makofi*).

Mhe.Spika: Nafikiri maelekezo yako sahihi rudi kwenye hoja tuendelee na michango.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mimi niko katika kujenga hoja Mhe. Spika, na hii ni kwa ajili ya maslahi ya Wazanzibari na wananchi wetu kwa ujumla. Sasa katika kujenga hoja sijafika tamati Mhe. Spika, napigwa utaratibu. Mimi nilikuwa nataka kumaliza hoja yangu halafu ndio nipigwe utaratibu.

Mimi nadhani katika hili uniachie nimalize hoja yangu. Mhe. Spika, mimi nilikuwa nasema...

Mhe. Spika: Nikuachie vipi maana sijakufahamu nikuachie vipi?

Mhe. Saleh Nassor Juma: Nimalize hii kwa sababu Mhe. Waziri kanikatisha.

Mhe. Spika: Achana nalo hilo endelea na hoja hii ilioko.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Kwa sababu Mheshimiwa tuko jirani pale nitamuomba tukitoka hapa Barazani asimamishe gari yake pale ili niweze kumueleza zaidi katika hili.

Mhe. Spika, nadhani sasa niende moja kwa moja kwenye hoja kama ulivyonitaka. Mhe. Spika. Zanzibar ni visiwa na kwa sababu ni visiwa ina milango miwili ya kuingilia na kutokea. Zanzibar mlango wa kuingilia wa kwanza ni kupitia bandari na wa pili ni kupitia katika Viwanja vya Ndege.

Mhe. Spika, wanaosimamia Bandari na wanaosimamia Viwanja vya Ndege hawa ni Mabawabu Wakuu katika kuingia na kutoka Zanzibar. Watu au taasisi wanaosimamia milango hii ya kuingilia na kutoka walitakiwa wawe makini sio tu kufanya mambo yenu kuwa makini katika kuwasafirisha abiria, lakini hata kupunguza usumbufu wa abiria.

Mhe. Spika, la kusikitisha sana nikiangalia katika suala zima la usafiri wa baharini kuna tatizo kubwa sana. Kuna tatizo ambalo lina muda mrefu sasa. Mhe. Spika, katika usafiri ambao ni *affordable* kwa wananchi ni usafiri wa baharini, huu ni mwepesi na rahisi. Kila mtu anamudu katika nchi hii kusafiria vyombo vya bahari. Lakini la kusikitisha Mhe. Spika, umakini katika suala zima la kusimamia usafiri wa baharini umekuwa mdogo sana, wananchi wanapata usumbufu mkubwa wakiwemo ndani ya vyombo na hata pale wanapoteremka vyombo hivyo. Mhe. Spika, kama kuna sehemu ambayo Serikali inatakiwa iwe makini basi ni katika sehemu za bandari na viwanja vya ndege.

Mhe. Spika, juzi hapa ilitokea ajali ya boti, taarifa ya boti ile kupata ajali ilipatikana baada ya Kapteni kufuga gati Malindi pale. Sasa inasikitisha sana kwamba Mamlaka ya Usafiri Baharini haina uwezo wa kufuatilia hata nyendo za vyombo vya nchi hii, wakati wafanyabiashara wa kawaida tu wa usafiri wanafuatilia vyombo vyao. Hivi sasa kama tuseme utakwenda pale *Azam Marine* katika *head office* yao Dar es Salaam anaweza akajua kwamba sasa hivi meli gani iko pahala fulani na ina abiria wangapi. Lakini sasa hivi

ukiangalia usafiri wa baharini wa mamlaka hii hawana hata ofisi, ni tatizo kubwa sana.

Sasa mimi nilikuwa naomba kwamba Serikali katika hili basi wajitahidi kuiwezesha hii mamlaka kuweza kufanya kazi, kinyume na hivyo watakuwa hawana uwezo kwa sababu katika kazi zao ni pamoja na kufuatilia masuala ya ajali baharini pamoja na uokozi. Sasa ikiwa wewe huna ofisi achilia mbali boti au helikopta ya kufuatilia ajali baharini utafanya kazi kiasi gani. Mimi nadhani katika hili mamlaka iko haja ya kupewa uwezo huo. Kama tatizo ni bajeti mimi nadhani sasa imeshafika wakati bajeti yao kupanuliwa, ili waweze kufanya kazi vizuri. Kwa sababu ajali za baharini zinatokezea mara kwa mara.

Mhe. Spika, sasa niende katika suala zima la usafiri wa anga. Inasikitisha sana katika Mamlaka yetu ya Viwanja vya Ndege sasa hivi wanashindwa sana kuweka *balance* baina ya pande hizi mbili. Zanzibar imefanywa na visiwa viwili, na Wazanzibari wa pande zote mbili wanalipa kodi sawasawa. Inasikitisha kwamba juzi tumepitisha mswada hapa wa kuzilinda karafuu. Sasa ninachokwambia Mhe. Spika, watu wanaanguka mikarafuu sana Pemba kule, na siku nyengine huanguka jioni karibu na magharibi wanataka matibabu hawapati kwa sababu Uwanja wa Ndege wa Pemba hauna taa. Hichi ni kilio cha siku nyingi na kila siku kunaelezwa kwamba taa zitawekwa. Napata tatizo sasa Mhe. Spika, anieleze Waziri ule mpango wa kuweka taa umefikia wapi? Kwa sababu watu wa Pemba nao wanataka wa-*enjoy* usafiri wa usiku. Kuna usafiri wa kawaida, kuna wagonjwa. Mimi mwaka juzi nilikuwa na Mwenyekiti wangu pale ilikuwa tabu kuondoka ndege usiku. Sasa huku mikarafuu watu wanaanguka tuwapeleke vipi hospitali.

Mhe. Spika, napata wasiwasi kwamba hata ile ahadi tuliyoambiwa hapa na Waziri wa Fedha kwamba kuna meli inatengenezwa basi nina wasiwasi kuwa itakuwa kama hivi viwanja vya ndege. Uwanja wa Ndege wa Pemba hatujui utapata lini suala zima la taa ili ziweze kufanya kazi usiku. Sasa nilikuwa nataka niseme tu Mhe. Waziri anieleze ni lini Uwanja wa Ndege wa Pemba utawekwa taa kwa mara nyengine tena aweke ahadi hapa.

Mhe. Spika, suala hili hili la usafiri wa baharini kuna tatizo kwamba tunapata usumbufu mkubwa sana, huku umeshapata usumbufu wa upepo kwenye bahari, umeshapata usumbufu wa kuhangaishwa na vyombo, halafu unateremka pale. Sasa hii ni kwa Serikali nzima sio Wizara tu ya Miundombinu na Mawasiliano. Watu inabidi wanalazimika kutoka Malindi hadi Maisara sasa hili ni tatizo. Mimi sijawahi kuona usumbufu nina uzoefu wa kusafiri.

Mhe. Spika, juzi niliteremka katika mji mmoja wanaita *Changsha* pale China, ni katika *Hunan Province.* Pale kuna ile *Central Railway Station* ambayo ndio *entrance* moja ya kuingia pale *Changsha* katika *province* ile, pembezoni kuna *taxi stand*, huku kuna *public transport stand*. Hapo hapo tu ukiteremka basi unakwenda aidha kwenye *taxi* au unakwenda kuchukua usafiri wa *public.* Sasa sisi utaratibu huu tumeugundua wapi, wa kwamba mtu ateremke kwenye boti pale kishasagwa na bahari, halafu aende kwa miguu moja kwa moja mpaka Maisara huku akiwa na pakacha la ndizi, watoto wanne kawashikilia, begi. Huu ni uonevu.

Mimi nadhani Mhe. Spika hili, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano pengine hana uwezo wa kulitatua peke yake, lakini kwa sababu leo Balozi Mhe. Makamu wa Pili wa Rais yupo hapa aone jinsi Wazanzibari tunavyodhalilika. Nchi zote zinathamini raia wake na wageni. Sisi tukienda katika nchi za watu tukitoka tu pale *arrival lounge* unaingia kwenye gari. Leo hii ukiteremka kwenye *arrival lounge* upandishe kilima kule ndio upate *taxi* kwa wanaosafiri kwa ndege, au ukiteremka kwenye boti uende karibu kilomita moja, hili ni tatizo. Kuna kunyanyasa walipakodi wa nchi hii.

Mhe. Spika, mimi nadhani katika hali nitoe ushauri kwa Serikali kwamba badala ya kuwapeleka watu Maisara, hebu tuondoeni haya makontena hapa karibu na Bwawani na tufukie pale, ili watu wakitoka Malindi waje pale wapande daladala tuondoshe usumbufu huo.

Mhe. Spika, niende katika usafiri wa barabarani. Mhe. Spika, kwanza niipongeze awamu ya sita kwa kuweza kujenga mabarabara mengi tu, kuweka *network* nzuri ya barabara, ile awamu iliyokuwa inaongozwa na Mhe. Rais Mstaafu Amani Abeid Karume. Wamefanya kazi kubwa ya kujenga miundombinu ya barabara. Lakini Mhe. Spika, miundombinu hii sasa inaanza kusinyaa. Wanapokuja makampuni kujenga wanapozi-*over tonne* zile barabara zimeanza kuharibika. Sasa mimi nadhani Mhe. Waziri katika hili utakapoingia *contract* na makampuni ya ujenzi wa barabara basi muweke asilimia fulani ya *renovation* ya *infrastructures*. Na vile vile mtoe asilimia 10 ya mazingira, kwa sababu kunakuwa na *environmental degradation*. Upeleke asilimia 10 ya *total project* Idara ya Mazingira ili waweze kufukia mashimo kwa kina Mhe. Subeit Khamis Faki, Makaani kule, Vitongoji, Mwambe, wafanye hivyo.

La mwisho kabisa Mhe. Spika, nadhani nimalizie kwa kuitaka Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwamba maendeleo ya nchi isiwe kafara kwa walipakodi wa nchi hii. Ikiwa hamna uwezo wa kujenga barabara basi mpaka upate uwezo. Yaani mimi nilikuwa na wavuvi wakaacha uvuvi kwa sababu fukwe zimechukuliwa na matajiri wakaja zao kuwekeza kwenye kilimo

Vitongoji pale wakapanda miembe. Leo huyu Mhe. Waziri kaenda kutoa amri waikate miembe ile upelekwe umeme Makaani kule. Huu ni mwaka wa pili hawajalipwa wale fidia zao. Sasa mimi namwambia Mhe. Waziri alisema kwamba watu wale watalipwa baada ya kuikodisha ile mashine. Hii mashine imeshakodishwa mwaka wa pili kwa nini hawajalipwa watu wale wa Vitongoji?

Sasa katika hili mimi nadhani Mhe. Spika, tunaandaa maandamano kuelekea kwenye Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kulipwa fedha zetu. Sasa katika hili hatukubali na naenda Vitongoji tukijaaliwa na nitakutaarifu. Uwepo Makamu wa Pili wa Rais kuona kwamba wakulima wa Vitongoji waliokatiwa miti yao kwa ajili ya kupeleka umeme Makaani tunalipwa kwa kupitia maandamano. Kwa sababu tumeshasema sana kwenye Baraza hatusikilizwi, tumeshamwambia sana Mhe. Waziri hawatusikilizi, sasa tunataka kwenda kwa Makamu wa Pili kwa maandamano. Mhe. Spika, naunga mkono hoja.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataala kwa kutujaalia uhai na uzima tukaendelea na shughuli zetu. Pili Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa fursa na mimi kuchangia mjadala wa ripoti hizi mbili za utekelezaji za Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano pamoja na Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ambayo mimi ni Mjumbe wake.

Tatu Mhe. Spika, niwashukuru wote ambao wamewasilisha ripoti hizo hapa mbele ya Baraza hili.

Mhe. Spika, mimi naomba nianze kwanza kuhusiana na suala ambalo lipo katika ukurasa wa 124 katika Ripoti za Kamati linalohusu kiwanja kinachoambiwa cha Mhe. Kamal Basha Pandu. Nalizungumzia hili Mhe. Spika, kwa sababu limo ndani ya Jimbo langu na ni mmoja katika watu ambao wamefuatwa na wananchi sana hasa wa eneo lile kueleza kukirihishwa kwao kwamba eneo la wazi katika maeneo machache yaliyobakia katika Mji Mkongwe sasa nalo tunaligeuza kuwa ni eneo la ujenzi.

Mhe. Spika, suala hili kama lilivyozungumzwa na Ripoti ya Kamati lilikuja Barazani, lakini namna lilivyokuja ilikuwa vigumu sana kwa mtu hasa sisi wengine hatujazoea kuchangia mambo ambayo hatujayaelewa undani wake. Nilikuwa nikijiuliza hapa nikawauliza baadhi ya Wajumbe wenzangu, hichi kiwanja tunachokizungumza ni kiwanja kipi kwa pale? Nimekuja kukijua baada ya kuwekwa bango nikashtuka Mhe. Spika. Kwa sababu lile ni miongoni mwa maeneo yaliyokuwa yamewekwa wazi.

Mhe. Spika, Mji Mkongwe wa Zanzibar umetangazwa kuwa ni eneo la Hifadhi ya Urithi wa Kimataifa chini ya *UNESCO*. Na katika mradi ule kulitanguliwa na ripoti ambayo ilifanywa na Taasisi ya Agakhan na ina ramani ambayo mimi ninayo nakala yake inayoonesha maeneo yepi ya wazi ambayo yanapaswa kuhifadhiwa. Moja wapo lilikuwa ni eneo lile ambalo tumezoea kuliita ni Uwanja wa Malindi.

Sasa bahati mbaya sana na ndio kila wakati unatutahadharisha Mhe. Spika, tukifika chombo hiki kuingilia mambo ya utendaji tunaweza tukasababisha mvutano kama ulivyokuwa umejitokeza sasa hivi. Tumepelekea kwamba kutolewa idhini ya kujengwa pahala ambapo hata kwa macho ya kawaida tu panakuonesha kuwa hapa hapakuwa na pahala pa kujengwa.

Mhe. Spika, pale pana *transformer* ya umeme. Na kuthibitisha kwamba hichi kiwanja ni mambo ya ajabu ajabu tu. Kilipopimwa kwanza mabati yalipozungushwa yalichukua mpaka eneo lenye *transformer*. Wameshaanza kuchimba wakakumbana na waya mzito wa umeme kimerejeshwa nyuma kiwanja. Sasa Mhe. Spika, ramani gani hizo za mji ambazo unataka kujenga unachimba kwanza unarudi nyuma. Sasa mimi nasema sote tunamuonea huruma Mhe. Kamal Basha Pandu, lakini ndio maana tukapendekeza kwamba atafutiwe pahala pengine, kama kutafuta rizki hawezi kukosa pahala pa kutafuta rizki katika nchi hii. Tumependekeza kwamba Wizara itafute utaratibu wa kupata eneo jengine mbadala lakini pale Mhe. Spika, tutapeleka ujumbe mbaya sana, si kwa wananchi wetu tu, lakini hata kwa taasisi za kimataifa.

Mhe. Spika, hivi sasa ukipita pale pahala hapajajengwa mandhari tayari imechafuka. Lakini huku kuna ujenzi na huku kumetolewa kiwanja unabakisha uchochoro unawaambia ndio njia ya kuelekea kwenye makaazi ya watu katika eneo lile. Mhe. Spika, si utaratibu mzuri wananchi wa eneo lile hawakuridhika na waliandika barua kwa Mamlaka ya Mji Mkongwe kuonesha malalamiko yao wakati lilipotoka tangazo la mwanzo, lakini bahati mbaya malalamiko yale ya wananchi yamepuuzwa na mamlaka zinazohusika. Namtaka Mhe. Waziri atusaidie kwamba kwa nini tuendelee kukubali ujenzi ule?

Na Mhe. Spika, bahati mbaya tulipoufuata utendaji wa Mamlaka ya Mji Mkongwe tukaomba kuona nakala ya hati ya mwanzo ya kilipotolewa kiwanja kile. Mhe. Spika, si utaratibu mzuri, kiwanja kile kajipa mwenyewe Mhe. Kamal Basha Pandu alipokuwa Waziri, na hati ile tumepewa nakala sisi ina saini yake.

Sasa Mhe. Spika, leo tukisema Baraza hili libariki vitu kama vile ni hatari, kwamba kwa sababu tu mtu alikuwa katutumikia kwa hivyo huyu tumruhusu kuvunja utaratibu. Mhe. Spika, si utaratibu sahihi hata kidogo. Na utaratibu wa mtu kuwa kakaa katika nafasi ya madaraka akajitizama nafsi yake kwanza ni kinyume hata na Katiba ya Zanzibar inayokataza kutumia cheo cha mtu kwa kujinufaisha kibinafsi. Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi nasema wazi kwa niaba yangu, na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe na hasa eneo lile kwamba pale nasema Serikali ifikirie utaratibu wa kumtafutia eneo mbadala impe, lakini pale paendelee kuheshimiwa ili Mji Mkongwe uendelee kunusurika kama ni urithi wa kimataifa.

Mhe. Spika, kwa taarifa yako, ninazo taarifa kwamba tayari kuna nchi moja miongoni mwa wanachama wa *UNESCO* imeshatoa taarifa ya kutaka kupeleka hoja kwamba Zanzibar itangazwe kwamba ni eneo hatarishi na linaanza kupoteza sifa ya kuwa eneo la urithi wa kimataifa, na hiyo ni hatua ya mwanzo ikikubalika itakuja kufuatiwa na hatua ya kuuondoa Mji Mkongwe wa Zanzibar katika urithi wa kimataifa. Mhe. Spika, hili naomba sana, na nadhani liwe fundisho kwetu kwamba mara nyengine tusitumie Baraza kushirikisha baadhi ya mambo ambayo yanaweza kuleta athari kubwa kwa nchi yetu.

Mhe. Spika, la pili nataka kulizungumzia ni suala la ujenzi wa jengo jipya la abiria kwa maana ya *terminal*, lakini nitalichanganya kwa sababu ya uchache wa muda na suala zima la kuipata kampuni kwa ajili ya kutoa huduma za Uwanja wa Ndege kwa maana ya *ground handling.*

Mhe. Spika, masuala haya mawili yalichukua mjadala mkubwa sana katika Baraza hili kwa miaka mingi. Mimi nakumbuka tangu nimeingia ndani ya Baraza hili tunalijadili suala hili mpaka hii leo. Na kuthibitisha kwamba wasiwasi ambao tuliutoa Mhe. Spika, ulikuwa ni wa msingi ndio maana mpaka leo miradi hii inakwamakwama. Serikali inatoa maamuzi lakini yenyewe inahisi kwamba kuna uzito. Moja limeonekana wazi katika ujenzi wa *Terminal II.* Kwa macho tu sasa hivi ukiteremka pale unaona kwamba baada ya kujengwa lile eneo la *apron* na *taxi way*, basi lile jengo ambalo *frame* yake imeshawekwa pale ya ujenzi wa *terminal* mpya liko chini. Huo si utaratibu mzuri wa ujenzi.

Lakini zaidi wataalamu kila anayekwenda pale anathibitisha kwamba jengo lile tutang'ang'ania kulijenga leo, lakini hasara yake itakuja kubebwa na wananchi wa Zanzibar huko mbele tunakokwenda. Lakini zaidi Mhe. Spika, imeonekana kwamba hata hizo gharama tulizokuwa tukizikimbia za dola milioni 10 kwamba tukiamua kusema livunjwe lirejeshwe nyuma kutaingia hasara ya gharama za ziada ya dola milioni 10. Tunaambiwa katika kipindi

hichi tu tayari ile kampuni ambayo ilikuwa ikifanya kazi ya ushauri elekezi pale mwanzo imedai kulipwa dola milioni 3 kama fidia. Mbali ya gharama ambazo tutaziingia kwa matumizi makubwa ya umeme kutokana na ujenzi wa jengo lilivyojengwa sasa hivi, na vile vile ufinyu wa nafasi ambao utakosesha maeneo ya kufanya biashara na kukosesha mapato ya mamlaka. Kwa hivyo wataalamu wote wanathibitisha kwamba hiyo gharama inayokimbiwa na Serikali ya dola milioni 10 inaweza ikarejeshwa ndani ya miaka mitano ikiwa tutafanya marekebisho ya uwanja. Kwa hivyo sifahamu kwa nini Serikali inang'ang'ania biashara ile.

Mhe. Spika, zaidi ni hili suala la *ground handling services* au Kampuni ya Kutoa Huduma za Uwanja. Wamesema wenzetu hapa na ripoti ya Kamati yetu imesema Mhe. Spika, kwamba pana tatizo kwa sababu kampuni iliyopo sasa hivi haina mshindani. Kulitangazwa zabuni tukaijadili Mhe. Spika, hapa ndani, hatimaye Serikali ikaamua kusitisha zabuni ile na badala yake kwa maelezo yaliyokuwa yametolewa kwa urefu ndani ya Baraza hili na Serikali, tukaambiwa kwamba Serikali imeamua kumualika mwekezaji mmoja ambaye atawekeza katika suala hili na masuala mengine kwa ajili ya kuipa huduma nchi yetu. Lakini Mhe. Spika, tangu uamuzi ule ulipotangazwa ndani ya Baraza hili mwezi wa Julai mwaka jana, mpaka leo mwezi wa Februari ni miezi minane. Tunafuatilia kama Kamati yetu hakuna chochote ambacho kimefanyika hadi leo. Tunajiuliza kama mwekezaji huyu alikuwa tayari kama ambavyo Baraza hili lilikuwa limearifiwa, kwa nini mpaka leo hakuna kitu kimefanyika? Tunaomba maelezo kutoka kwa Serikali juu ya suala hili. Kuna nini hapa Mhe. Spika?

Mhe. Spika, nikiacha hapo naikumbusha Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, nilisema mwaka juzi, mwaka jana nikanyamaza, nawaambia wajiandae katika bajeti ya mwaka huu. Kuna milioni 40 za Jimbo la Mji Mkongwe zimetafunwa na Wizara. Kwa sababu gani. Mhe. Spika, hizi ni fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo za Mbunge. Hapa kwanza tulipozitaja Wizara ilisema kwamba haikuwa na vielelezo, baadaye wenyewe wakanithibitishia kwamba fedha zimeingia katika mfuko wa Wizara kutoka katika Baraza la Manispaa linalosimamia. Lakini mpaka leo Mhe. Spika, hakuna kilichofanyika zaidi ya kipande kile cha Mkunazini pale, kinyume na makubaliano ambayo barua yake tunayo iliyoandikwa na aliyekuwa Waziri wa Mawasiliano wakati ule, kinyume na ahadi zinazotolewa kila siku ndani ya Kamati kwamba litafanyiwa kazi. Mpaka leo barabara za Mji Mkongwe zimeachwa hazijafanyiwa kazi yoyote, pamoja na kwamba kumepelekwa mchango wa milioni 40. Mhe. Spika, nataka maelezo katika hili. Niwaambie kabisa hapa ni Kamati hakuna vifungu lakini bajeti inakuja tukijaaliwa. Katika hili Mhe. Spika, tumeshastahamili vya kutosha hatuwezi kuvumilia tena.

Mhe. Spika, jengine ambalo mimi naomba maelezo ni suala hili la deni la umeme la *TANESCO*. *TANESCO* wanasema bilioni 70, *ZECO* wanasema bilioni 44. Lakini mbali na maelezo hayo ya Serikali itwambie ni lipi hasa deni sahihi? Naomba pia atusaidie. Kwa taarifa tulizonazo sisi Mhe. Spika, umeme ule ulipokuwa unaletwa Zanzibar, Zanzibar ilitoa mchango uliotokana na msaada ambao Zanzibar ilipatiwa miaka ile ya 70 na 80. Na *line* yote ya umeme kutoka Ubungo mpaka Ras Kiromoni ambapo ndio ilipotoka kuletwa Zanzibar, inasemekana ni mwekezaji wa Zanzibar, na ni moja katika *line* ambazo zinaingiza mapato makubwa kwa *TANESCO* katika maeneo makubwa ya kibiashara na makaazi ya watu. Sasa tuambiwe Zanzibar je, inapata nini katika uwekezaji ule ambao ulifanya. Kwa sababu umeme ule hauji Zanzibar tu, unapita katika maeneo makubwa ya kibiashara unaingiza mapato kwa *TANESCO*, tuambiwe nini fungu la Zanzibar.

Mhe. Spika, namuomba vile vile Mhe. Waziri kuna suala moja anisaidie, kuna wananchi wa Matemwe wameleta malalamiko yao kwetu. Wanasema kwamba kuna nyumba na mazao yao yaliathirika kutokana na mradi wa ZAWA kupitisha miundombinu ya maji na wakaambiwa watalipwa fidia, lakini mpaka leo hawakulipwa fidia. Wamefuatilia kwa Sheha, wamefuatilia kwa Mkuu wa Mkoa, na wanavyosema wamefika mpaka kwa Waziri kufuatilia fedha za fidia zao ambazo waliambiwa tayari zilikuwa zimeshatolewa, lakini mpaka leo hawakulipwa. Ningemuomba Mhe. Waziri akija na hili aje anisaidie.

Sasa Mhe. Spika, nikiondoka hapo katika ripoti za utekelezaji za Mawaziri. Mhe. Spika, mimi kidogo napata wasiwasi kwamba kwa majibu ya aina hii maagizo na maoni ya Kamati yatakuwa yanaendelea kujirejea yale yale kila mwaka. Kwa sababu maelezo mengi tunayoyapata Mhe. Spika, hayatoshelezi. Ni bahati mbaya kwa sababu ya muda sitaweza kujieleza kwa kina, lakini nitatoa maelezo kwa ufupi nifahamike.

Nianze na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Mhe. Spika, ukurasa wa saba agizo nambari 15 inasema "Kamati inashauri kuangalia Bodi za Wataalamu na Bodi ya Wakandarasi kwa kuzitengea fungu lake la bajeti, ili bodi hizo ziweze kufanya kazi zake vizuri. Majibu ni kwamba Wizara inaendelea na jitihada za kuomba fedha kwa ajili ya bodi zake hizi mbili ili ziweze kutekeleza vyema majukumu yake.

Mhe. Spika, Wizara inaendelea kuomba fedha. Sisi Kamati hii inaendelea kukutana na bodi hizi bado inalalamikia kwamba fedha. Kwa hiyo maana yake ni kwamba mwaka mzima uliopita hakuna kitu katika suala hili.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa nane agizo nambari 17 kuhusu Bustani ya Forodhani inahusu Mamlaka ya Mji Mkongwe. Tumekuwa tukilizungumza mara nyingi tunaambiwa hatua zitachukuliwa za kupeleka maji Bustani ya Forodhani lakini mpaka leo halijatekelezwa.

Mhe. Spika, agizo jengine nambari 22 hili linahusu usafi katika Mji Mkongwe. Pamoja na kwamba linaendelea kuripotiwa katika ripoti ya kila mwaka bado suala lipo katika hali mbaya sana. Mhe. Spika, juzi ilibidi nipige picha katika baadhi ya maeneo. Pale tulikuwa tunamuuliza Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ akasema kwamba wanajitahidi na hali imeimarika. Nikampigia picha katika simu nataka nije nimuoneshe jinsi majaa yanavyofurika bila taka kukusanywa. Hivi sasa ningemuomba mimi Waziri apite katika maeneo mbali mbali ya Jimbo la Mji Mkongwe, Michenzani akatazame taka zilivyofurika katika yale matangi yaliyowekwa pale kutupia taka mpaka hazikusanywi.

Mhe. Spika, jengine ni agizo nambari 24 linalohusu kupeleka maji katika maeneo ya Mji Mkongwe na katika Bustani ya Forodhani vile vile hakuna ambacho kimefanyika pamoja na maelezo hayo yaliyokuwa yameripotiwa na Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, agizo nambari 27 kuhusu gari la kufyonzea maji kwa majumba ya maendeleo kwa upande wa Pemba. Tumeambiwa gari hili lipo Baraza la Manispaa kupitia mradi wa *ZUSP*. Sina hakika kama Waziri kaelewa, maana Baraza la Manispaa ninavyofahamu katika Zanzibar ni moja tu la Mji wa Zanzibar, Pemba sifahamu kama kuna Baraza la Manispaa. Mhe. Spika, Mhe. Waziri atueleze katika hili kumetekelezwa nini.

Mhe. Spika, la mwisho katika Wizara hii kwa ajili ya muda naomba nizungumzie agizo nambari 34 linahusu Shirika la Umeme. Hili linahusu Taasisi za Serikali kulipa madeni yake. Hapa Mhe. Waziri katwambia Wizara imelitekeleza na mafanikio yameanza kuonekana kwa baadhi ya Taasisi na Wizara hizo kuanza kufanya marejesho ya madeni. Mimi nadhani Mhe. Spika, kwa chombo kama hiki majibu haya hayatoshelezi. Alikuwa atwambie taasisi zipi zimelipa na zipi bado zinadaiwa, zimelipwa kiasi gani, deni lililobakia kiasi gani. Nadhani ndio utaratibu mzuri wa kuripoti kwa chombo kama hiki. Laa kama sivyo Mhe. Spika, itakuwa maelezo haya ya jumla jumla yanapelekea kila siku Kamati hairidhiki yanarejea mambo yale yale kila mwaka.

Mhe. Spika, kwa dakika zilizobakia naomba nimalizie na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano nayo vile vile niseme. Kwanza katika ukurasa wa 7 mpaka wa 8 kuna suala la madeni ambayo Shirika la Bandari linadai. Na

hapa tumeripotiwa kwamba kumeundwa Tume Maalumu chini ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Nafikiri Mhe. Spika, ukiondoa maneno haya ya jumla jumla tungeambiwa tumefikia wapi. Kwa sababu haya maelezo ni ya jumla tu kwamba kumeundwa chombo, hatujaambiwa kwamba hilo suala limetatuka kiasi gani.

Vile vile Mhe. Spika, katika ukurasa wa 15 katika ripoti hii ya utekelezaji wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kuna suala la kutengeneza kanuni kwa ajili ya mamlaka ya usafiri baharini. Kuna maelezo juu ya hatua nyingi zinazofuatwa lakini mpaka sasa hivi hatujaelezwa kanuni ngapi zimekamilika na kutangazwa. Ningeomba maelezo katika hili.

Mhe. Spika, jengine ni ukurasa wa 17 nalo linahusu ulanguzi wa tiketi. Mhe. Spika, tumeliona mpaka juzi katika ajali iliyotokezea katika boti ya Kilimanjaro kwamba watu wengi wamepotea haikuweza kufahamika mara moja ni akina nani kwa sababu inaonekana bado kuna tiketi zinauzwa bila ya kufuata utaratibu wa kutoa vitambulisho. Nilikuwa naomba tuelezwe kwamba na hili pia limefikia wapi.

Mhe. Spika, agizo jengine lipo katika ukurasa wa 19 linalohusu Serikali kupitia Wizara kuipatia Mamlaka ya Uwanja wa Ndege fedha kwa ajili ya kununua vifaa mbali mbali zikiwemo mashine za *x-rays* limeendelea kuripoti tena katika ripoti ya mwaka huu ya Kamati yetu kwa sababu halikutekelezwa.

Mhe. Spika, jengine ni ukurasa wa 20 kuhusu suala la *airport service charges*. Hili Mhe. Spika, naomba Waziri akija atusaidie hasa. Kwa sababu Serikali inasema kwamba haiwezi kuruhusu *airport service charges* katika mamlaka. Lakini sheria tuliyopitisha ndani ya Baraza hili ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kifungu namba 19 (1) (b) inalisema wazi kwamba moja wa vyanzo vya mapato vya mamlaka ni *airport service charges*. Kwa nini Serikali inavunja sheria kwa kutoipa mamlaka ambayo yametajwa ndani ya sheria iliyotuletea katika Baraza hili.

La mwisho kabisa Mhe. Spika, sikuridhika hata kidogo na majibu yaliyokuwa katika ukurasa wa 27 wa majibu ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kwa mambo mawili. Moja, pana ripoti zinazohusu Mamlaka za Muungano, na pili zinazohusu Zantel. Hapa katuripotia tu kwamba kishafikisha, anaamini kwamba yatatekelezwa.

Mimi nadhani Mhe. Spika, hiyo haitoshelezi, yeye ndiye msimamizi wa sekta hizi alipaswa kama haya mengine atuchukulie majibu atuletee katika Baraza la Wawakilishi, kuwa majibu yale yalikuwa yamepokelewa na chombo hiki

na yakaidhinishwa. Maana yake anayewajibika kwetu hapa ni yeye, aje atwambie kwamba haya yametekelezwa kiasi gani.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naiunga mkono Ripoti ya Kamati, lakini naomba maelezo juu ya yale mambo ambayo nimeyatolea hoja mbali mbali. Mhe. Spika, nakushukuru ahsante sana.

Mhe. Spika: Mhe. Ismail Jussa Ladhu tunakushukuru. Waheshimiwa Wajumbe kwa kipindi hichi tukomee hapo na tukutane jioni ambapo kuna wachangiaji wapatao watano hivi wamalize hao ili Waheshimiwa Mawaziri watupatie majumuisho na majibu ya hoja mbali mbali. Na wakati huo Mhe. Mwenyekiti naye awe anajitayarisha na kuja kufanya majumuisho yake.

Kuna tangazo moja Waheshimiwa Wajumbe Wawakilishi wa CCM wanaombwa wabaki kwa muda kidogo, mara baada ya kuakhirisha kikao kuna mazungumzo muhimu ambayo Mhe. Mnadhim wa upande huo anataka kuzungumza na Waheshimiwa Wajumbe wa CCM.

Baada ya hayo basi Waheshimiwa Wajumbe niakhirishe kikao hichi hadi saa kumi na moja jioni leo.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa jioni hii tupo hapa katika hali ya uzima na afya njema. Pia Mhe. Spika, nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi.

Lakini pia nimpongeze kwa dhati kabisa Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa umakini wake mkubwa kuandika ripoti hii nzuri ya kuleta mafanikio katika nchi yetu na wizara mbili hizi. Lakini pia Mhe. Spika, nimpongeze ndugu yangu Mhe. Mahmoud Thabit Kombo kwa ushindi alioupata wa kishindo katika Jimbo la Kiembesamaki. (*Makofi*).

Baada ya hayo Mhe. Spika, kwanza mimi ninaunga mkono ripoti hii asilimia 100 kwa 100. Kwa upande wangu nitagusia baadhi ya sehemu za wizara hizi mbili, sehemu zenyewe ni sita ili kutoa ufafanuzi zaidi kwa ajili ya kamati yetu.

Kwanza nimpongeze sana mkurugenzi wetu wa airport Ndugu Said kwa jitihada zake kubwa sana katika kuiletea mamlaka yetu ya viwanja vya ndege

Zanzibar maendeleo makubwa. Kwa kuanzia Mhe. Spika, nianzie katika ukurasa wa 99 Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Nitaanzia uwanja wa ndege wa Zanzibar hususan nitazungumza kuhusu uchakavu wa vifaa, na vifaa vya usalama.

Mhe. Spika, kwa kweli tunavyojua *airport* yetu hasa hii ya Zanzibar wageni wetu wengi wanakuja katika nchi hii lakini kuna uchakavu au uhaba wa vifaa muhimu sana vya ku-*check* mambo mengi. Tukianzia na *X-ray machine* Mhe. Spika, imebakia moja na moja ya nje ni mbovu. Pia watendaji wetu wanashindwa hata kugundua hata madawa ya kulevya yanavyoingia. Kwa hivyo ninaomba sana wizara iangalie suala hili hasa katika *X-ray machine*. Kuna vifaa vyengine pia ambavyo hatuna pale airport kama hivi *walk through mental detectors* na *harold mental*.

Pia *CCTV* hamna mpaka hivi sasa Mhe. Spika. Naomba sana wizara iangalie suala hili ni muhimu sana hasa katika mambo ya ajabu ajabu ya madawa ya kulevya yanavyopitishwa hivi sasa kwa wingi.

Lakini Mhe. Spika, nizungumzie suala la vipaza sauti. Kwa kweli katika *airport* yetu vipaza sauti hamna na ukitazama Mhe. Spika, vipaza sauti sio gharama kubwa ya hivyo. Zinaweza kuondoka ndege tatu, nne, tano kwa wakati mmoja zile *charter* , unakuta hata utangazaji wao wa kuwaambia abiria ndege fulani inaondoka, sio nzuri, inakuwa inachanganya abiria.Kwa hivyo naomba wizara na mamlaka iangalie sana suala hili la sauti katika airport yetu ya Zanzibar.

Pia niseme mkurugenzi anajitahidi sana, lakini la kusikitisha aliomba mkopo wa kununua mabasi kwa ajili ya wafanyakazi, lakini hajapatiwa mpaka leo. Wafanyakazi wanahangaika. Kwa hivyo naomba sana Mhe.Waziri aliangalie suala hili.

Mhe.Spika, suala la *AC* kwenye *airport* yetu hivi sasa imefungwa, imekuwa feki lakini *AC.* Sehemu ya kuondokea abiria wanakuwa wengi jua kali, kwa kweli mpaka watu wanaumwa, wanapata *pressure* kwa joto kali.

Pia nizungumzie suala la watu wengine wanapokwenda kusafirisha abiria, wanafika pale *airport* wanakuta mpango uliokuwa hivi sasa, unaambiwa abiria muache nje kule usisogee naye kabisa huku. Sasa yule abiria anakuwa anaingia ndani hana hata simu saa nyengine, inakuwa ni matatizo hawezi kuwasiliana na yule mwenyeji wake aliyekuwa nje. Kwa hivyo nilikuwa ninaomba utaratibu wale wasindikizaji angalau wasongee kidogo eneo la *airport*, wawasiliane nao hao wageni wanaoondoka, ili wakipata usumbufu wowote wapate kuwasiliana na mwenyeji wao kiurahisi.

Mhe. Spika, nije suala hili la *parking*. Unapokwenda *airport* unalipishwa shilingi mia tano mlangoni, lakini unafika pale mbele usisimamishe gari wala usishuke pale. Sawa hamna kushuka, huteremshi mizigo, lakini kama mtu ana mgonjwa je, mtu mzima, kushuka pale kwa dakika moja pia inakuwa sio ruhusa!

Kwa kweli nimuombe mkurugenzi hili suala Mhe. Spika, aliangalie sana ili wananchi wasipate usumbufu kiasi hicho. Hasa kuna kijana mmoja huyu anaitwa Haji; huyu kijana ana lugha mbaya kabisa, hajui huyu mtu mzima, huyu kijana, huyu mheshimiwa, yeye anatukana watu tu, anapenda kusema kwamba nyinyi Waheshimiwa sio munatunga sheria hizi.

Mkurugenzi malengo yako ni mazuri ya kuleta maendeleo ya nchi yetu, lakini huyu kijana anayeitwa Haji ambaye yupo katika eneo la *security* anaweza kukuharibia. Naomba muangalie sana kijana huyu.

Mhe. Spika, niendelee kwenye ukurasa wa 100 katika *airport* yetu ya Pemba. Mhe. Spika, kama tunavyojua *airport* yetu ya Pemba ni ndogo na abiria wanapoondoka, mimi juzi mwenyewe nilikuwa shahidi pale nilipoingia lile jua lote linapiga pale. Sasa inakuwa usumbufu mkubwa kwa abiria. Kwa hivyo naomba sana Mhe. Spika, mkurugenzi wetu kupitia wizara kuwajengea kipaa wananchi kwa haraka kuondosha usumbufu huu wa jua, kwani kipaa hicho sio gharama kubwa kitakachoweza kuwasaidia hao abiria wetu.

Naomba sana suala hili liangaliwe kwa sababu suala hili ni la muda mrefu, Kamati iliyopita imezungumza lakini hakuna utendaji wowote na Kamati hii inazungumza.

Mhe. Spika, suala jengine la ndege ikitokea dharura. Ule uwanja ulivyo unakuta hata ile *fire* ikitaka kwenda katika eneo husika haiwezi kufika, mpaka itembee kwenye njia ile inayorukia au kutulia ndege. Nilikuwa ninawaomba mamlaka ifuatilie na wizara pamoja, itengeneze njia ili *fire* liweze kufika kwenye eneo la tukio likitokezea. Kwa sababu kuna mabonde hata lile *fire* haliwezi kufika kule. Kamati imekwenda imeangalia na imeona hali halisi ilivyo Mhe. Spika.

Vile vile Mhe. Spika, nije kwenye suala hili kubwa kabisa la taa. Tunazungumzia mara nyingi sana uwanja wa Pemba hauna taa. Mambo mengi yanaweza kutokezea zikiwemo ajali kwa sababu ya taa na ukitazama gharama ya taa hizi sio kubwa sana, ni milioni elfu mbili mia saba. Kwa kweli hatushindwi kununua taa hizi Mhe. Spika, na ahadi ya Mhe. Waziri aliyoisema katika bajeti iliyopita mwaka 2013/2014, hizi taa zitanunuliwa lakini mpaka leo bado. Mhe. Spika, hapa kuna nini?

Kwa mfano, kama juzi, siku tatu za nyuma ndege *Zanair* ilipata hitilafu, haijaanguka lakini ilishindwa kufunga breki zake, ikabidi kwenda mpaka kwentye mazao ya watu. Lakini kama kungelikuwa na taa angeona kwa mbali na angejua atue vipi. Mwenyezi Mungu katunusuru sana hajafariki mtu, na wala hajaumia mtu.

Mhe. Spika, tumeweza kununua meli kwa fedha chungu nzima na wizara zote zimekatwa fedha kwenye bajeti zao, naomba na hili tufanye hivyo hivyo, ninajua serikali yetu haina fedha nyingi lakini naomba sana tufanye kama tulivyofanya mwaka jana tupate pesa za taa kwa ajili ya uwanja wa Pemba.

Mhe. Spika, kama tunavyojua kisiwa cha Pemba hivi sasa wageni wengi wanakwenda kukitembelea. Kila siku zinavyokwenda mbele wageni wanazidi kutoka sehemu mbali mbali, wanakwenda katika kisiwa cha Pemba. Kwa hivyo naomba sana Wizara iangalie suala hili la kushughulikia la taa.

Mhe. Spika, nije kwenye suala la uzio vile vile. Ukitazama uwanja wetu wa ndege wa Pemba hauna uzio, kuna uzio upande nusu tu, na Kamati yako Mhe. Spika, imetembelea na imeona hali halisi, wanyama wanaweza wakasogea pale wakati ndege inaruka au inatua wakaingia kwenye njia ya kurukia ndege au kutua. Kwa hivyo naomba suala hili la uzio uwanja wetu wa Pemba litizamwe.

Mhe. Spika, nije kwenye ukurasa wa 94 kuhusu Shirika la Bandari Zanzibar. Mhe. Spika, kama tunavyojua Shirika la Bandari ni muhimu na kama nilivyoeleza mwanzo milango yetu ni miwili; bandari na anga. Suala hili ni muhimu sana kwa wananchi wetu kufanya biashara zao hasa katika bandari ya Zanzibar. Wanaleta bidhaa mbali mbali na kusafiri kwenda Tanzania Bara. Lakini suala hili la makontena yao wanayoweka pale Bwawani, kwanza ninawapa pongezi sana Shirika la Bandari. Kwa sababu kazi wanayoifanya ni kubwa, ukitizama kazi ile ya kupanga makontena hadi usiku.

Hata hivyo Mhe. Spika, makontena yale wanavyoyapanga ni hatari. Wanapanga mpaka makontena matano matano, maana yake moja, mbili, tatu mpaka tano. Sasa linaweza likaanguka likahatarisha maisha ya watu. Lakini pia tufikirie Mhe. Spika, hili eneo wanataka kulichukuwa kupewa mwekezaji lakini ikiwa tunawahamishia hawa bandari kule Saateni Mpigaduri, ile hatua ya kuyapeleka makontena yale kule, hizi njia zipo wapi za kupita magari makubwa kama yale.

Ninafikiri tutakuja kusababisha ajali kubwa. Kwanza kwa sasa hivi kwa muda huu naomba sana bandari ile bado kujengwa, naomba sana serikali iwaachie kulitumia eneo la Bwawani. Kwa sababu kazi yao ni kubwa na makontena

yao ni mengi na wanajitahidi sana kuyarejesha pale bandarini mpaka usiku wanafanya kazi hiyo kiurahisi. Lakini tutakuwa hata hizo ajira ambazo tunazozitegemea zitapotea sana.

Sasa niingie kwenye suala hili la gati ya Mkoani Pemba Mhe. Spika. Kwa bahati nzuri sana Kamati yako ilitembelea juzi juzi Pemba katika kazi yake, na bahati kulikuwa na mvua. Kuna siku moja wale wananchi walikuwa wanapata taabu sana kufika kule kwenye meli kupanda, kwa sababu utakuta wana watoto wadogo, mizigo na ile mvua na lile eneo halina chochote, wakati wa jua kali inakuwa hatari na wakati wa mvuahalkadhalika. Kwa hivyo wanapata taabu sana, kwa sababu mizigo yao inaroa na watoto wanaroa kwa kweli Mhe. Spika. Naomba hili tuliangalie sana tuwajengee kipaa hawa abiria wanaosafiri kupitia bandari ya Mkoani. Pia *crane* japo moja iende Pemba, ikae pale kwa sababu mizigo inakuja mikubwa wanaipakua kwa mikono yao, wanapata shida sana.

Mhe. Spika, sasa niingie katika Idara yetu ya Utunzaji wa Barabara kwenye ukurasa wa 93. Kwanza niwapongeze sana ndugu hawa wa barabara kwa kazi yao ya barabara ya Amani-Mtoni karibu inakwisha.

Kwa hivyo nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa kazi yake nzuri. Pia nimshukuru Waziri na Naibu Waziri kwa juhudi ambayo wanayoichukua katika jimbo langu la Bububu. Sasa hivi tunavyojua kazi moja inaendelea pale Kigamboni, Bububu kwa Handhari njia ya kwenda Mwanyanya, lile daraja linaendelea hivi sasa kutengenezwa.

Hivyo Mhe. Spika, lakini kuna kitu kimoja ninasikitika kidogo. Serikali yetu inajitahidi sana kuboresha miundo mbinu hii. Lakini kuna barabara moja pale Mwanyanya juzi juzi imetiwa kifusi, ni mwaka mmoja sasa hivi, imetoka Bububu mpaka jeshini na kuzunguka kote. Lakini Mhe. Spika, cha kusikitisha ile barabara sasa hivi inaanza kuharibika tena. Imeshaanza mashimo tena na baada ya muda mfupi itakuwa haipitiki. Sasa naomba Mhe. Waziri aangalie kuitia lami ile barabara kabla haijaharibika kabisa.

Mhe. Spika, sasa niingie kwenye Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kazi yake nzuri na anajitahidi sana kwenye shughuli zake zote za wizara hii. Kwani wizara hii ina mambo mengi na ina majukumu mazito inayogusa jamii.

Katika ukurasa wa 94 wa ripoti yetu ya kamati. Kwanza nipongeze sana Shirika la Umeme, Meneja na wafanyakazi wake kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa kujitahidi miundombinu isiharibike. Lakini Mhe. Spika, kitu cha kusikitisha wananchi wanapokuwa wanadaiwa pesa kidogo tu, hata

shilingi laki moja unakutiwa umeme. Naomba waangaliwe wananchi wetu wengi ni maskini. Saa nyengine labda uwape *notice* ya siku mbili, tatu, lakini sio unamkatia na unamwamba alipe faini tena.

Mhe. Spika, labda mimi niseme kuna taasisi za serikali zinadaiwa pesa nyingi sana, mamilioni ya pesa,

Mhe. Spika: Mheshimiwa una dakika tatu kumaliza hotuba yako.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Lakini wanakuwa wao hawakatiwi, kwa hivyo naomba hizi taasisi nazo zilipe.

Lakini niseme Mhe. Spika, katika kamati yako ya Baraza lako la Wawakilishi...

Mhe. Spika: Sasa unazo dakika mbili.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante sasa Mhe. Spika, ninamalizia. Tuliwahi kwenda *TANESCO* kutembelea lakini masikitiko makubwa tuliyoambiwa tunadaiwa pesa nyingi kama hizo. Mhe. Spika, kweli imenisikitisha sana, tunadaiwa karibu bilioni sabini na wakati wowote wanasema wanaweza wakakata umeme na wametoa indhari kubwa. Mwisho amesema mkurugenzi kama ule mtambo pia nikupeni nyinyi Wazanzibari mutie mafuta tu, lakini mutashindwa.

Lakini mimi ninashukuru sana serikali mbili hizi na muungano wetu mpaka leo tuna umeme bila ya kukatiwa. Ninawashukuru sana *TANESCO* na waendelee kutustahamilia.

Mhe. Spika, nimalize suala moja la mwisho la bustani ya Forodhani. Suala la bustani ya Forodhani wageni wetu wengi wanatembelea pale. Lakini mpaka leo bustani hii haina maji na deni la ZAWA ni milioni tisa lakini mpaka leo hakuna malipo yaliyofanyika, wala maji pale hayajafunguliwa.

Makubaliano ya mwisho maji yatafunguliwa ili bustani ya Forodhani iweze kupata maji. Lakini mpaka leo hamna chochote kuhusiana na suala hili. Pia niwapongeze wananchi wa Mji Mkongwe hasa askari jamii kwa juhudi zao kubwa kulinda miundombinu ya pale na kulinda wale wageni wetu wapate kutembea kwa vizuri kabisa na kuiona haiba ya Zanzibar, kwa ajili ya kuvutia utalii.

Mhe. Spika, mimi ninashukuru sana na ninaunga mkono ripoti hii. Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Salmin Awadhi Salmin: Ninashukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi nikaweza kuchangia mawili matatu kuhusiana na ripoti ya kamati hii muhimu iliyobeba wizara muhimu sana pamoja na utekelezaji wa maagizo ambayo yametolewa katika ripoti za wizara hizi kwenye bajeti iliyopita.

Lakini kabla ya hilo nitumie nafasi hii adhimu sana kumpongeza Mwenyekiti wa kamati Mhe. Mahmoud Muhamed Mussa kwa uwasilishaji wake na ripoti yake ambayo imegusa karibu maeneo yote. Pia niwapongeze wajumbe wa Kamati hii jinsi walivyoshirikiana katika kufanya shughuli hizi za Baraza katika maeneo mbali mbali.

La pili kama mnadhimu wa Chama cha Mapinduzi, nitumie nafasi hii kuwapongeza sana wananchi wa Jimbo la Kiembesamaki kwa kufanya haki yao ya kidemokrasia ya kumchagua mgombea wa Chama cha Mapinduzi Ndugu Mahmoud Thabit Kombo kuwa mwakilishi wa jimbo hilo, kujaza pengo lile lililokuwa wazi ambalo lilikuwa ni la mwakilishi wa Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*).

Mhe. Spika, jengine niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hasa chombo cha ulinzi na usalama kwa kuweza kuweka hali ya usalama na utulivu katika uchaguzi ule. Kama tunavyojua Mhe. Spika, kwamba chaguzi zetu hizi zinakuwa za ushindani mkubwa, lakini tunashukuru alhamdullahi vyombo hivi vimefanya kazi, hatimaye wananchi wamepata haki yao ya kuweza kupiga kura bila ya bughudha, bila ya vitisho. Kwa hivyo tuvipongeze sana vyombo hivi.

Ninajua Mhe. Spika, sisi ni watu wa ukweli, wanapofanya kazi vizuri basi tutawapongeza lakini pale wanapofanya kazi ovyo ovyo tutawaambia, ili wapate nafasi ya kujirekebisha. Kwa hivyo kwa hili tunawapongeza sana. Lakini jengine Mhe. Spika, nimshukuru sana Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa ufafanuzi ambao alioutoa wakati wa asubuhi juu ya hali ya mwenzetu; mwakilishi mwenzetu ambaye ni Mwakilishi wa Jimbo la Makunduchi Mhe. Waziri wa Kazi na Utumishi wa Umma, Mhe. Haroun Ali Suleiman.

Kwa kweli Mhe. Spika, tokea jana na juzi tumekuwa tukipata masuala mengi sana juu ya jambo hili mpaka unafika pahala unajiuliza kulikoni. Lakini sasa lazima tujue chimbuko la jambo hili. Inaonekana chimbuko la jambo hili ni matumizi mabaya ya simu ambapo inaonekana kuna baadhi ya wananchi wamesambaza *messages* za simu kuonesha kuwa serikali imetoa tangazo la kifo.

Sasa jambo kama hili Mhe. Spika, ninadhani serikali isilinyamazie. Ningeomba kutumia fursa hii niisome *message* ambayo nilitumiwa ambayo na huyu aliyetumiwa na yeye katumiwa. Kwa hivyo inaonekana ndio chimbuko hasa la matatizo haya. *Message* hii inasema hivi Mhe. Spika;

> "Tangazo maalum Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inasikitika kuwaambiwa wananchi wake kuwa Waziri wa Elimu wa zamani Mhe. Haroun Ali Suleiman amefariki dunia huko South Africa na kwa sasa ni Waziri wa Ardhi na Mazingira Zanzibar, tuwe pole kwa sote".

Mhe. Spika, *message* kama hizi ndizo zilizosababisha wananchi wababaike na haya ni matumizi mabaya ya simu. Na hivi karibuni tumesajili simu kwa makusudi ili wale wanaozitumia simu kwa njia hii waweze kujulikana. Sasa mimi ninataka kuiambia serikali, pamoja na kwamba ipo lakini Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ambao wao ndio wanaoshughulikia na masuala ya *ZANTEL*, sijui waziri gani yupo ambaye atachukua ujumbe wangu kwa sababu naona Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais haipo. Mhe. Spika, hebu niulizie.

Ninataka Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano lakini na ofisi ya serikali, iko wapi. Sasa kwa sababu mambo kama haya ndio mara nyingi tunasema tunakuwa hatupo *serious* katika mambo yetu. Leo tunajadili mambo kama haya ofisi kama hii haipo. Sasa tunapotoa maagizo yetu, maana yake yatachukuliwa na nani, baadae tumshike nani. Haiwezekani kwamba nyote ni serikali, lazima awepo mtu *responsible* ya jambo linalohusika. Hatuwezi kuwakamata nyote. (*Makofi*).

Tunataka mtu *responsible* hapa ambaye tutakuja kumuuliza, ni wewe, haya. Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utawala Bora atachukua dhamana. Ninachotaka kusema ni kwamba *message* hii ni lazima ifuatiliwe na ajulikane aliyeisambaza. Kwa sababu vyovyote vile chanzo chake kipo.

Huyu aliyeanza mche wa kusambaza, halafu wengine wakapata nafasi ya kuzisambaza kwa wengine, ni lazima serikali imtafute na kupatikana kwake inawezekana, kwa sababu simu hizi zimesajiliwa. *ZANTEL* imesajili kwa madhumuni kwamba mtu atakayetumia mawasiliano ya simu ajulikane.

Kwa hivyo serikali kwa kushirikiana na Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano wahakikishe kwamba mtu huyu anapatikana aliyeanza chembe ya kuzusha uzushi huu. Kwa sababu hili suala kama tutalinyamazia likiendelea hivi, leo kazushiwa huyu, kesho atazushiwa mwengine, hatimaye

hata Rais anaweza kuzushiwa juu ya mambo haya. Tunasahau kama sisi ni Waislamu...

UTARATIBU

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, naomba muongozo wako. Serikali ni nini na ukisema serikali kwa kushirikiana na Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, ina maana huyu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano si serikali. Naomba ufafanuzi.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano ni sehemu ya serikali. Anachokusudia Mhe. Salmin ni kwamba yule kiongozi wa shughuli za serikali ndani ya Baraza hili, ndicho alichokusudia yeye.

Na kama yeye hayupo basi yule ambaye huwa anachukua nafasi kwa niaba yake, kwa bahati mbaya wote kwa sasa hawajafika. Lakini tunaelewa kwamba benchi hii wote ni viongozi wa serikali ikiwa na pamoja Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano. (*Makofi*).

Haya tuendelee.

Mhe.Salmin Awadh Salmin: Mhe.Spika, asubuhi hapa tulisikia Makamu wa Pili wa Rais akitoa taarifa, hawakutoa wote hao; tulimsikia Makamu wa Pili wa Rais ndio anayetoa tamko la serikali. Sasa kama ilikuwa serikali yote basi nyote mungetoa. Lakini munajua kiongozi wa shughuli za serikali ni Makamu wa Pili wa Rais ndiye anayetoa matamko ya serikali. (*Makofi*).

Sasa suala hili Mhe. Spika, lazima lifuatiliwe lieleweke kwa sababu mambo haya tukiyaachia yaendelee, yataendelea. Kwa kweli tokea juzi na jana hali ya jambo hili ilikuwa inatia mashaka. Kwa hivyo, hatua zichukuliwe na taarifa tuzipate juu ya mtu huyu ambaye ametupa *message* hii.

Mhe. Spika, sasa nije kwenye ripoti ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati. Nianze na Shirika la Bandari. Mhe. Spika, maoni na ushauri wa Kamati kuhusiana na Shirika la Bandari, kuna maoni na ushauri mengi sana hapa yanafika 13 ambapo Kamati imetoa. Lakini mimi nitazungumzia hili moja juu ya kurundikana kwa makontena pale katika eneo la Bwawani, ambapo Shirika la Bandari inaonekana *twabaan* ndipo wanapoweka.

Kwa kweli Mhe. Spika, ni lazima tuwe wakweli kwamba wakati mwengine tunaamua mambo ambayo hata kwenye sura za kidunia inakuwa ni kichekesho. Hivi pale Bwawani ndipo pahala la kuweka makontena kiasi kile.

Mhe. Spika, kwa kweli haipendezi, ni lazima serikali itafute eneo jengine la kuweka makontena matupu, lakini sio pale.

Kwa hivyo, mimi nakubaliana na maoni au ushauri wa Kamati, juu ya kuyahamisha makontena katika eneo lile na kuyapeleka katika eneo jengine. Lakini sio kule walikoelekeza Saateni nyuma, hapana. Tunayo maeneo huru kule Fumba, kuna eneo kubwa tu kule, wanaweza kuomba eneo wakapimiwa rasmi likawa ni eneo la kuweka makontena na sio mbali hapo.

Eneo jengine Mhe. Spika, ni mamlaka ya usafiri baharini. Mamlaka ya Usafiri Baharini ina changamoto kubwa hapa ambayo nimeiona. Kwanza ni ukosefu wa ofisi ya kudumu ya mamlaka ambapo kwa sasa wanakaa katika jengo la kukodi kwa gharama kubwa sana, imeongezwa sana, hatujui ni kiasi gani.

Mhe. Spika, siku hizi tunazo taasisi zetu ambazo zinatoa mikopo. Kwa mfano ZSSF. Sasa unapoona maelezo kama haya yanatushangaza, kwamba kwa nini taasisi hizi au serikali kila wakati inakodi majengo kwa gharama kubwa. Pia ukiangalia ile hesabu ambayo wanalipa kule kwenye kukodi majengo, pengine kodi ya miaka mitatu au mitano basi inaweza ikajenga jengo moja kubwa tu la serikali.

Kwa nini tuendelee kukodi majengo kwa gharama kubwa, wakati uwezo na maeneo yako mikononi kwa serikali, kwa nini tusitafute maeneo tukajenga, mkachukua mikopo katika mfuko wa hifadhi, wana pesa nyingi pale hawana vya kuzifanyia. Twende tukachukuwe pesa tukope tujenge, halafu tutalipa taratibu. Lakini maelezo kama haya ya kukodi majengo kwa gharama kubwa, hii haipendezi ni lazima tufike pahala tubadilike na kwa sababu tunapojenga, maana yake tunaujenga na mji wetu, sio kila wakati tunakodi. Pengine kuna dili za watu humu humu.

Mhe. Spika, mimi ningependekeza kwamba taasisi hizi zenye matatizo ya majengo, basi watafute maeneo wakachukuwe mikopo, mikopo inakubalika, wenzetu wa Mfuko wa Hifadhi wana pesa nyingi sana. Mfuko ule uko chini ya kamati yangu, siku zote wanasema jamani wacheni serikali ije ikope na riba yao sio kubwa, kopeni pesa mujenge majengo badala ya kukodi majengo. Huo ndio ushauri wangu Mhe. Spika.

Jengine Mhe. Spika, ni kuhusu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ambayo ina changamoto hapa, ambazo Mhe. Mwenyekiti amezieleza nazo ni nyingi. Kwa sababu zimeanzia (a) mpaka zimemalizia (t), ni nyingi ukizisoma huwezi kuzimaliza.

Kuna changamoto ya kwanza (a) ambayo inasema:

"Kampuni ya *ZAT* kutolipa deni wanalodaiwa na mamlaka, kuna ada ameitaja hapa ambayo ni shilingi karibu milioni 400, pamoja na kukataa kufunga mkataba mpya na mamlaka kama ilivyoagizwa".

Sasa mimi najiuliza, kama wamekataa kufunga mkataba sasa wanafanyakazi vipi. Mhe. Spika, hawa watu wanafanya shughuli pale wanatoa huduma kwenye viwanja vya ndege, lakini kama wanakataa kufunga mkataba wanafanyakazi vipi na kama wao wanatoa huduma pale, kuna ada hii inalipwa shilingi milioni 400, kwa nini wasilipe na wao wanafanya shughuli pale na wala hawafanyi bure wanapata pesa.

Sasa haya mambo mengine wala sio changamoto ni mambo ya kuchukuliwa hatua. Ni lazima hatua zichukuliwe kuhakikisha kwamba hizi pesa zinapatikana na mkataba unafungwa, ili waweze kufanyakazi kwa mujibu wa mkataba.

Lakini eneo jengine kama changamoto ya (b), inasema;

"...uchakavu wa vifaa muhimu vya ulinzi na usalama kama vile *X-Ray machine",*
na vyengine ambavyo wamevitaja hapa.

Lakini kuna changamoto moja kubwa sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Kwa dakika tatu. (*Kicheko*).

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Juzi Mhe. Spika, wakati nasafiri kwenda Pemba, ile ndege ambayo nilikuwa nasafiria, iliwekwa kule kwenye Uwanja wa Ndege wa serikali, ndege ya Kampuni ya As Salaam Air. Fikiria niko *VIP*, natoka pale nje nauliza ndege iko wapi, naambiwa iko kule. Hivi kweli, mambo haya ni *very local*! Tunashindwa hata na Viwanja vya Ndege vya Mwanza, kuna mabasi unapokwenda ndege ikiwa mbali basi unapanda kwenye basi unapelekwa. Leo tunazungumzia suala la mabasi ya abiria, lakini yale mabasi ya huduma katika uwanja wa ndege hayapo, unatembea zaidi ya nusu kilomita kwa miguu kufuata ndege. Sasa hiyo ndio *administration* ya aina gani?

Mhe. Spika, kwanza kutembea katika kiwanja cha ndege ni hatari haikubaliki hata kidogo. Kwa hivyo, suala hili Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ni lazima walirekebishe, na watafute mabasi kwa ajili ya kupeleka abiria.

Mwisho Mhe. Spika, ni katika eneo hili hili juu ya *terminal* hii ya viwanja vya ndege. Hapa Kamati imeeleza mambo mengi, lakini kuna mambo mengine

mimi yamenishtua, kwa sababu ni tofauti na yale maelezo ambayo yanatolewa.

Mradi wa *Airport Terminal II,* kuna maelezo hapa mengi ambayo yametolewa na Kamati ambayo yanatofautiana kabisa na yale maelezo tulioambiwa na serikali wakati ule na Mhe. Omar Yussuf Mzee Waziri wa Fedha, juu ya *position* ya lile jengo lilivyo. Lakini suala hili Mhe. Spika, ni lazima lifanyiwe kazi.

Mhe. Spika, kuna maelezo ambayo Kamati ilieleza hapa inasema, licha ya kuwepo maelezo kutoka serikalini kuhusianana na maamuzi ya kuendelea na ujenzi wa *terminal* hiyo kwa kuirekebisha, bado kamati inashindwa kushawishika kwamba njia iliyochaguliwa na serikali ndio sahihi na ambayo haitaleta hasara kwa nchi yetu. Haya ni maelezo mazito yaliyotolewa na Kamati, lakini pamoja na maelezo mengi sana.

Kwa hivyo, mimi Mhe. Spika, pamoja na muda wangu kuwa ni mdogo, lakini nilikuwa nina maelezo mengi juu ya sehemu ya majengo na kadhalika. Lakini suala hili ni lazima serikali ijipange upya. Kwa sababu kuna maelezo mengi juu ya athari ya jengo lile. Naamini kama serikali itauchukua ushauri wa Kamati na kuufuatilia na kuufanyia kazi, basi serikali itakaa katika sehemu nzuri, kuliko kufuata yale maelekezo ya mwanzo ambayo waziri alitoa maelezo juu ya ujenzi ule wa *terminal.*

Kwa kweli Mhe. Spika, inatusononesha sana, kuona kwamba *terminal* ile haikamiliki, na kila wakati tunaulizwa na siku zinakwenda. Kesho na keshokutwa karibu *terminal* inachukua zaidi ya miaka mitano na gharama zinaongezeka kila kukicha, suala hili linatusononesha sana.

Mhe. Spika, kwa kuwa muda wako ni mdogo, basi tutalizungumza zaidi hili wakati wa bajeti itakapofika, wakati huo tuna zaidi ya dakika 30 kuzungumzia jambo hili. Mhe. Spika, naunga mkono hoja na sina matatizo na ripoti hii ya Mhe. Mwenyekiti, lakini ushauri na maelekezo yaliyotolewa basi serikali inatakiwa iyazingatie vya kutosha. Ahsante Mhe. Spika. *(Makofi).*

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuweza kuichangia taarifa hii ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. Kwanza na mimi nianze kwa kutoa pongezi kwa ushindi wa kishindo wa Chama cha Mapinduzi. Halikadhalika kumpa pongezi Mhe. Mahmoud Thabiti Kombo kwa kurudi tena katika Baraza lako hili tukufu na kwa aina yake.

Mhe. Spika, nianze na kumuunga mkono Mhe. Hamza Hassan Juma kuhusiana na suala zima la msaidizi wako, aliyekuwa Naibu Spika, Mhe.

Kamal Basha Pandu ambaye ndiye aliyenikabidhi kijiti cha kuleta maendeleo katika Jimbo la Rahaleo.

Mhe. Spika, viongozi wetu wakuu hawa ipo haja ya kuwaenzi kama alivyotangulia kusema Mhe. Hamza Hassan Juma na mimi niunge mkono pendekezo lake la kwamba suala lake lile la eneo ambalo alipewa, basi nimuombe Mwenyekiti wa Kamati aungane na Mhe. Hamza Hassan pamoja na mimi ili nafasi ile mwenzetu, mzee wetu aendelee kuendeleza maisha yake katika eneo lile.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nianze na Shirika la Bandari. Mhe. Spika, Shirika la Bandari, kama alivyozungumza Mhe. Hussain Ibrahim na mimi nichukuwe fursa hii pia kulipongeza Shirika la Bandari kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Pale bandarini kazi ambayo ameifanya mzalendo na Mzanzibari mwenzetu ni kubwa na ipo haja kuweza kuipongeza kazi ile, kwa sababu ni faida ya Wazanzibari na maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, pale bandarini sasa hivi ukenda na ukitumia bandari ile ni sehemu nzuri na wananchi wetu wanapata matumizi mazuri ya pale na wajumbe wako wa Baraza lako tukufu hili wanapata huduma nzuri pale. Tatizo liliopo pale Mhe. Spika, ambalo limekuwa ni kubwa sana kwa wananchi wetu, kwa sababu wananchi hutumia sana usafiri huu wa baharini kwa kutumia meli na maboti mbali mbali kwenda Dar es Salaam, Pemba, Tanga na kwengineko, ni la sehemu ya kuwaweka wagonjwa ambao wanasafirishwa kupelekwa Dar es Salaam au Pemba au sehemu nyengine kwa ajili ya kwenda kufanya matibabu.

Kwa hivyo, mimi ningeliomba shirika na wizara husika kwa jumla kuhakikisha kwamba wanaandaa sehemu pale angalau wale wagonjwa wawe na mahala ambapo wanaweza kukaa kiusalama na kuondoa ule msongamano.

Vile vile Mhe. Spika, nije katika Bandari ya Mkoani ambayo wananchi wetu wanapata matatizo makubwa, kama alivyozungumza Mhe. Hussein Ibarahim Makungu. Wakati wa jua au mvua wanapata tabu. Hawa ni wananchi wetu na ni wapiga kura wetu, wanahitajika kupewa maendeleo na kutokupata matatizo wakati wote.

Kwa hivyo, mimi ningeliomba sana Shirika la Bandari na kumshirikisha hususan huyu mzalendo ambaye ametuwekea majengo mazuri katika bandari hii ya Unguja, basi tumuombe kwa kushirikiana na serikali kuweza kujenga uzio pale na kuweka majengo yenye mapaa ya kuweza kuzuwia mvua pamoja na maji. Niliombe sana shirika kulifanyia kazi suala hili katika Bandari ya Mkoani.

Mhe. Spika, pia nije katika Mamlaka ya Maji. Mhe. Spika, tatizo la maji bado ni kubwa katika maeneo mbali mbali hususan katika maeneo ya majumba ya Maendeleo ya Michenzani. Wananchi wa maeneo yale bado wana matatizo makubwa ya maji. Naiomba sana Mamlaka ya Maji kuhakikisha kwamba inafanya miundombinu ya kuwawezesha wananchi wetu kupata maji katika maeneo haya ya majumba ya maendeleo.

Mbali na majumba ya maendeleo pia kuna maeneo mbali mbali hususan katika Jimbo langu la Rahaleo Mhe. Spika, kwenye maeneo ya Barastekipande na Mlandege hayo ni maeneo ambayo huwezi hata kuchimba kisima kuweza kupata maji.

Mhe. Spika, matatizo ya maji hayako katika maeneo haya tu, hata ukenda kwenye sehemu za Bweleo kuna matatizo makubwa ya maji, hata Kombeni kule. Mhe. Spika, wananchi wa Bweleo na Kombeni katika Jimbo la Dimani kuma mzalendo mzaliwa wa Zanzibar na ni mzaliwa wa Bweleo na wananchi wa Bweleo walielekezwa kutoa shilingi milioni 77 kwa ajili ya kulipa Mamlaka ya Maji ili kutatuliwa matatizo ya maji katika maeneo hayo. Lakini Mhe. Spika, ahadi ambayo ilitolewa na Mamlaka ya Maji mbele ya Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, basi mpaka leo tatizo lile halijatatuliwa. Wananchi wa Kombeni na Bweleo bado wana matatizo makubwa ya maji.

Mhe. Spika, katika maeneo haya kuna vianzio vingi vya maji, lakini bado tatizo hili Mamlaka ya Maji hawajalifanyia kazi, wanawaacha wananchi wanaendelea kupata matatizo. Kwa hivyo, ningeiomba sana Mamlaka ya Maji kufanya kazi kwa bidii ili kuhakikisha kwamba wananchi wa Bweleo na Kombeni wanatatuliwa tatizo hili la maji.

Mhe. Spika, vile vile nije katika Idara ya Nyumba za Maendeleo. Mhe. Spika, katika nyumba hizi za maendeleo za Michenzani na sehemu nyengine, tatizo kubwa pale ni miundombinu ya kuondoa maji taka. Ukienda katika majumba yale ya Michenzani ambapo na mengine yapo katika Jimbo la Rahaleo na mengine Jimbo la Kikwajuni na mengine Jimbo la Mji Mkongwe.

Mhe. Spika, hivi juzi kulikuwa kuna malalamiko makubwa na nimeona mimi mwenyewe katika TV, jinsi wananchi walivyokuwa wakimlalamikia mwakilishi na mbunge. Sasa Mhe. Spika, mwakilishi na mbunge aende kutatua tatizo la maji taka! Hili ni tatizo kweli. Lakini mimi nikasema nilisemee hapa kwamba mamlaka na idara hii ya nyumba walifanyie kazi suala hili, inakuwa ni uchafu mkubwa katika majumba yetu yale ya maendeleo Mhe. Spika. Wananchi wanapata harufu mbaya na ninashangaa kwa nini, kwa sababu wafanyakazi wapo.

Kwa hivyo Mhe. Spika, ningemuomba sana Mkurugenzi wa Idara ya Nyumba na Maendeleo alifanyie kazi suala hili, pamoja na Mhe. Waziri, kwa sababu haya majumba yamejengwa na mzee wetu kwa ajili ya wananchi ili wapate maendeleo na waishi katika maisha mazuri. Lakini sasa harufu na ugonjwa ambao wanaupata katika majumba haya ni makubwa na ni tatizo. Tunaondoa haiba ya mji wetu na tunaondoa haiba ya uzuri wa majumba yetu haya.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, mimi niunge mkono ripoti ya kamati hii kwa asilimia 100, na namtakia kila la kheri mwakilishi mwenzetu ambaye atawasili kesho katika jengo hili. Kwa hivyo, waheshimiwa tumpokee kwa shangwe na vigelegele kesho wakati atakapokuja kuapishwa. Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, nakushukuru. Ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, baada ya kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii. Mhe. Spika, naomba nitumie fursa hii kwanza kumrekebisha kidogo mnadhimu mwenzangu, kwa vile alivyosema kwamba kauli ya serikali anayeweza kutoa kauli ya serikali ni Mhe. Makamu wa Pili wa Rais tu pekee, na mimi naona kwamba sio sahihi kusema hivyo.

Kwa sababu hata Mhe. Issa Haji Ussi Gavu ambaye ni Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, basi akisimama hapa anatoa kauli ya serikali pamoja na mawaziri wote, nafikiri hiyo ndio sahihi zaidi. Maana yake yule waziri anayeweza kulisemea jambo fulani, basi huwa anaisemea serikali, hasemi kama yeye Gavu. Kwa hivyo, nadhani sahihi zaidi ni hivyo, lakini tukija tukibakisha kwamba ni Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pekee, nafikiri haitokuwa sahihi.

Vile vile naomba nitumie fursa hii kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Kiembesamaki, kwa kuweza kupiga kura zao kwa salama na amani. Lakini pia nawapongeza na wale wananchi wa majimbo mengine ambao walipata fursa ya kupiga kura. *(Makofi).*

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo, sasa nataka nianze moja kwa moja kwenye ripoti hii ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. Mimi nataka nianze kwa matokeo haya ya ajali ambayo kwa kweli yanaendelea kwa *speed*, ajali za meli nakusudia.

Mhe. Spika, sisi ni watu wa visiwa na kwa sababu usafiri wetu mara kwa mara ni wa kutoka ama Zanzibar kwenda Pemba au Zanzibar kwenda Dar es Salaam ni lazima tuvuke maji. Kwa hivyo, nadhani tungekuwa na chombo kilichokuwa *serious* sana na ambacho ni *committed* kweli kweli katika kuangalia hali ya hewa na mwenendo wa bahari. Idara ya Hali ya Hewa tunayo hapa Zanzibar nayo inatoa taarifa zake. Sasa na wale wanaosafiri au

waliokuwa na vyombo vya baharini, mimi nadhani wangezingatia sana ule utabiri wa hali ya hewa.

Mhe. Spika, ajali ile ya juzi ya boti, mimi nilikuwa nyumbani kwangu pale wakati wa Magharibi, ulivuma upepo sana na ukivuma upepo mimi akili yangu yote inaelekea baharini, husema jamani hakuna chombo huko kinachotaka kusafiri. Sasa kwa usiku ule hakikuwepo chombo, lakini asubuhi ndio ikatoka boti kutoka Pemba. Nilipokuwa narudi Msikitini asubuhi kusali na wenzangu tunazungumza habari ya upepo ule uliovuma jana, mwenzangu mmoja jirani yangu pale akaniambia aah! Mimi nina wanangu wanne wanatoka Pemba leo wanakuja. Kufika saa 5.00 nikasikia meli ile imepata ajali, na yule jirani yangu maskini wanawe watatu wamepotea.

Mhe. Spika, mazingira peke yake yanaonesha kwamba ile siku ilikuwa ni hatari kwa vyombo kama vile. Sasa kinachonisikitisha Mhe. Spika, ni kwamba tuna vyombo tumeunda sisi hapa. Kwa mfano kama hii *ZMA* hivi kazi yake ni nini. Hali ya hewa imesema kwamba kesho mawimbi yatakuwa ya ukubwa fulani, sijui ya mita ngapi kila kitu wanasema. Hawa *responsibility* yao ni kuwazuwia watu wenye vyombo vile vidogo visivyohimili mawimbi kama yale. Lakini Mhe. Spika, bado Wazanzibari hatujawa *serious*, tunatawaliwa na muhali. Maana aah! boti ya Bakharesa ukiizuwia bwana aah!. Sasa tunawauwa watu. Mimi nadhani wangetoa kauli kwamba boti ile isitembee basi tungeweza kuyanusuru maisha ya watu. Lakini siku zote tunapokea majanga ya namna hiyo.

Halafu Mhe. Spika, kuhusu *modification.* Mhe Makame Mshimba Mbarouk kazungumza hapa, kwamba bado muhali unaendelea, kwa sababu zile boti zilipokuja hapa hazikuwa na viti pale mbele. Leo wamejenga viti pale watu wanakaa na ilipotokea ile ajali basi wale waliokuwepo pale juu ndio waliokumbwa na ajali. Lakini waliokuwepo ndani walikuwa salama. Huu pia ni muhali hawawezi kumwambia mtu usifanye hivi, sijui ni kwa sababu gani. Sasa hii sio *commitment* ya kazi tuliyowaachia. Mimi nadhani kama hatutoondoa muhali na kuwataka watu wafuate sheria kwa mujibu wa tulivyozitunga, basi tutaendelea kupokea taarifa za ajali kila siku Mhe. Spika.

Kwa hivyo, nawaomba hawa wenzetu wa *ZMA* wawe *serious* kweli kweli, kwa sababu Wazanzibari hawana njia ya kupita na kwenda pahala pengine, wengi wao wanatumia maboti kwenda Unguja, Pemba na Dar es Salaam. Ni wachache sana walio na uwezo wa kupanda ndege na hizo ndege sasa hivi ndio mnasikia kama hivyo, mara ime-*fail* inaelekea mpaka wapi sijui ni mtihani moja kwa moja.

Hata mawasiliano katika vyombo vya baharini nalo ni tatizo kubwa. Mhe. Spika, chombo kinapata tatizo, basi wale wadhamini wa chombo kutoa mawasiliano wakaomba msaada inakuwa ni tatizo pia, matokeo yake watu pengine wanaanguka. Nusu saa tu kama mawasiliano yanafanywa basi watu wako karibu wanaweza kuja kusaidia, lakini hakuna mawasiliano. Matatizo yote hayo Mhe. Spika, yanachangia kupoteza watu wetu kiholela.

Nikiondoka hapo Mhe. Spika, nataka nizungumze kidogo kuhusu usalama wa viwanja vyetu vya ndege, lakini hata na bandarini. Usalama huu sio wa hizi boti zinazotembea baharini, lakini usalama huu ni wa pale kwenye lile eneo la bandari na viwanja vya ndege. Mhe. Spika, viwanja vyetu vya ndege na bandari zetu zinatakiwa zifuate sheria za kimataifa katika kuweka *standard* ya usalama unaotakiwa pale.

Kuna wakaguzi maalum wa *International* wanakuja kuvikagua viwanja vya ndege usalama wake, lakini wanakagua na bandari na kama hatu-*qualify* basi wanaweza kuzuwia bandari ile isitumike *International*. Wanaweza kuzuwia Kiwanja kile cha Ndege kisitumike *International*. Sasa tuangalieni nchi yetu, *base* ya uchumi wake ni utalii, watalii ambao wanapita bandarini na pia wanapita kwenye viwanja vya ndege.

Mhe. Spika, hebu fikiria siku moja viwanja hivi vikafungwa kwa sababu havi-*qualify* katika masuala ya usalama, na watalii wakishakata mwezi mmoja tu wasije tutatumia nini sisi. Suala hili serikali wanalijua na mpaka leo halijapewa kipaumbele. Sijui kuna wataalamu gani huko wanaopanga vipaumbele vya serikali kuwa jambo hili hawajaliona.

Mhe. Spika, nilikwenda pale uwanja wa ndege wanatumia magari mabovu yale ya *fire*, ambayo hayako *standard* kabisa na wameshapewa onyo. Sasa tusubiri kiwanja cha ndege kifungwe hiki halafu tuone tutafanya nini.

Siku moja Mhe. Spika, nilikuwa nasafiri pale uwanja wa ndege basi lile *screen* la usalama ni bovu halifanyi. Kwa hivyo, sasa abiria wote wameganda sasa binafsi akamate mkoba mmoja mmoja apekue afanye nini, jamani ndio kweli *international airport* yetu hiyo, tutafika wapi. Na nilisema siku moja hapa, sisi ni waislamu, kwetu sisi mbwa ni *najis* na mbwa akigusa nguo yako kwa mujibu wa sheria zetu za kiislamu nguo hiyo uioshe mara 7. Leo inasikitisha unakuja na mzigo wako pale analetwa mbwa ananusa nusa kila kitu pale. Mhe. Spika, hilo mimi siko radhi nalo na najiandaa kuja kuzuia bajeti ya mawasiliano kama mbwa yule pale hawatamuondoa kabisa kabisa.

Nilikuwa nataka kuzungumzia habari ya t*erminal* ile mpya inayojengwa, lakini Mhe. Salmin Awadh Salmin, kaizungumza vizuri na kawakilisha haya mawazo hasa niliyokuwa nayo. Kwa hivyo, naomba hii niache.

Sasa nizungumzie habari ya mipango miji, kuna Idara ile ya Mipango Miji Mhe. Spika, mimi naona tuna tatizo kidogo kwa sababu tunapanga miji yetu, lakini halafu sijui kama hili suala litakuwa linaigusa hiyo Idara ya Mipango Miji moja kwa moja au linagusa Wizara ya Mawasiliano au linagusa nani.

Nakusudia kusema kwamba kwa mfano mji wetu ule pale mpendae umekatwa viwanja vizuri, lakini hauna haiba nakusudia hasa suala la barabara, barabara zote za Mpendae ni mbovu hakuna njia moja inayopitika na tuombe Mungu isinyeshe mvua ikinyesha mvua pale mtu anajishauri apite wapi mpaka afike nyumbani kwake.

Kwa nini hatuzitengenezi zile barabara? Mji kama ule kwa wenzetu unavutia, vile ukiona tu maana barabara zake zote zimetengenezwa vizuri, zikatiwa lami. Kwa hivyo, una hamu hasa ya kupita kwenye ule mji. Lakini sisi wakishapanga *plan* yao, wakeshakata viwanja vyao, basi mji wanauweka vile vile na hili tatizo litatukumba kila pahali hata kule Tunguu, mwezi wangapi tunawakera angalau mule mlio na alama za barabara wakamchonge, mule mpaka leo wameshindwa.

Ukenda Mawasiliano wanakwambia nenda Ardhi, ukenda Ardhi anakwambia Mawasiliano. Kwa kweli hatuwezi kufika pahali tukajisifu kama tunaendelea ikiwa mambo madogo madogo kama haya mpaka leo yanatushinda mwaka wa 50 huu.

Mhe. Spika, jambo la mwisho ambalo nilitaka nilizungumzie kidogo ni kuhusu maji, Mhe. Spika, bado pamoja na juhudi wanazofanya *ZAWA*, lakini bado tuna tatizo kubwa sana la maji. Maji yamekabiliwa na miundombinu mibovu, maji yanakabiliwa na matatizo ya umeme, lakini maji yanakabiliwa na uharibifu
mkubwa sana wa vyanzo vya maji na Mhe. Spika, kwa kweli maji ndio kila kitu, yaani mtu kukaa kutwa moja asiwe na maji, hawi mtu tena anakuwa kama mnyama, maana yake ananuka kila harufu.

Sasa mimi nilikuwa nashauri hapa kwa sababu zamani mimi nakumbuka tulipokuwa wadogo, sisi nchi yetu ilikuwa na maji ya kutosha, kule kwetu kulikuwa na mito na ile mito ilikuwa katika hifadhi nzuri sana, ilikuwa inakaa maji kutoka *season* moja ya mvua mpaka *season* ya pili maji hayakauki. Maji yale yalikuwa yanasaidia sana kunywesha wanyama kwa wale wachungaji kama ng'ombe, mbuzi na punda, walikuwa wanatumia maji yale kunywa.

Maji yale pia walikuwa wanatumia wakulima kumwagilia kwa *project* zao ndogo ndogo. Sasa vyanzo vile vya maji vimeharibika vyote, matokeo yake sasa hivi mvua ikikatika tu hakuna sehemu hata moja ambayo inabakia na maji. Kwa hivyo, haya maji yanayovutwa na umeme sasa ndio hayo watu wananyweshea wanyama wao, ndio hayo hayo watu wanafanya *irrigatio*n. Kwa hivyo, ule upungufu maji unaendelea kutokea kwa sababu kama hizi.

Sasa mimi nilikuwa ninaiomba *ZAWA* itoe kwa kushirikiana na sisi Wawakilishi, Madiwani na Masheha, lakini tutoe taaluma maalum ili wananchi wetu waone umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji na kwa kweli vishaharibika vyote, labda sasa tupate taaluma na uwezo wa kuvifufua. Lakini kuna haja kubwa Mhe. Spika, mvua zinanyesha katika visiwa vyetu hivi *ahamdulillahi*, maji ya mvua yote yanaondoka hayabakii kwa sababu ile miondombinu ya kuibakisha yale maji tayari yote yameharibiwa, hakuna mto uliokuwa na maji sasa hivi.

Kwa hivyo, naomba sana *ZAWA* watoe taaluma ili wananchi waweze wenyewe, wakipewa taaluma uwezeshaji mdogo wanaweza wakafufua vile vyanzo vya maji na maji yakawa yanaendelea kubakia tukapunguza mzigo kwa hawa watu wa *ZAWA.*

Mhe. Spika, mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia. Ahsante.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, na mimi ninakushukuru sana kuweza kunipatia nafasi hii kutoa mchango wangu unaohusiana na Wizara mbili hizi. Mhe. Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu *subhanahu wataala* kunijaalia kuwa katika hali ya uzima pamoja na wenzangu wote, tuliomo ndani ya chombo chako hiki kitukufu cha kutunga sheria. Lakini Mhe. Spika, nichukuwe nafasi hii kuwashukuru wawasilishaji wote wa Wizara mbili. Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi Maji na Nishati na Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano pamoja na mwenyekiti wa kamati hii niwapongeze sana.

Mhe. Spika, nikielekea na mchango wangu moja kwa moja, nende kwenye Shirika la Meli na Uwakala katika ukurasa wa 94 na naomba kwa ruhusa yako unipe fursa kunukuu kidogo. Mhe. Spika, Shirika la Meli na Uwakala limeundwa na serikali kwa madhumuni ya kusimamia uendeshaji wa meli za serikali ili wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba wapate huduma ya usafiri wa uhakika na unafuu.

Mhe. Spika, kwa sasa shirika hilo linaishi katika wakati mgumu hali inayopelekea lengo hilo la serikali kufifia, kutokana na ukweli kwamba kwa sasa matatizo mengi yanalikabili shirika hilo kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, Shirika hili la serikali limeundwa kwa kutoa huduma Unguja na Pemba ndani ya visiwa vyetu vya Zanzibar. Na utakubaliana na mimi kama Pemba na Unguja pamoja na bahari, lakini njia kuu ya wasafiri wanaokwenda Unguja na Pemba, kila siku ya mwenyezi Mungu tuko njiani katika kusafiri, wananchi wanahitaji huduma hii kwa sababu hakuna njia nyengine isipokuwa ni anga na wengi hawana uwezo. Lakini mimi niseme tu katika shirika hili la meli, basi tuombe watu wa shirika na Waziri wetu wa Miundombinu watafautishe sana na makampuni yanayotoa huduma hii iwe ni hali ya juu Shirika la Serikali.

Nathubutu kusema hayo kwa sababu ukiangalia mtazamo Shirika la Meli pamoja makampuni, basi bei zao zinalingana tofauti na maelezo yaliyoko ndani ya kitabu. Mhe. Spika, tunaliomba Shirika la Meli kwanza liwe linatoa huduma bora, halafu liwe na unafuu, bei zisilingane hata kidogo na makampuni ambayo ni ya mtu binafsi kwa maelezo aliyoeleza ndani ya kitabu hiki. Mhe. Spika, tuwaombe wananchi wetu bei kidogo itafautiane iwe ya unafuu na huduma bora ipatikane kwa kila mtu akimbilie meli hizi za serikali kwa kuona huduma zake ni nzuri. Hilo moja.

Nikielekea katika Shirika la Bandari, Mheshimiwa Shirika la Bandari hapa nataka niipongeze sana serikali pamoja na Mkurugenzi wa Bandari pamoja na muekezaji mzalendo Bwana Salim Bakhresa kwa mambo makubwa aliyoyafanya katika bandari yetu ya Zanzibar. Ukiangalia katika bandari ya Zanzibar ukaja na Kiwanja cha ndege hicho hapo ni tofauti kubwa sana. Ambao uzuri ule ulikuwa upatikane kiwanja cha ndege kuliko bandarini, lakini tumpongeze sana Bwana Salim Bakhresa.

Inasikitisha sana huyu katika matengenezo aliyoyafanya pale bandarini, lakini mpaka leo ukiangalia ofisi yake hailingani na matengenezo aliyofanya pale. Tunaiomba serikali na Waziri wa Miundombini pamoja na Mkurugenzi wa Bandari wampe sehemu ajenge Ofisi inayolingana na ile sehemu. Ukenda ukikata tiketi ukiangalia hiyo Ofisi anayokaa Meneja Mashauri pale hairidhishi kabisa. Tunaomba umpe nafasi japo ndogo, lakini apate sehemu ya kujinafasi pale.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika mambo ya Viwanja vya Ndege. Katika viwanja vyetu viwili vya ndege kwanza niende hapa Unguja au Zanzibar kwa ujumla Mheshimiwa kiwanja cha ndege cha Unguja ni kiwanja cha Kimataifa cha Mzee Abeid Amani Karume, lakini ukiangalia hakistahiki kuitwa kiwanja cha Kimataifa. Mimi kasoro kubwa niliyoiona katika kiwanja kile na sehemu hizi ndogo ndogo mnazotupeleka kutembea, basi inatia aibu na fedheha, mpaka leo hii katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Zanzibar ndege ikitaka kuondoka, basi kuna yule mtu

anatangaza kwa mdomo kabisa ambao watu wengine hata taarifa hazipati. Mtu kama yuko chooni hawezi kusikia.

Mimi ninasikitishwa sana na Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano wakati akiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, Mheshimiwa waziri huyu jambo hili alikuwa analipigia kelele sana, mimi nimefarajika vya kutosha nikaona tatizo hili limeondoka, ninakumbuka kabisa alikuwa analitilia mkazo kweli kweli, lakini jambo lile kapata Uwaziri hajaliondoa ni aibu na fedheha kabisa.

Mheshimiwa ninakuomba kwa muda mfupi sana japo kuwa ni spika ya mkononi iwepo, lakini pia heri ya hivyo, basi mazingira yake si mazuri, wakati wa bajeti italia kwata hapa.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu naelekea kwenye Shirika la Umeme *ZECO*, kwa kweli watu wa Shirika la Umeme pamoja na matatizo madogo madogo yaliyopo wanafanya vizuri kwa kiasi. Lakini zuri lisilokuwa na kasoro. Mheshimiwa, hawa watu umeme wamekuwa na maneno mengi kuliko vitendo.

Pia, niizungumzie nikiwa mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano wakati huo kabla ya kubadilishwa kwenye Kamati ya Uwezeshaji, Wananchi na Ustawi wa Jamii, basi tulifika katika maeneo haya na changamoto zilizokuwepo mpaka sasa zijirudia rudia tuliwaambie hawa haiwezekani mtu kutoka Micheweni akafuata umeme Chake au Wete, wananchi wetu ni maskini, mtu anakwenda kununua umeme wa shilingi elfu mbili, lakini akatumia shilingi elfu tatu nauli yake, hili ni tatizo. Tunamuomba Mhe. Waziri, pamoja na watendaji wote wa Idara zake, basi watusaidie pale Madenjani ni *centre*, watuwekee kituo cha kuuzia umeme. Hata mtu anaweza akatoka Wingwi kwa baskeli ukenda akanunua umeme, lakini bila ya hivyo, mtatupelekea majanga mazito. Ni wazuri wa kuitikia, lakini si wazuri kwa vitendo, tunawaomba watufanyie neema, tena sasa inakuwa watu hawa wanatupanga, mtatupanga mpaka lini. Mhe. sisemi kama ni waongo, lakini uongo unaweza ukawadanganya wote hawa, lakini ukiwadanganya kwa siku nyingi watakugundua kama wewe ni muongo. Kwa hivyo, tujaribuni kueleza mambo ambayo tuna uwezo nayo kuyafanya. Mhe. Spika, ninaiomba sana Wizara hii ifanye mambo hayo.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu ambao ni wa mwisho, sitaki kukupotezea muda wako kwa sababu nadhani muda unakidhi haja ili uwaite mawaziri wafanye majumuisho. Naelekea katika bustani ya Forodhani. Bustani hii imekuwa ni ndoto ya alinacha, Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, katika bajeti tulikamatana sana na walisema watajitahidi

kuondoa tatizo lile na wafanyabiashara katika bustani ya Forodhani wanajitahidi kulipa kodi zao, lakini tulizungumza ndani ya Baraza lako tukufu hili kama hawapati huduma hasa huduma ya maji.

Na pahali popote palipokuwa hapana maji hapana usafi, tunakuomba tena Mhe. Waziri pamoja na watendaji wako wote, basi huduma hii iwafikie. Pale sehemu inakuja wageni wengi, lakini bila ya maji usafi hakuna.Kwa hivyo, tunakuombeni hili suala mulizingatie lisiwe linajirejea rejea mara kwa mara.

Mhe. Spika, kwa haya machache naunga mkono hoja mia juu ya mia. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, nami nitakuwa si mwingi wa fadhila kama sijakushukuru wewe kunipa fursa hii. Mwanzo kabla ya yote nimpongeze Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, kwa ushindi alioupata kwa kishindo tuna wimbo wetu unasema wembe ule ule.

Baada ya hapo Mhe. Spika, nianze na bandari yetu ambayo ni eneo kuu la kitega uchumi kutokana na ufinyu wa bandari ule na mengine, naweza kuthubutu kwa kujitakia wenyewe hatujawa tayari, ingawa mbuzi anakula majani kutokana na urefu wa kamba yake.

Mhe. Spika, bandari yetu kweli ni ndogo, lakini hapo mwanzo ilikuwa ikitoa huduma masaa 24 na sijui cha kushangaa, vipi hata ikafika hatua ya kuzuia masaa 24 yale ikafika muda wa saa mbili, saa tatu. Msongamano wa meli umekuwa ni mwingi hivi bandarini hivi sasa na mapato yanazidi kushuka na wengine kutoiamini bandari ile, hasa pale vitendea kazi inapokuwa kitendawili. Mhe. Hussein Ibrahim, alichangia hapa akasema Pemba *crane* hakuna, ukweli kwa muda mrefu *crane* bandari ya Pemba haina. Ile peke yake inasababisha msongomano wa meli, mzigo kushushwa kwa bega na kwa *crane* ni vitu viwili tofauti, muda unakuwa ni mwingi na kazi haifanyiki kwa mpangilio.

Halkadhalika bandari yetu ya Zanzibar ndio vile vile *crane* iliyokuwepo ni moja na ina meli karibu 6, *crane* moja hiyo inahitajika. Sasa msongomano huu tunaufanya kwa makusudi na hatujawa tayari. Mnadhim wa chama changu cha Mapinduzi alisema hapa kama Shirika la Bandari hawana pesa kweli wakakope kwa *ZSSF*, mtu kinachomfaa chake Mhe. Spika. Kwa kweli wananchi wanateseka sana na hasa wafanyabiashara vile vile ni muda mrefu na hakuna kinachoendelea.

Kuhusu kuondoshwa bandari ya forodha mchanga Mhe. Spika, wawekezaji wazalendo wa nchi hii wamepiga kelele kwa muda mrefu, wakaondoshwa

pale wakapelekwa eneo la Mpiga duri, mpaka jana Mpiga duri wamezuiliwa, sasa tunawafanya nini? Ikiwa eneo lile wameondoshwa waekewe pahali pengine, jana wamekwenda kupakia magari yao kule, wanaambiwa hakuna ruhusa kupakiwa magari mpaka sheha awepo, tunawavunja moyo wawekezaji wazalendo wa nchi hii.

Mimi niliomba sana Mhe. Waziri, hili suala ukaliangalia kwa jicho la huruma, wazalendo wa nchi hii wana haki yao vile vile, sio mpaka aje tajiri aheshimiwe nchi hii. Muda mrefu suala la *crane* leo miaka mingapi linapigiwa kelele, karibu miaka 20 au miaka 15.

Nije kwenye kituo cha daladala cha Darajani, mimi ningeomba sana serikali ikalifikiria upya suala hili wananchi kwa kweli wanapata shida na wanateseka hasa wanaokwenda hospitali ya Mnazi mmoja, hili suala ningeomba sana serikali wakaliangalia upya kabisa. Katika sherehe za Mapinduzi Rais wetu aliwahi kuzungumza Yoweri Museveni Rais wa Uganda alisema mtaji ni wananchi, serikali ndio wananchi, mimi serikali naiomba sana iangalie kituo kile kutafuta pahali muafaka kwa kukiweka.

Mhe. Spika, kuhusu *airport* yetu ya Zanzibar, viongozi wapo baadhi ingawa tunatafsiriwa vibaya, lakini ukweli viongozi hawaheshimiwi. Mifano iko hai ikiwemo Naibu Katibu Mkuu wa CUF ambaye alikuwa Waziri wa Wizara hiyo, gari yake kufungwa karibu kwa wiki moja pale Waziri Hamad Masoud. Juzi Mheshimiwa mwenzangu hapa Mwanajuma Mdachi alipata mtihani mpaka nikatokea mimi naingia kati yupo hapa sitaki kumsemea, mwanamke kama huyu anataka kuadhirika, tena mwanamme anayemuadhiri tena Mheshimiwa.

Mhe. Spika, mimi ninafikiri Ofisi yako itajaa siku zote risiti ya shilingi elfu ishirini kuletewa kila Ofisi kwako, sijui kama hizo pesa zitalipwa. Kama hatukujipanga kwa suala la Uwanja wa Ndege, wananchi wanateswa na wanateseka. Leo Mhe. Mnadhim kazungumza uwanja wa ndege unavyokwenda kuipanda masafa karibu nusu kilomita nzima.

Si wakati wa kwenda, wala kushuka, isitoshe wakati wa kuteremka unatoka nje, pana mlango pale umefungwa umetiwa mpira, umefungwa bure bure hakuna sababu unambiwa uzunguke kule, wafanyakazi wapite mwananchi wa kawaida asipite. Umemteremsha mgonjwa, hujateremsha gari, ishafungwa mnyororo ni kitu cha kusikitisha sana.

Utendaji wa Uwanja wa Ndege, mimi ninafikiri Mhe. Waziri, sijui kama ni shemegi au umesoma nae huyu Mkurugenzi, mimi ninafikiri iko haja ya

kuliangalia upya suala hili. Wananchi na viongozi wanateseka, tofauti na Tanzania Bara, nenda Tanzania Bara uone heshima unaoipata kiongozi.

Jengine kuhusu upekuzi bandarini wanawake kupekuliwa na wanaume, hiki kitu Mhe. Waziri, kiangalie vizuri kabisa wanawake wengine wana heshima zao na kupekuliwa isivyo halali.

Nije kuhusu Wizara ya Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati.Wananchi wa Bwejuu na Jambiani wamehangaika kwa muda mrefu nilikuwa nataka kuuliza ule mkopo wa umeme upo au haupo? Wamekuwa wakiteseka sana kwenda na kurudi na kama unavyojua nauli zenyewe zipo shida hivi sasa na maisha yenyewe, nataka kujua suala hilo umeme wa mkopo kwa wananchi upo au haupo?

Mhe. Spika, pia, kuhusu suala la maji, mimi ni miongoni ninayepata shida sana katika Wawakilishi katika Mamlaka ya Maji *ZAWA*. Jitihada ninazifanya kubwa kupitia Mbunge wangu pamoja na yeye, lakini bado utendaji unasikitisha sana katika Mamlaka ya Maji *ZAWA*. Hata masuala ninayoleta Barazani najibiwa halafu hayafiki pahali.

Wananchi wangu wa Pete Jimbo la Muyuni ikiwemo Kitogani na Muyuni wamekuwa wakikosa maji kwa muda mrefu, baadhi ya sehemu mimi nishasema nifikiwe, niko tayari kuchangia kwa lolote kusaidia gharama hizi ili wananchi wangu waondokane na usumbufu huu ambao unawakuta kwa muda mrefu, muda wao unapotea mwingi kusaka maji kuliko kuhangaika kwa sehemu ya kilimo. Mimi narudia kuomba tena mjipange, mimi niko tayari kusaidia suala hili.

Cha kusikitisha leo wananchi wa Jambiani wamekwenda kung'olewa mifereji yao yote, mifereji ambayo nimeinunua mimi na Jambiani nzima imeng'olewa na maji yenyewe hayatoki. Nimekwenda kuitafuta, hamna imebidi juzi ninunue mengine kwenda kuifunga Jambiani.

Mhe. Spika, hili linasikitisha na linarejesha nyuma huduma za Mwakilishi, kitu ukanunue, maji yenyewe hayatoki, halafu yale maji yanakwenda kufungwa na mifereji, inachuliwa imebidi ninue mengine, mimi jana kuipeleka kule jimboni, huduma yenyewe ya dhiki kwa kweli ni kitu cha kusikitisha sana Mhe. Waziri, hili suala ni la kukaa na kuliangalia upya.

,

Kwa hayo, machache Mhe. Spika, ninafikiri dakika kumi zangu zimekaribia, siungi mkono hoja mpaka nipate maelezo hasa ya Jimboni kwangu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa mara nyengine tena napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi tena ya kuzungumza katika ukumbi huu juu ya ahadi mbali mbali na maagizo mbali mbali ya kamati yetu ya Miundombinu ambao Wizara yangu ilipewa nafasi kueleza namna alivyotekeleza na nimefaidika sana na mchango wa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na kwa idhini yako, naomba muwatambue watu wote ambao wamechangia na wametoa rai mbali mbali inayohusu wizara yangu ambao wote ni 12:-

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2. Mhe. Asha Bakari Makame
3. Mhe. Hamza Hassan Juma
4. Mhe. Mohammed Haji Khalid
5. Mhe. Saleh Nassor Juma
6. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
7. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
8. Mhe. Salmin Awadh Salmin
9. Mhe. Nassor Salim Ali
10. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
11. Mhe. Hamad Hassan Omar
12. Mhe. Jaku Hashim Ayoub

Mhe. Spika, michango yao ni ya msaada mkubwa kwangu na wanachotaka Waheshimiwa wajumbe hawa ni utekelezaji zaidi kuliko majibu. Maana utekelezaji ndio utasaidia kuleta maendeleo kwa wananchi wetu kuliko majibu tu, ambayo itakuwa umesema na mmoja amesema hapa kujibu tu, kila mara haisaidii kitu, kitu muhimu utekeleze lile ambalo watu wamelitoa kama ni rai kwa ajili ya kufanikisha maendeleo ya wananchi wetu.

Hata hivyo, nalazimika katika baadhi ya maeneo kidogo na nitachukua nafasi hii kuzungumza kiliopo. Katika Idara ya Ardhi ninashukuru wajumbe kwa kutoa rai ya kutaka Wizara kuchukua juhudi kuepusha ujenzi holela katika maeneo mji wakati wa utayarishaji wa *master plan* unaendelea.

Wizara tayari imechukua hatua kwa kutengeneza kanuni maalum zitakazotumika ndani ya kipindi hiki kabla ya kukamilika kwa *master plan*. Ile *notice* ya kupitisha kanuni hizi imeshatengenezwa na wizara imeshachukua hatua mara tu *legal notice* itakapochapishwa katika Gazeti Rasmi, hivi karibuni katika robo hii ya mwaka mpango mpya wa usimamizi wa maendeleo ndani ya eneo lote la *master plan* utaanza kutumika chini ya usimamizi wa Mkuu wa Mkoa.

Ninawashukuru vilevile, waliozungumzia juu ya kiwanja cha Mhe. Kamal Basha Pandu, lakini hapa ninachotaka kusema ni kwamba kiwanja hiki kilitolewa na kikawa kina maelezo mengi, kikafutwa halafu ikaja tena hoja ndani ya Baraza hili, wakaleta hoja kwamba kwa nini kiwanja kile kimefutwa ambacho kinamsaidia mwenzetu na Wizara yangu ilipita kwa msukosuko juu ya suala hili mpaka ikabidi nichukuwe ahadi kwamba kiwanja hiki nitakirejesha tena, nimekirejesha tena.

Sasa uamuzi wa kwamba nikifute tena ni wa Baraza hili Mhe. Spika, kwa sababu kilifutwa kikaombwa arejeshewe, akarejeshewa, sasa kuja tena kifutwe tena, sasa Mhe. Spika, naona suala hili kwangu mimi kidogo litakuwa linanipa msuko suko kidogo katika kutekeleza.

Hata hivyo, yale matatizo ambayo yametajwa baadhi yake naona kama kwamba wenyewe watu wa Shirika la Umeme pamoja na kuwa pale pahala palikuwa karibu na *transformer* yao, walitoa eneo gani liachwe ili kiwanja hiki kianzwe kujengwa na lile eneo waliosema limeachwa kama kawaida. Lakini hata hivyo, mimi ni msikivu kulisikiliza Baraza linasema nini sina matatizo na hilo.

Hivi sasa ruhusa aliyopewa yule si wa kunyanyua moja kwa moja mpaka juu, amepewa ruhusa ya kujenga jamvi kwanza, halafu akutane tena na Mji Mkongwe kwa ajili ya kuendeleza ujenzi ikiwa tu kwa haya masharti aliyopewa katika hilo jamvi yamekamilika kama vile alivyoagizwa kuyafanya.

Matatizo ya ardhi yanayosabaishwa na ujenzi holela na utoaji vibali ovyo, Mhe. Spika, ni kweli kuwa kuna tatizo la ujenzi holela na mara nyengine utoaji wa vibali kwa taasisi tofauti, wizara tayari imeshalichukulia hatua suala hili kwa kufanya yafutayo:

Kwanza, Wizara imeshakamilisha matayarisho ya mpango mkuu wa matumizi ya ardhi ambayo utaongoza masuala yote ya utumiaji ardhi nchini.

Pili, kuanzia mwezi wa tano mwaka jana Wizara iliendelea na utayarishaji wa *master plan* ya mji wa Zanzibar katika eneo la Mkoa Mjini Maghribi, kazi hii itaondosha matatizo ya ujenzi holela na itakamilika mwezi saba. Aidha mipango kama hii itafanywa kwa mikoa yote 4 iliyobaki Unguja na Pemba.

Tatu, kanuni mpya zimetayarishwa ambazo zitaweka mfumo mpya wa utoaji vibali vya ujenzi katika miji baada ya kuchapishwa ndani ya gazeti rasmi kipindi kifupi kijacho. Suala la utoaji wa vibali litashughulikiwa na taasisi

moja itakayokuwa chini ya Mkuu wa Mkoa kama nilivyokwisha kusema mwanzo.

Kuhusu maeneo ya ukanda wa utalii yasioendelezwa. Mhe. Spika, kazi ya kufanya uhakiki inaendelea ili kuyatambua maeneo hayo. Kazi hii inafanywa kwa kushirikiana na *ZIPA*, lengo ni kuyarejesha serikalini na kuwapa wawekezaji wenye malengo ya dhati ya kuwekeza. Mhe. Spika, kazi hii imefanywa sana na wizara yangu na kuna orodha ambayo nimebahatika kuiona hapa katika Ripoti ya *PAC*, ambayo kwa kweli inatoka ndani ya wizara yangu na imeeneza haya maeneo yote ambayo yamekaa hivi sasa hayatumiki.

Sisi kwetu tunaita maeneo yaliokuwa na *speculators*, yaani watu waliotenga ardhi kwa ajili ya kuuza. Sisi hatukubali kuendelea kuacha maeneo yale yasitumike yakae vile vile yalivyo.

Kuhusu eka tatu. Suala la eka tatu limeandaliwa waraka maalum wa serikali ambao utasaidia katika kutoa maamuzi juu ya hatma ya ardhi hiyo. Aidha, idara inaendelea na jukumu la kuwaelimisha wananchi kuheshimu mipaka ya ardhi ya eka tatu. Tunatengeneza waraka maalum na tutaufikisha serikalini na tutatoa maamuzi hasa juu ya hatma ya eka tatu, mana uharibifu wa eka tatu ni mkubwa sana.

Kuhusu kiwanja Nam. 547 Kiwengwa, Idara ya Ardhi pamoja na Idara ya Mipango Miji na Vijiji zimechukua hatua za kusitisha ujenzi kwenye ardhi husika. Hata hivyo, mwananchi mmoja amekaidi amri hiyo na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake. Sasa mimi juzi tu ndio nimechukua hatua hii. Kwa hivyo, tutakwenda kumshughulikia zaidi.

Kuhusu familia ya Nungwi, Kendwa. Nimepokea shauri hilo nalifanyia kazi. Mwanasheria wa wizara analipitia jalada lao na ataishauri ipasavyo, hatua zitachukuliwa kwa mujibu wa sheria. Mhe. Spika, watu hawa walikuja hata kuniona mimi na wakanieleza mambo yao na kunionyesha nyaraka zao, nikawaambia waandike barua na nashukuru kwamba wameandika na liko ofisini kwangu suala hili.

Idara ya Ujenzi, Kiwanda cha kupiga Matofali ya Udongo Kwarara. Mhe. Spika, ni kwamba kusema kweli hiki kiwanda kina matatizo, juhudi za mwanzo zimechukuliwa kwa kulipima eneo hilo la kiwanda na kukiwekea mipaka, hati imeshatolewa na Idara ya Ujenzi imeomba fedha za kujenga uzio kukizungusha hiki kiwanda. Kusema kweli eneo la kiwanda mpaka sasa hivi halijaguswa, lakini ni kweli majumba yamekaribia katika eneo la kiwanda na

bila shaka wakati wowote wanaweza wakalivamia wakaingia katika eneo la kiwanda.

Kwa kuzuia uvamizi wa eneo hilo, hatua zilizochukuliwa ni kuweka ulinzi, yupo mlinzi anaishi eneo hilo na anatoa taarifa za kuwazuia watu wanaotaka kuingia katika eneo hilo kwa nia ya uvamizi.

Kuhusu vifaa vilivyoibiwa ambavyo hadi hivi sasa havijarejeshwa, kesi hiyo inaendelea na uchunguzi wa polisi. Tukio la mwanzo liliripotiwa Kituo cha Polisi Mazizini.

Bodi ya Usajili Wakandarasi na Bodi ya Usajili ya Wahandisi wasanifu na wakadiriaji majengo. Mhe. Spika, wizara inajitahidi kuzipatia fedha bodi zote mbili zilizopo katika Idara ya Ujenzi ambazo ni Bodi ya Usajili Wakandarasi na Bodi ya Usajili ya Wahandisi, Wasarifu wa Majengo na Wakadiriaji Majengo. Juhudi za kuwasilisha serikalini makadirio ya matumizi katika bajeti ya mwaka 2014/2015 hatua zinachukuliwa kwa kuwasilisha bajeti zao za uendeshaji bodi hizo ili serikali izipatie fedha za uendeshaji kwa kazi za bodi hizo.

Mhe. Spika, kwenye suala la nishati hakukuwa na mashauri mengi, Hivyo, kamati imeshauri serikali kujipanga vizuri katika matayarisho ya kuimarisha Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia. Mhe. Spika, ushauri kuhusiana na mambo manne muhimu kunachukuliwa na kufanyiwa kazi kwa madhumuni ya kuendeleza Sekta ya Nishati.

Mhe. Spika, kuna masuala yanayohusu *ZECO*, mwenyekiti aliuliza deni halisi tunalodaiwa na *TANESCO* ni kiasi gani? Deni la *ZECO* hadi kufikia Januari, 2014 ni shilingi 43,778,894,721. Hilo ndilo deni. Walileta bili ya kwamba wanaidai *ZECO* shilingi 70 bilioni, lakini walisahau kwamba walifanya kikao cha pamoja kabla wakazungumzia juu ya deni tangu wakati huo deni ni shilingi 38 milioni, ikabidi kuna baadhi ya madeni yasiingizwe katika bili ya Zanzibar. Mfano malipo ya huduma ya *EURA* Zanzibar haipati huduma za *EURA*. Kwa hivyo, haina haja ya kuongeza madeni ya *EURA* katika deni la Zanzibar.

Pia, yako mengine madogo madogo ambayo vile vile walikuwa wanayaingiza na ambayo huduma hizo zinatoka Tanzania Bara hazitolewi hapa Zanzibar. Katika kulipunguza juzi walikutana wakazungumza suala hili na ndio ikafikia kiwango hichi ambacho nimekitaja hivi sasa na bado mazungumzo yanaendelea. Kwa hivyo, tunategemea kwamba huenda hiki kiwango cha 43 bilioni kikashuka zaidi kutokana na makubaliano mbali mbali waliyokubaliana katika kulijadili suala hili.

Mhe. Mohammed Haji Khalid, aliuliza kuhusu kuongeza vituo katika maeneo ya Konde na Mtambile. Mhe. Spika, shirika limeshafungua vituo huko Gamba na Makunduchi. Hivi sasa limo katika matayarisho ya kutafuta eneo la kujenga ili kuweza kufungua vituo huko Konde na Mtambile.

Mhe. Spika, utatuaji wa moja kwa moja katika suala la ununuzi wa umeme ni kujiunga na mitandao ya simu, hilo tatizo la moja kwa moja, unaingiza fedha zako katika simu yako kama shilingi milioni kumi au kumi na tano, unapewa *password* unatia *password* yako, unaeleza kiwango cha umeme unachokitaka, mtandao unakata pesa kutoka katika pesa zako ziliomo ndani ya simu, basi moja kwa moja huna haja ya kutoka kwenda dukani.

Huu unaweza ukaununua hata saa nane ya usiku au tisa unaletewa nambari tu, ukitia kwenye mita yako moja kwa moja unapata umeme ambao ushaununua kwa mujibu wa kiwango unachokitaka. Unachotakiwa ni kujaza pesa ndani ya simu na sio kwenda kufuatilia kununua mahala. Huo ndio utaratibu ambao utakuwa mzuri na kuondoa tatizo hilo kusema kweli Mhe. Spika.

Kuna suala la Zanzibar inavyonufaika na miundombinu inayotumiwa na *TANESCO*. Katika makubaliano ya bei hayo niliyozungumza, sasa hivi ni kwamba *TANESCO* imekubali kupunguza bei ya kuwauzia umeme *ZECO* kwa asilimia mbili ikiwa ni kufidia matumizi ya miundombinu ya Zanzibar wanayotumia upande wa Tanzania Bara.

Mhe. Spika, kuna suala moja liliulizwa hapa tuliposema kwamba kuna madeni ambayo yanadaiwa mawizara na tukaambiwa kwamba tueleze hasa ni kiasi gani, nani keshalipa na nani hajalipa. Nachukua nafasi hii kueleza kwamba wa kwanza ambao wameshaanza kulipa hadi Disemba mwaka 2013 ni Wizara ya Afya, Idara ya Anga, Sauti ya Tanzania Zanzibar, Wizara ya Kilimo na Maliasili, Chuo cha Mafunzo, KMKM, TVZ, Bandari Huru, Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Chuo cha Utalii, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, Chuo cha Uongozi wa Fedha, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Waliokuwa hawajalipa mpaka sasa hivi chochote ni: Manispaa, Ofisi ya Rais Ikulu, JKU, Baraza la Wawakilishi, Uwanja wa Amani, Idara ya *UUB*, Idara ya Ustawi wa Jamii, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Idara ya Uchapaji, Mrajis wa Mahakama Kuu na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Hizo mpaka sasa hivi hazijaja kulipa, niliambiwa nizitaje hizi ili ziweze kujulikana. Kwa hivyo, nategemea kuzitaja hapa ni kwamba kesho watakwenda pale *ZECO* kwenda kurekebisha haya madeni ili tuweze kuondoa tatizo hili.

Mhe. Spika, malipo ya fidia kwa waathirika wa mazao wa Matemwe. Serikali kupitia mamlaka imeshaanza kufanya malipo kwa vipando vilivyoathirika katika upitishaji wa miundombinu ya maji kupitia mradi wa maji safi na usafi wa mazingira unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*), Shirika la Ukaazi la Umoja wa Mataifa na Serikali ya Mapidnzui ya Zanzbar. Jumla ya shilingi 267,523,600 zimetumika kwa awamu ya kwanza kuwalipa wananchi walioathiriwa na mazao kwa uchimbaji wa mtaro wa bomba la maji kutoka Kidombo, Kiashangwe, Fukuchani na Bwereu.

Hilo suala lililouliziwa ambalo Kiashangwe peke yake ni kwamba kwa njia iliyokwendea Kijini shilingi 53 milioni wamelipwa kama ni fidia ya nyumba zao na Kiashangwe Shehia ya Kidombo shilingi 201 milioni zimelipwa. Hivi sasa jitihada zinaendelea katika kuona kwamba wanalipwa mazao, maana kwanza walilipwa, sasa hivi jitihada inayokwenda wanalipwa mazao. Serikali inaendelea kufanya tathmini katika maeneo ambayo yalitarajiwa kutumika kwa upitishaji wa miundombinu ya mradi. Ufanyaji wa tathmini unajumuisha Ofisi ya Kilimu Kaskazini ‘A’ Unguja, masheha wa shehia husika na wananchi walioathirika na mazao hayo.

Mhe. Spika, limezungumzwa suala la maji Kombeni hadi Bweleo na kuna shilingi 57 milioni. Suala hili Mhe. Spika, mimi namshukuru sana Mhe. Nassor Salim Ali, kwamba amelitaja hapa na vizuri aje anielimishe nilifahamu na nitalifanyia kazi kwa haraka sana. Kwa sababu siwezi kusema kitu ambacho mpaka sasa hivi sifahamu na wafanyakazi wangu hawakuwahi kuniletea taarifa kamili juu ya suala hili.

ZAWA kutoa taaluma kwa utunzaji wa vyanzo vya maji. Hili ni wazo zuri tunatoa kila siku kuwafundisha watu kutunza vyanzo vya maji, ni suala muhimu sana kwa sababu vyanzo vya maji kama alivyosema Mhe. Abdalla Juma Abdalla, ni kwamba vinapungua kila siku.

Halafu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, sijui kwa nini hakuja kuniambia habari ya mifereji iliyong’olewa Jambiani, yote kabisa kwa sababu gani nikapata kujua sababu ya mifereji ile kung’olewa. Sasa nalo hili ni kama hili la shilingi 57 milioni kwangu ni jipya. Kwa hivyo, siwezi kusema tu hivi hivi nikasukuma hapa *just* kwa sababu nionekane nimetoa majibu, ni vizuri Mhe. Jaku Hashim Ayoub, vile vile, aje tulifanyie kazi suala hili.

Mji Mkongwe. Kamati inashauri Mamlaka ya Mji Mkongwe ikutane na Mamlaka ya Maji *ZAWA* ili waweze kukubaliana na kulipatia ufumbuzi tatizo la maji linalowakabili wananchi katika maeneo hayo na wafanyabiashara katika eneo la bustani ya Forodhani. Mhe. Spika, katika ushirikiano huku

Mamlaka ya Maji *ZAWA* imeweza kupeleka maji ya kutosha katika mahodhi maalum yaliyokusudiwa kwa umwagiliaji na matumizi ndani ya bustani hiyo.

ZAWA kwa jitihada ya zaidi itatoa msaada kwa mafundi na kuweza kufanya uungaji wa matangi ya ziada yatakayoungwa ya kuhifadhia maji kwa madhumuni ya kuongeza wingi wa maji mbali na yale yaliojengwa wakati wa matengenezo ya bustani.

Mhe. Spika, katika suala hili mimi nimewataka *ZAWA* pamoja na Mji Mkongwe waende pamoja kwenye bustani ya Forodhani wakatizame tatizo nini, maana maji yapo. Kwa sababu kuna mwekezaji mmoja kaja juzi pale akasema anataka kuunga maji kutia katika ujenzi wake anaotaka kuufanya pale katika mkahawa wake mpya anaojenga, bila shaka kayaona maji yapo ndio akaja akaleta hilo ombi. Lakini nafikiri kuna haja ya mafundi hawa badala ya kuzungumza tu hivi hivi naona halitaisha, bora twende hasa pale tukaifanye hiyo kazi kwa pamoja kwa kushirikiana tuone tatizo ni nini. Kama ni kuongeza *ROS over* pale katika ardhi ile na *pump* ziweze kufanya kazi kuona maji yanapatikana pale.

Halafu Kamati inazidi kusisitiza umuhimu wa usafi katika maeneo yote ya Mji Mkongwe. Hivyo, kamati inaagiza Mamlaka ishirikiane na Baraza la Manispaa katika kuhakikisha masuala ya usafi katika maeneo hayo linatekelezwa. Mhe. Spika, Mamlaka ya Mji Mkongwe katika suala la usafi inashirikiana na kulikabili suala kuondosha aina yoyote ya uchafu, mbali na taka za kawaida.

Vile vile, vifusi vya ujenzi na maji machafu kwa kufanya kazi kwa pamoja na kuwa na mikakati maalumu juu ya usafi wa Mji Mkongwe kwa kushirikiana na Baraza la Manispaa. Bado mashirikiano hapa naahidi katika wizara hii nitaendelea kuyasimamia kwa udhati kuona kwamba yanatekelezwa ipasavyo.

Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Makaazi. Ukarabati wa nyumba ya Kengeja bado haujaanza, sababu imetajwa hapa na mwenyekiti mwenyewe kwamba bado pesa zile shilingi 200 milioni tulizoahidiwa hazijaingizwa, tunategemea zitakapoingizwa hizo pesa tutaanza angalau kuliezeka lile jengo kunusuru hiyo hali. Kwa hivyo, agizo limesikika na ni imani yetu kuwa fedha za matengenezo zitaingizwa.

Suala la kutafuta gari ya kunyonyea maji machafu Pemba limefikia wapi. Wizara imefanya jitihada ya kutafuta gari la kufyonzea maji machafu na tayari limeshaanza kazi, gari hili ni la Baraza la Mji Wete kupitia Mradi wa *ZUSP*. Namuomba radhi Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kwamba tulitaja Manispaa,

lakini ni Baraza la Mji la Wete ndio wanalo hili gari la kufyonzea maji machafu. Kwa hivyo, limeshaanza kazi pale, tunalo kabisa.

Tatizo la maji machafu nyumba za maendeleo Michenzani kama alivyozungumza Mhe. Nassor Salim Ali, nalipokea na ninaahidi kwenda kulifanyia kazi.

Mhe. Spika, sina maelezo mengi sana juu ya suala hili, isipokuwa naona ni vizuri kwamba ni kwenda kulifanyia kazi zaidi kuliko kujibu. Na kwa sababu nakuja kwenye bajeti hapa nishajua hizi ndio nondo za kwenda kujiandaa zisije zikanipiga hapa.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasialiano: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia kukushukuru wewe kwa kunijaalia na mimi nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi.

Mhe. Spika, naomba nianze mchango wangu kwa njia ya kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya mambo ambayo yameguswa au yameelezwa moja kwa moja katika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Spika, la kwanza kabisa limezungumziwa suala zima la utaratibu wa uongezaji wa viti katika vyombo vya usafiri na hasa mfano uliotolewa ni katika Meli ya *Azam Link* kwamba imeongezwa viti. Mhe. Spika, meli hii ya *Azam Link* ni meli ambayo imetengenezwa nchini Ugiriki ikiwa ina urefu wa takribani mita 99.65 na upana mita 16 pamoja na *draft* ya mita 2.75. Baada ya meli hii kuundwa ilikuwa ikitumika kule kwa ajili ya kufanya shughuli za kusafirisha abiria, lakini pia baada ya kuuzwa kwa Kampuni ya *Azam* kama ilivyo desturi wataalamu wetu wa *ZMA* waliipitia na kuihakiki kabla na baada ya kufika nchini.

Kwa hiyo, idadi ya viti viliomo ndani ya meli hii vinaakisi na kukidhi matakwa ya sheria na kanuni za usalama na usafiri baharini. Hakuna utaratibu wa kuongeza vitu kinyume na utaratibu au kinyume na sheria kama vile maelekezo ya Baraza hili na maelekezo ya sheria husika yanavyoelekeza.

Jambo la pili, liliulizwa suala la wachukuzi katika eneo la Bandarini. Mhe. Spika, suala la wachukuzi liko katika maeneo mawili, upande wa mizigo wanaendelea kutoa huduma zao, lakini sote tunavyotambua kwamba mifumo ya mizigo imebadilika. Zamani takriban mizigo yote ilikuwa ikija nchini iko

katika mfumo wa magunia, hivi sasa asilimia kubwa ya mizigo inayokuja nchini iko katika mfumo wa makasha yaani makontena.

Lakini upande wa abiria tunashukuru kwamba wenye makampuni kwa kupitia Kampuni ya *Azam Marine* wamejaribu kuboresha huduma zile kwa kuona kwamba ile mizigo yote ya mkononi, mabegi na mengineyo wanachukua wao jukumu la kuidhibiti mizigo ile na kuikabidhi kwa mwenyewe akiwa tayari ameshashuka katika chombo husika.

Suala jengine lililozungumziwa ni suala la uwekaji wa matuta ovyo barabarani pamoja na usafirishaji wa makontena. Suala la uwekaji wa matuta kama alivyoeleza Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, kwamba yeye amelalamika kuwa anasumbuliwa hana pa kwenda katika Idara ya *UUB*. Maelekezo ni kwamba, katika Idara ya *UUB* utakapokwenda watakupa maelekezo kuhusiana na barabara za ndani, wao watakupa maelekezo na uwezo wa kwenda kusaidia kuweka matuta.

Kwa barabara kubwa utaratibu uko wazi, muandikie Mhe. Waziri, Bodi husika ya Mamlaka ya Usafiri Barabarani itakaa itapitia baadae itakwenda kumshauri Mhe. Waziri na baadae Mhe. Waziri, akiwa ameridhika atatoa Baraka za kwenda kuwekwa matuta hayo katika eneo husika.

Suala jengine lilizungumzwa la kwenda kuweka lami katika maeneo ya makaazi ya Mhe. Rais. Hili tumelipokea tutahakikisha kwamba tunakaa na wenzetu wa Mfuko wa Barabara tuweze kuona kiogozi wetu huyu tunamuenzi vizuri kwa kuweka lami katika makazi yake yote mjini pamoja na kule Kibele.

Suala jengine lilizungumzwa kuhusu Uwanja wa Ndege. Naamini Mhe. Waziri, atatoa maelezo mazuri yenye kuridhisha suala zima la uwekaji wa taa katika Uwanja wa Ndege wa Pemba.

Suala la pili, lililozungumzwa na Mhe. Asha Bakari Makame, ni suala zima la watoto wadogo kupatiwa leseni. Mhe. Spika, kama kuna mtoto yoyote aliye na umri chini ya miaka 16 akiwa na leseni ya kuendesha chombo chochote mtoto huyo, atakuwa amefanya kosa la jinai na lazima akamatwe na kushtakiwa kufanya kosa hilo.

Tunatambua kwamba mfumo wetu wa utoaji wa leseni za uendeshaji wa vyombo vya moto tunaruhusu kijana mwenye umri wa miaka 16 kwa leseni ya *category M*. Leseni hii ni leseni ya kupanda vyombo vidogo vya moto kama *moped* na *pasola* baadae umri wa miaka 18 nakuruhusu kwa leseni C na D, umri wa miaka 23 nakuruhusu magari ya dalala na mengine ya kufanyia

biashara. Lakini hatuna eneo lolote tunalomruhusu mtoto au kijana yoyote mwenye umri chini ya miaka 16 kuwa na leseni ya kuendeshea chombo.

Hivyo basi, nimuombe Mhe. Asha Bakari Makame atusaidie kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi tuweze kuwatafuta na tukiwabaini watoto hao tutawashitaki kwa kufanya kosa kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, suala jengine aliulizia je, viongozi wa wizara kama tumepata bahati ya kuitembelea bandari yote ili kuona na kuhakikisha usimamizi na taratibu zinaheshimika. Bahati nzuri kwamba mimi pamoja na Mhe. Waziri, tumepata bahati ya kutembelea eneo lote la bandari na kuona changamoto zilioko. Sote tunakiri kwamba eneo la bandari limekuwa finyu kutokana na mizigo, harakati na huduma zinazotoka katika bandari yetu.

Matarajio yetu kwamba ndoto yetu ikisimama uwezo wetu wa kujenga bandari mpya changamoto hizi zitapunguka. Kwa hivi sasa tunahakikisha kwamba mipango yetu mizuri iliyopo ni kupunguza mabanda yaliopo, kuhamisha ofisi zetu za watendaji katika jengo jipya na iliyokuwa *duty free* ili kuongeza eneo na wasaa wa kutosha kwa ajili ya uwekaji na huduma za makontena na huduma nyengine katika eneo la bandari.

Aidha, limezungumziwa suala la maegesho ya magari na matumizi hasa katika eneo la ndani ya bandari, lakini pia barabara inayopita nje ya bandari ile. Ni kweli Mhe. Spika, hasa wakati ambapo vyombo vinafika au vinasafiri kumekuwa na tatizo kubwa sana la abiria na wananchi wanaotumia huduma hizo kuweza kusumbuka. Sisi kama wizara husika tutahakikisha tunakaa na wenzetu wa polisi ili kuweza kutafuta njia mbadala ya kuweza kuondoa usumbufu huo.

Hivi sasa tayari wenzetu wa Kikosi cha Usalama Barabarani wamekuwa wakishirikiana nasi katika kuona kwamba nyakati hizi za *peak hours* wanakuja kutusaidia. Tunataka utaratibu ule wa kuwepo askari angalau uwe endelevu kwa masaa yasiopungua manane kwa kila siku ili kuweza kunusuru changamoto na shida ambazo zinaweza kujitokeza kwa wananchi wetu wanaosafiri ili kuondoa usumbufu wa kukaa muda mrefu barabarani bila ya kupata huduma ya kutumia barabara yao vizuri.

Suala jengine lilizungumziwa suala la malipo katika huduma za ukumbi wa watu mashuhuri. Maombi yalikuja hapa kwamba yale ni maamuzi ambayo yametolewa na wizara ni busara yakaondoshwa.

Mhe. Spika, maamuzi ya matumizi ya kumbi za watu mashuhuri hayakuwa maamuzi ya wizara peke yake, yalikuwa ni maamuzi ya serikali. Serikali ndio

iliyopanga nani wa kutumia ukumbi wa watu mashuhuri, kiasi gani kilipwe na vipi kilipwe. Kwa hivyo, tumuombe Mhe. Mwakilishi, kwamba aendelee kutumia huduma za ukumbi wa watu mashuhuri kwa kufuata taratibu husika ikiwa ni pamoja na kulipa, kama huo utakuwa usumbufu, bado ana nafasi ya kutosha ya kuweza kutumia kwa wasafiri wa kawaida pasina usumbufu wowote wa kulazimishwa kulipa.

Lakini akitumia ukumbi wa watu mashuhuri atalazimika kulipa na analipa kwa sababu ya huduma zinazotolewa kule ikiwa ni pamoja na vinywaji, vyakula na huduma nyengine za kwenda kuangalia tiketi na mambo mengine yanayohusiana na maandalizi ya safari yake.

Suala jengine ni suala la wizi katika eneo la chelezo. Hili nasema kwamba tumelichukua na tutakaa na waziri mhusika wa Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ pamoja na wenzetu wa Jeshi la Polisi ili kuweza kuona wanalidhibiti vipi eneo hili kwa ajili ya kuzuwia uharamia na watu wanaofanya shughuli za wizi katika eneo hilo.

Suala jengine ilikuwa la utaratibu wa wenye meli kuweza kutoa huduma za ushushaji wa mizigo. Ni kama tulivyoeleza kwamba hii ni sehemu ya kuendeleza utaratibu wa uwekezaji mzuri wa kuweza kuwasaidia abiria kushusha mizigo yao ndani ya vyombo husika.

Suala jengine ni suala la *CCTV* pamoja na *X-Ray machine* katika uwanja wa ndege kwamba hazipo na hazioni au mhusika hafanyi shughuli ya kuangaza vizuri. Mhe. Spika, utaratibu wa matumizi ya *X-Ray machine* ni kwamba mashine inawekwa mhusika anapaswa kupita katikati ya mlango ili mashine ziweze ku-*detect* nini ambacho kimepita na hasa ukiwa umepita na kitu cha *metal* au chuma kiweze kubaini.

Lakini suala la *CCTV*. Mhe. Spika, *CCTV* ni mitambo ambayo unachagua maeneo wewe mwenyewe wapi uweke. Kazi kubwa ya kamera ile ni kumurika kitakachopita usawa wa kamera husika. Sasa mimi nataka nilitoe hofu Baraza lako tukufu kwamba *CCTV* ziliopo katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, Kisauni zimetusaidia sana kubaini mambo mengi ya uovu.

Zimetusaidia kubaini watu wanaopokea rushwa katika eneo la uwanja wa ndege ikiwa pamoja na watendaji wetu na watendaji wa idara nyengine, imetusaidia kubaini vitendo vya uovu, uharibifu na uchafuzi wa mazingira katika eneo lile. Lakini pia, imatusaidia kubaini wahalifu na watumiaji wengine wasiokuwa na nia njema kwa uwanja ule.Pia, hata katika hili tukio la juzi la watu ambao walikuja kutelekeza mikoba yao ya shehena ya unga.

CCTV zile zimeweza kutusaidia na kubaini nani wahusika hasa waliokuja na mzigo ule.

Kwa hivyo, imani yangu kwamba Baraza hili ningelipongeza mamlaka kuweza kuamua kuweka mitambo ili kuweza kusaidia kufichua wahalifu na watu wengine wasioitakia mema nchi yetu.

Suala jengine lililoulizwa ni suala la ada ya kuingilia uwanjani iondolewe kwa watendaji wa *airport.* Naamini hili Mamlaka wameshalichukua *management* watalifanyia kazi ili kuondoa usumbufu unaojitokeza.

Suala jengine ni suala la eneo kwa ajili ya malipo ya *visa,* kwamba halijatolewa. Mhe. Spika, tayari mawasiliano mazuri yameshafanyika kati ya Mamlaka pamoja na Wizara ya Fedha na matarajio yetu kwamba mamlaka itafika pahali itaweza kuona umuhimu huu baada ya kuridhika na sababu zao za msingi walizozitoa. Lakini sote naomba tukumbuke kwamba eneo husika hivi sasa katika uwanja wa ndege ni maeneo madogo sana.

Kwa hivyo, eneo la kuweza kujenga kibanda hiki kwa ajili ya uwekaji wa hizi mashine ni lazima na wenzetu wa Wizara ya Fedha watalizingatia kwa kutambua kwamba maeneo katika uwanja wa ndege yamekuwa finyu, bila shaka watatafuta eneo ambao litakuwa na akisi, lakini pia huduma kama hii nadhani serikali itaichukua kwa kuilenga katika ujenzi wa uwanja mpya wa *Terminal II* utakapokamilika.

Suala jengine la mwekezaji wa uwanja wa ndege mdogo eneo la Kigunda. Mhe. Spika, uwekezaji huu una maeneo mawili, eneo la kwanza ni suala la ardhi. Naamini kwamba waziri mhusika atakuwa amelitolea maelezo kiasi gani wanaweza kumpatia hiyo ardhi. Sisi kama Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano tunachohusika ni kwamba tunatakiwa tukamilishe utaratibu wa kuwa na bodi au chombo ambacho kitakuwa kinafanya kazi kama ilivyo *TCA* kwa kuweza kumshauri Mhe. Waziri, ili kuweza kutoa vibali kwa ajili ya mwekwezaji huyu kupata ruhusa ya kuweza kuwekeza.

Mhe. Spika, eneo ambalo analiomba hata sisi kama wizara na kama mamlaka tayari tuna *interest* ya kujenga kiwanja kidogo cha ndege kwa malengo ya kutoa huduma kwa watu wa upande wa Kaskazini. Lakini pia, kuweza kuutumia uwanja huo pale yanapotokea matukio ya dharura ikiwa pamoja na kuweza kutumika kwa harakati za uokozi, hasa kwa maeneo ya mkondo wa Nungwi.

Mhe. Spika, suala jengine ni suala la usafiri na leseni kwamba magari yanatembea barabarani hayana namba za usajili. Hili ni kweli yapo baadhi ya

magari ambayo yanatembea barabarani hayana nambari za usajili na hali hii inatokana na mfumo wetu wa usajili. Sisi kama wizara tumekaa kwa kushirikiana na wenzetu wa *ZRB* kuweza kuona kwamba tunaandaa utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba kila gari inayoingia nchini kabla ya kutoka bandarini inaweza kusajiliwa ili kuondoa usumbufu huu ambao unajitokeza.

Mhe. Spika, suala jengine ni suala la deni la *ZAT* la shilingi 400 milioni alilozungumza Mhe. Mohammed Haji Khalid. Deni hili tayari limeshalipwa na tunaamini kwamba utaratibu wa kuweza kupata fedha hizi kwa mamlaka kutoka Hazina Kuu ya Serikali nalo litachukuliwa hatua. Na muda utakapofika wenzetu wa mamlaka watakwenda kuzungumza na kukutana na wenzetu wa hazina, ili kuweza kutumia fedha hizi kwa matumizi muhimu yakiwemo ununuzi wa mabasi, vifaa vya *X-Ray* na vifaa vyengine muhimu ili kuweza kuimarisha huduma katika uwanja wetu wa ndege wa Abeid Amani Karume pamoja na uwanja wa Pemba.

Suala jengine ambalo amelizungumza Mhe. Mohammed Haji Khalid, kwamba uwanja wetu unakabiliwa na changamoto nyingi ikiwa pamoja na upungufu wa vifaa. Ninamhakikishia Mhe. Mwakilishi, kwamba kadiri ya upatikanaji wa fedha changamoto hizi tutazipunguza.

Pia alizungumzia suala la chombo cha kutolea matangazo. Napenda nimthibitishie Mhe. Mwakilishi pamoja na Baraza lako tukufu kwamba tayari mashine ile ya kutolea matangazo imeshafungwa pale na nilikuwa namsikiliza Mhe. Hassan Hamad Omar wakati anatoa maelezo kwamba alikuwa akisema kwamba hakuna huduma hizi.

Jambo la msingi ambalo nilichokumbuka mara nyingi anaposafiri anatumia ukumbi wa *VIP*, sasa hajapita huu ukumbi wa *ordinary* hii mashine iko upande wa *ordinary*, kama atapita kesho ataiona. Tayari mashine ipo na utaratibu wa kutolewa matangazo popote katika eneo la Uwanja wa Ndege utaisikia mashine hii ikitoa maelekezo kuhusiana na suala zima la nani anasafiri ndege ya aina na muda unaosafiri.

Suala jengine ambalo limezungumziwa na Mhe. Saleh Nassor Juma kuhusiana na suala la usafiri wa baharini. Kuna tatizo kubwa sana hapa la usimamizi. Napenda kumthibitishia yeye pamoja na Baraza lako tukufu kwamba mamlaka ya usafiri baharini pamoja na wizara tutahakikisha tunafuatilia kitendo kwa kitendo kuweza kuona kwamba ufanisi na upatikanaji wa tija kama vile mamlaka hizi zilivyoanzishwa basi unafikiwa.

Suala jengine alizungumza suala la vifaa vya utambuzi na uokozi pamoja na suala la uwekaji wa taa Pemba. Naamini kwamba Mhe. Waziri atalitolea

ufafanuzi wa kina utakaoweza kutosheleza na kuridhisha Baraza lako hili tukufu.

Suala la kituo cha daladala kuwekwa mbali na bandari. Tunaamini kwamba mamlaka husika watakaa na kujadili kushirikiana na wizara yetu ili kuweza kuona maeneo yalipo yanaboreshwa ili kuweza kutoa huduma nzuri kwa wananchi wetu.

Suala jengine nilizungumza suala la miradi ya barabara. Mhe. Spika, ni kweli kwamba kuna changamoto kubwa sana katika utekelezaji wa miradi hii ya barabara. Inawezakana kama mradi una barabara kilomita 50. Lakini mkijikuta kwamba maeneo ya kwenda kuchukua kifusi au vifaa vyengine vya kuja kujenga hizi kilomita 50 ikapelekea usumbufu au uharibifu wa barabara zile ambazo mmekwisha kujenga. Hili kama wizara tumelipokea na tunaamini kwamba tunalifanyia kazi.

La kwanza kuhakikisha kwamba tunalinda barabara zetu kwa kuona kwamba magari yote yanayopita katika barabara yanakwenda kwa mujibu wa vigezo na viwango vya barabara husika. Kama barabara imeruhusiwa kupitisha tani 7 hatutokuwa na nafasi ya kuruhusu gari lililopakia tani 10 kupita barabara ile kwa sababu tunatambua tukiruhusu gari ambayo imebeba mzigo zaidi ya uwezo wa barabara tutakuwa tunakaribisha tatizo la uharibifu wa barabara husika. Lakini pia tuhakikishe kwamba katika miradi ile kuwe kuna fedha kidogo zinatengwa kwa ajili ya kunusuru maeneo haya ambayo yameharibika.

Aidha suala la fidia wananchi wa Vitongoji katika upitishaji wa umeme naomba nimtoe wasiwasi kwamba tayari wizara tumeshaliona na tumeshaandaa utaratibu mzuri na tutaanza kulipa kwa njia la *installment.* Kila mwezi tutalipa kiwango kisichopungua shilingi milioni kwa wahusika kwa deni lao lote la shilinghi milioni 33 wanalotudai.

Mhe. Spika, suala jengine limezungumzwa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu suala la Kanuni za *ZMA* naamini kwamba Mhe. Waziri atalitolea ufafanuzi wa kutosha.

Mhe. Spika, suala jengine alilozungumzia Mhe. Hussen Ibrahim Makungu; anazungumza suala la uchakavu wa vifaa vya *Airport* hasa mashine ya *x-ray* pamoja na *CCTV*. Imani yangu kwamba maelezo yangu ya awali niliyatoa kuhusiana na upatikanaji wa fedha hizi basi tutaweza kupata mashine nyengine mpya na vifaa vyengine vipya ikiwemao na mabati kwa ajili ya kutoa huduma kwa ajili ya wasafiri wetu. Kwa sababu si muda mrefu huduma za uwanja wa Ndege hapa mbele ya jengo liliopo hivi sasa vitafungwa na

huduma zote zitahamia upande wa kusini kunako jengo jipya ili kuweza kupitisha ujenzi uendelee kwa eneo ambalo lipo sawa kwa jengo letu.

Kwa hivyo, ili tuweze kutoa huduma vizuri tutalazimika tuwe na mabasi ya kuweza kuchukua abiria kuweza kwenda ng'ambo ya pili ili kuweza kuondoa usumbufu ambao Mhe.Mnadhimu wa Chama cha Mapinduzi ameueleza kwenda kupanda ndege eneo refu.

Mhe. Spika, limeelezwa pia suala la *Air Condition*, hili tumelichukua na tutahakikisha kwamba mashine zilizokuwepo kama zina matatizo zitafanyiwa marekebisho ili kuweza kutoa huduma nzuri ya kupata umande utakaokidhi katika eneo lote la *Airport.*

Aidha, lilizungumziwa suala la upokeaji na usindikizaji wa wageni liangaliwe upya. Hili tumelipokea na naomba nikiri kwamba kuna tatizo hilo kwamba eneo pale unaposhuka kutokana na utokaji wa watu wanapotoka Uwanja wa Ndege. Lakini pia kuondoa mrundikano wa magari pale, maelekezo ya Mamlaka imeonekana kwamba si busara kusimamisha magari, lakini tukaona tuangalie kwa hali gani kwamba watu ambao wana kesi maalumu wanaweza kupata msaada huo ikiwa pamoja na kushusha mgonjwa au kupokea mgonjwa ambaye atakuwa anasafiri au amekuja nchini akitoka kupata matibabu.

Suala la kipaa cha kukinga jua kwa upande wa Uwanja wa Ndege wa Pemba. Hili nalo tumelichukua na tutahakikisha kwamba haraka iwezekanavyo tutatafuta njia ya kuweza kutoa huduma hiyo ili kuweza kuwakinga wasafiri wasipate huduma za mionzi ya jua hasa nyakati za jioni. Pamoja na suala la gari ya zima moto tunaamini kwamba wizara husika watakuwa wamelipokea nao ili tuweze kushirikiana katika utafutaji wa mitambo hii muhimu na adhimu. Maana tutapokuwa na huduma mbovu za magari ya zima moto uwanja wenu unaingia katika hatari ya kuweza kufungiwa kwa sababu utakuwa haukidhi matakwa na masharti na miongozo mingine ya kuhakikisha usalama katika maeneo wa uwanja wa ndege.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu aliomba kwamba tuendelee kutumia vizuri eneo la Bwawani kwa uwekaji wa Makontena. Hili tumelipokea, pia na suala la kupeleka mashine japo moja Pemba hili nalo tutalifanyia kazi.

Mhe. Spika, suala jengine lililozungumziwa ni matumizi mabaya ya simu. Hili ni kweli kwa mujibu wa Sheria ile ya *EPOKA* inamtaka kila mtumizi wa simu yake aweze kuisajili na kutosajili simu unalazimika kupigwa faini ya shilingi milioni tano. Lakini pia katika hili Mhe. Mnadhimu alikuwa anakusudia suala zima la kuweza kubaini chanzo cha nani ameanzisha ile *message* ya kwanza iliyotengeneza uvumi ambao hauna ukweli. Suala hili na

sisi tutalichukua kwa kuweza kushirikiana na mamlaka husika pamoja na shirika husika ili kuweza kuona kwa namna gani anaweza kusaidia upatikanaji wa mtu huyu ambaye hakuwa na nia njema katika upotoshaji wa taarifa hizi ambazo hazikuwa na ukweli wowote.

Aidha pia naye ameshauri suala la Makontena kuwekwa Bwawani halileti taswira nzuri. Ni kweli halileti taswira nzuri lakini naomba tu ukumbuke Mhe. Salmin Awadh kwamba kontena moja kuliondoa bandarini mpaka kulifikisha pale Bwawani kuna gharama zisizopungua shilingi elfu 40 kwa kontena la futi 20.

Sasa tunapotaka kulihamisha kontena lile kulipeleka Fumba bila shaka gharama hiyo itaongezeka na gharama ile itarudi kwa wenzetu wasimamizi ambao ni Shirika la Bandari. Kwa hivyo, ili kuweza kwenda huko lazima tubadilishe taarifa zetu ili kuweza kuwa *accomodate* hilo. Lakini kwa kipindi hiki tunaona tuendelee kutumia eneo lile na tukaweza kujenga bandari yetu mpya basi usumbufu huu hautakuwepo tena.

Suala jengine ambalo amezungumza Mhe. Salmin Awadh ni suala la kukodi kwa kuonesha mfano wa majengo ya *ZMA*. Tayari sasa *ZMA* wamesharudi baada ya kupata jengo letu la Bohari kule wameachana na lile jengo la kukodi na wanakusudia kurudi katika jengo la Bohari sehemu ambayo ilikuwa ikitumika wizara baada ya wizara kuhamia katika maeneo ya Kisauni.

Suala jengine ni suala la kampuni ya *ZAT* kulipia deni lao. Tayari deni hili limeshalipwa na jambo la faraja kwamba leo hii jioni tumepata taarifa nzuri kwamba kulikuwa na bakaa karibu dola elfu 92 nazo zimelipwa kwa huduma zetu za Uwanja wa Ndege.

Suala jengine limezungumzwa na Mhe. Nassor Salim Ali kuhusu suala la uwekaji wa kipaa alitaka tushirikiane na bwana Bakhressa. Sisi kama wizara husika hatuna tatizo na kushirikiana na mtu yeyote tunaendelea kufanya utafiti kuweza kuona kama katika eneo lile kwa kuzingatia maumbile husika pamoja na pepo zinazovuma kwa uwezo gani kipaa kitakachojengwa kitaweza kuhimili uwepo wake. Ikiwa itawezekana tutatafuta mshirika wa maendeleo tuweze kushirikiana naye ili tuweze kujenga kipaa kwa ajili ya kujikinga mvua na jua lakini pia na usumbufu wanaopata abiria wetu.

Suala jengine alilouliza Mhe. Abdalla Juma Abdalla lilikuwa ni la Mamlaka husika katika usimamizi mzuri na huduma nzuri kwa wananchi wetu, alitolea mfano wa *ZMA* kuhusiana na hatua gani wanazozichukua katika ukingaji wa majanga. Nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba kwa kushirikiana na Mamlaka husika ikiwa ni pamoja na wenzetu wa *TMA* kuhakikisha kwamba

kila taarifa wanayotupatia tunaifikisha kwa walengwa ikiwa ni manahodha pamoja na watumiaji wengine wa huduma za usafiri wa anga wa barabarani, pamoja na usafiri wa majini ili kuweza kujikinga na majanga ambayo tunaweza kuyazuia

Aidha amezungumzia suala la utengenezaji na uingizwaji wa viti akatolea mfano katika Kilimanjaro. Tutahakikisha kwamba jambo hili halipo na kama tulivyosema kwamba hatutoruhusu chombo chochote kuengezwa viti au idadi ya abiria bila kukidhi matwaka na utaratibu wa kisheria uliowekwa.

Mhe. Jengine limezungumziwa suala la Shirika la Meli na uwakala kwa kuimarisha huduma zake, bado suala la eneo la ofisi kwa Kampuni ya Azam. Hili nalo tumelipokea kuhakikisha kwamba kampuni ya Azam tunakaa nao kuweza kupata eneo muafaka ili kuweza kutoa huduma zao.

Suala jengine alilozungumzia Mhe. Hassan Hamad lilikuwa ni suala la *PA* nalo pia tumeshalitolea maelezo.

Mhe. Spika, suala la mwisho alilozungumza Mhe. Jaku Hashim Ayoub alizungumza suala zima la *crane* kwamba inasumbua ni moja inasumbua wafanyabiashara na wananchi. Naomba tu Mhe. Spika, kwamba Mhe. Jaku Hashim atambue kwamba Shirika la Bandari linajiendesha kibiashara, na jambo lolote ambalo litakuwa na maslahi na wananchi wa Zanzibar pamoja na shirika lenyewe, serikali au shirika halitosita kuchukua hatua.

Kwa hiyo, hatuna dhamira wala lengo la kuona kwamba tunakuwa na *crane* moja kwa lengo la kutoa usumbufu kwa wananchi wetu. Nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba shirika linaendelea kutafuta nguvu za kuwekeza mitambo hii mikubwa kama tunavyotambua mitambo hii ni ya gharama. Na kama kuna mtu ambaye atakuwa na vifaa kama hivi kwa kufuata taratibu husika na masharti yaliopo serikali hatuoni tabu mtu huyo kuja kwa malengo ya kushirikiana na serikali katika utoaji wa huduma.

Suala la pili alizungumzia suala la Bandari ya Forodha Mchanga. Mhe. Spika, bandari hii imeshaondoshwa na tayari tuna *ramp* ambayo ina uwezo wa kutoa huduma hizi za kutosha katika bandari yetu ya Malindi. Nimuombe Mhe. Mwakilishi kwa kupitia kwake yeye pamoja na rafiki zako wanaofanya biashara hii basi watumie *ramp* iliyoko bandarini Malindi kwa ajili ya kutoa huduma hizi na waachane na huduma hizi zilizokuwa zikitolewa kule bandari ya Forodha Mchanga.

Suala la kituo cha daladala tumeshalitolea maelezo kwamba tutahakikisha kwamba mamlaka husika tunashirikiana nao ili kuweza kuona tunawezaje kuondoa usumbufu huo kwa wananchi.

Suala jengine amezungumza la *Airport* kwamba viongozi hawaheshimiwi katika maeneo hayo. Naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba kama itatokea tukio la kiongozi yeyote kuvunjiwa utaratibu na watendaji wetu asisite kuwasiliana na mamlaka husika, ikishindikana basi awasiliane na wizara husika ili tuweze kuona hatua muafaka za kinidhamu zinachukuliwa kwa mtendaji ambaye atakuwa amemvunjia taratibu kiongozi yeyote katika nchi hii.

Suala jengine amezungumza suala la mabasi kwa wasafiri wanaomba yapatikane. Hili tunaamini kwamba baada ya kupata pesa zao mamlaka watakaa na kuangalia kipaumbele kilichopo ili kuweza kutoa huduma hizi kwa wananchi husika.

Suala la mwisho Mhe. Spika, lilizungumziwa suala zima la uimarishaji wa huduma katika maeneo ya *Airport;* kwamba wanaona wanasumbuliwa. Nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba huduma hizi hakuna anayesumbuliwa na tutahakikisha kwamba wananchi wote wanakuwa sawa katika upatikanaji wa fursa na haki zao pamoja na wajibu katika huduma zote zinazotolewa na serikali.

Mhe. Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja asimilia mia moja kwa mia moja. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano. Wakati namkaribisha Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano niwaombe basi Waheshimiwa Wajumbe walioko nje waingie ndani ili kuja kumaliza shughuli hii haraka iwezekanavyo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Kwanza napenda nichukue nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai, uzima na taufiki ya kuzungumza.

Pili nichukue nafasi hii kwa kuwa asubuhi Mhe. Spika, nilipewa salamu za kuhuzunisha sikupenda kuchanganya. Wakati tunamuombea dua mwenzetu aweze kupata afueni ya haraka, Mwenyezi Mungu amjalie salama na arudi salama.

Napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Mahmoud Thabit Kombo kuwa na nafasi katika Baraza la Wawakilkishi kwa mara ya pili. Naamini akija mara hii atayakuta mambo yamebadilika tofauti na ambavyo tulikuwa Kikwajuni. Kwa hivyo, inabidi aje na kasi hii hii ya mabadiliko ambayo yametokea.

Baada ya hilo Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hii ya Mawasiliano na Ujenzi kwa juhudi walizochukua katika kupitia wizara yetu na kwenda katika baadhi ya maudhui kwa kina na kuona baadhi ya mapungufu. Baadae Wajumbe wakachangia ambao kwa kulinda muda wako kwa sababu Mhe. Waziri wa Maji ameshawataja naomba itoshelezeke hivyo hivyo.

Vile vile namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri wangu kwa kupunguza karibu asilimia 60% ya majumuisho ya majibu yetu. Kwa kuokoa muda vile vile nisingependa kuingia katika majibu ambayo tayari ameshayajibu. Isipokuwa mimi nitachukua yale ambayo yamebakia.

Mhe. Spika, Suala moja kubwa ambalo limezungumzwa na wachangiaji wawili au watatu, ni suala la jengo la *Terminal II*. Mhe. Spika, *Terminal II* tukubali kwamba lilifanyika kosa katika uanzwaji na uendelezwaji wa jengo lile na siku zote ikiwa litafanyika kosa watu hawaharibu kile kitu wanajaribu kukitengeneza.

Kila kosa litakalotokea ukajaribu kukiharibu kile kitu inakuwa kama uliyekuwa hukutumia bongo. Sasa ilipotokezea kuonekana kwamba jengo lina makosa wizara ilikaa kitako na wakandarasi na kujadiliana nao na tukafikia wakati tukakubaliana kwamba makosa yapo. Lakini tufanye nini, mshauri wetu aliyekuwepo uwanjani wakati huo Kampuni inayoitwa *ATM* alitumika katika kufanya matayarisho ya mwanzo ya marekebisho ya jengo liliopo, naye akaja na mbinu zake tatu tofauti. Serikali ikakaa kitako ikazitizama na ikakubaliana na mbinu moja ya kulifanyia marekebisho jengo lile, lakini katika hali ya kulibakisha liwepo pale pale lifanyiwe marekebisho.

Baada ya serikali kupitisha maamuzi hayo kwa mjadala mkubwa haikutoshelezeka kwa sababu lile jengo linaitwa *Terminal II*. Kwa maana ni jengo la pili la kufikia na kuondoka abiria wanaotoka sehemu zote za dunia. Ingelikuwa ni jengo letu wenyewe tu maamuzi yale yangekwishatoshelezeka, lakini kwa sababu ni jengo litakalotumika kupokea ndege kutoka nchi mbali mbali kubwa na ndogo ikaona kwamba sisi hatuna utaalamu wa kimataifa wa kutizama kwamba jengo lile je, sisi tumeshasema jengo lile libaki. Je, jengo lile likibaki pale linaweza kutumika kweli kwa kazi ambayo tumeipangia.

Mhe. Spika, wizara ikaishauri serikali na serikali ikakubaliana na wizara kwamba kweli kunahitaji mshauri muelekezi yaani *Consultant* akatangaziwa *Consultant* kwa tenda za kimataifa na akapatikana katika watano waliopeleka, watatu walijibu uzuri na mmoja akachaguliwa nayo ni Kampuni ya *ADPI* ya Ufaransa.

Kazi ya mwanzo tuliyompa tulimwambia tunataka ulitizame hili jengo lipo hapa tunataka kuliendeleza kufanya *terminal II.* Je, kuna njia ngapi ambazo sisi tunaweza kuliendeleza hili jengo. Mshauri muelekezi yule akafanya kazi akaja na njia nne; mbili katika hizo ni kulibakisha jengo pahala pake pale pale lilipo, na mbili akasema mnaweza kuliondoa halafu mkafanya haya na haya kwa marekebisho.

Sasa serikali ilikuwa imeshaamua kwamba tukilibakisha kutokana na hoja ambazo zimetolewa, mshauri muelekezi kaleta njia mbili katika nne mnaweza mkalibakisha. Nambie mtu ambaye ametumia bongo yake angelilivunja. Kwa sababu ukisema kuwa jengo lile livunje mshauri muelekezi kasema mnaweza kulibakisha jengo lile katika njia mbili na mkaweza kupata jengo la abiria la kufanya kazi. Hayo hakuyatoa kwa mdomo kayatoa kwa maandishi, hili nataka lieleweke wazi.

Kampuni hii ni ya pili katika dunia katika mambo ya viwanja vya ndege, na makao makuu yao yako Ufaransa hili la kwanza.

Pili mimi nikiwa Waziri baada ya kusikia ile *speech* ya kwenye bajeti nilikwenda kwa mainjinia wakuu ambao ni *Consultant DIASPORA* ni wataalamu wetu walioko nje Wazanzibari na sisi tumetegemea hapa kitengo cha *DIASPORA* kusaidia sio kusaidia pesa tu au mitumba lakini ni kusaidia mawazo katika wizara. Akanambia kwamba mambo mawili nakushauri kwanza hawa sisi tunafanya kazi na hata Rais wao mimi namjua na nitazungumza naye ili aisaidie Zanzibar katika mambo ya Anga na Viwanja vya Ndege.

Lakini anasema katika sheria za ujenzi duniani madhali mmemwita *Consultant* na kataja kwamba kuna njia mbili za kulibakisha jengo na mkaliendeleza hata mngekwenda kwenye mashitaka msingeshinda kwamba nyie mnataka kulivunja.

Sasa sisi kule tumezoea ushindani kwa sababu tuliwahi kukata mnazi kwa kuhesabu makuti. Sasa kama mnatuweza tuendelee na ushindani, lakini tunataka tulifanye hili jambo kitaalamu tusishindane tu. Wakati liko vile lile jengo limeshalipwa dola za kimarekani 37.5 milioni. Sasa ukisema wewe ulivunje pesa hizo atatoa nani?

Lazima tuwe watu wazima tutizame kila upande. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mwezi wa Februari tukijaaliwa Wachina wanakusanya zana na kuanzia mwezi wa Machi tukijaaliwa sisi kama tunakwenda Dodoma tukijaaliwa tukirudi nitawapitisha nyote hakuna ruhusa Mwakilishi yeyote kutoka Dodoma akaenda nyumbani lazima apite *Terminal II* kwanza akatizame kazi inavyofanywa.

Kwa hivyo, huu ni mualiko rasmi nawapa na tutakuwa na viburudisho kwa ajili ya kuwaonesha Wawakilishi wetu kwamba hii ndio kazi inavyofanywa tukijaaliwa. Kwa hivyo, nawaomba wote wanaotoka Dodoma wasifike Magomeni, wasifike Kwamtipura wala wasifike Rahaleo, wapite pale kwanza. Mhe. Spika, kwa *point* hiyo naomba nimalizie hapo.

Jambo jengine lililozungumzwa ambalo Mhe. Naibu Waziri alilitaja hapa ni taa za Uwanja wa Ndege Pemba. Hii ni ramani ambayo iliyokamilika ya kuweka taa za Uwanja wa ndege Pemba. Sasa siku moja nilisema hapa kwamba mie nilipokuwa Mwakilishi katika sehemu ya pembeni kule nilikuwa najua nafanya kazi mbili katika Baraza moja. Kwanza namuangalia Waziri na mwenendo wake.

Pili namtakia nusu ya yule Waziri huku Wizara ya Fedha aweze kuonekana. Lakini nyie mnavyofanya kazi wengi wa pembeni huko mnamtizama waziri tu, lakini hamumuombei chochote kwa Wizara ya Fedha. Sasa yeye anataka kufanya nini kama hajapewa? Mimi nawaomba sana wale ambao wamefuata ile kauli niliyotoa mwanzo ya kutetea taa za Uwanja wa ndege basi wanitizame mie na waniombee na fedha kule Wizara ya Fedha nitawashukuru sana. Kwa sababu mipango yetu sisi imeshakamilika kwa kutia taa inatakiwa idondoshwe tu fedha taa zinatiwa. Kwa hivyo nawahakikishia kwamba mipango imekamilika, sisi tayari tumeshapeleka maombi yetu rasmi Wizara ya Fedha kama ambavyo tumekubaliana. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ajaalie kwamba wakati wowote zikidondoshwa taa zitawekwa katika Uwanja wa Ndege wa Pemba.

Haya ndio mambo mawili makubwa ambayo nilitaka kuyazungumza ili tufahamiane kwamba sisi Wizara hatuna tatizo. Kwa sababu Waziri anapopewa bajeti unamtizama je, kaitumia? Tumerejesha pesa hatukutumia kwa kile kilichokusudiwa? Kwa hivyo tunapoangalia ile bajeti, hata siku hizo za bajeti unapoangalia unaona kuwa Waziri mwezi wa Machi kadondoshewa pesa hapa lakini mpaka mwezi Juni hajatumia kitu, lakini *OC* zinavyoingia na mambo mengine yanavyoingia lazima na hizi tuangalie.

Mhe. Hamza Hassan Juma aliuliza kuhusiana na kujitoa kwa Mkurugenzi Mkuu katika Kampuni ya *AEROTECH.* Kwa sababu mwenyewe hayupo aliyetoa jibu hili na sijui yeye mwenyewe aliyeuliza kama yupo maana simuoni nafasi yake. Suala hili lilijibiwa katika majumuisho ya bajeti na Mwanasheria Mkuu, na hii hapa *hansard* nimeichukua mimi. Kathibitisha huku Mwanasheria Mkuu kwamba yeye kathibitisha kwa vigezo vya kisheria kuwa Mkurugenzi Mkuu amejitoa katika hiyo kampuni. Sasa kama kuna masuala mengine itakuwa sisi hatuna njia kwa sababu Mwanasheria Mkuu aliyetumwa na Serikali kathibitisha kwa *hansard* hii kwamba Mkurugenzi Mkuu kwa vigezo vya kisheria kajitoa. Na mimi mwenyewe leo nimemuuliza umeshaambiwa hukujitoa, sema tena nimejitoa, eee nimejitoa. Sasa kama Mwakilishi yeyote atakuwa na ushahidi wowote kwamba hakujitoa aupeleke kwa Mwanasheria Mkuu, na Mwanasheria Mkuu kaahidi hivi, naomba hapa kunukuu alimalizia Mwanasheria Mkuu.

"Kwa hivyo mimi nikubaliane na Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba kuna tuhuma hizo, lakini hatukuzidharau tumezifanyia kazi, na tutaendelea kuzifanyia kazi kwa sababu bado ni tuhuma hatuwezi kuzichukulia kwamba ni *conclusive evidence".*

Sasa ilivyokuwa Mwanasheria Mkuu alisema hivi, yeyote yule ambaye anaona kwamba huyu Mkurugenzi Mkuu hakujitoa katika hiyo kampuni bado anaendesha shughuli za anga, apeleke ushahidi wake kwa Mwanasheria Mkuu atuletee sisi nakala tu. Mwanasheria Mkuu atashughulikia kwa sababu yeye ndiye aliyetumwa na Serikali. Lakini kuja kuendelea kusema hapa hakusaidii kwa sababu Mwanasheria Mkuu kathibitisha kwamba kwa mujibu wa taratibu za kisheria kajitoa.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nizungumzie tena kidogo kuhusu maendesho ya gari kwa watoto wadogo. Hili ni suala la kushirikiana. Siku hizi familia zina gari moja, mbili au tatu, ni juu ya wazee kuangalia kwamba watoto wao hawawaachii gari kama hawana leseni, kwa sababu atahatarisha maisha yake na maisha ya watu wengine.

Lakini la pili kwa kupitia sisi viongozi na Masheha tuhakikishe kwamba wale wanaopewa vitambulisho hawajafikia miaka 18, wasipewe. Kwa sababu ukimpa mtoto kitambulisho kwa madhumuni yako unayoyajua aliyekuwa hakufikia miaka 18, akienda yeye sehemu ya leseni akipeleka atapewa leseni kwa sababu anacho kitambulisho. Na kitambulisho cha Mzanzibari ni miaka 18. Sasa ukimpa mtoto mdogo atakitumia popote pale atakapoweza kutafuta leseni na mambo mengineyo. Kwa hivyo na hili tujilazimisheni kuliacha, kama ni kura wanatosha hao tulionao wakienda.

Mhe. Spika: Mheshimiwa hebu pumzika kidogo. Kufuatana na muda nadhani inabidi tuwaombe Waheshimiwa Wajumbe, ili tuongeze muda kumaliza kazi hii, najua Mhe. Waziri kabakia sehemu ndogo. Ili hatimaye tumuombe Mhe. Mwenyekiti naye amalize maneno yake.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa muda uliopo mbele yetu hautoshi kumaliza shughuli zilizo mbele yetu. Kwa hiyo kwa ruhusa yako naomba niliombe Baraza liweke kanuni ya muda kando ili tuweze kumaliza shughuli zilizo mbele yetu kwa leo. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wanaokubaliana na hoja wanyanyue mikono. Wanaokataa hoja. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Nakushukuru Mhe. Spika. Suala jengine ambalo ni matumizi ya shilingi milioni 40 za ujenzi wa barabara zilizotolewa na Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mji Mkongwe kupitia Mbunge. Mhe. Spika, hili suala ni tete. Toka mimi nilipoingia Uwaziri nimeletewa suala hili na nimefuatilia vya kutosha, tokea Katibu Mkuu wa mwanzo mpaka huyu wa pili, lakini baada ya msisitizo mkubwa na baadhi ya barua kupelekeana na kufuatilia ikaonekana kwamba hizi pesa ziliingizwa katika Wizara, lakini walioleta matatizo ni waingizaji, waliingiza kama vile mtu anavyoingiziwa fedha za zawadi, hazina karatasi yoyote iliyoambatana nayo.

Mhe. Spika, kikawaida fedha za Serikali zinapoingzwa katika akaunti zinafuatana na maandishi ya *voucher* ambayo ina madhumuni ya yale yaliyoingiziwa. Lakini fedha hizi ziliingizwa na Manispaa bila ya karatasi yoyote tokea mwaka huo mpaka hivi leo. Hata hao Manispaa hawakuleta barua, wala hawakuleta karatasi, wala hawakufuatilia, wala hawakufanya chochote. Sasa baada ya Wizara kuona kwamba malalamiko yamekuwa makubwa na kufuatiliwa huko Manispaa ikaenda *deep* kwenye mahesabu yake ya miaka mitatu iliyopita. *Balance* kutoka benki ikaenda ikachukuliwa za miaka mitatu iliyopita ndio ikaonekana kwamba milioni 40 ziliingizwa na Manispaa lakini ziliingizwa kwa njia hiyo kama mtu anayekutilia zawadi.

Sasa kwa sababu pesa zimeonekana katika akaunti ya Wizara, Wizara inathibitisha kupokea pesa hizi. Na Wizara inachukua jukumu la kuzitumia fedha hizi kwa njia zilivyopangiwa. Lakini vile vile inawataka Wawakilishi

na Wabunge wanaotumia njia hii wasiingize fedha kwa njia hii, lazima fedha ziambatane na karatasi ambayo itaonesha kwamba hizi zinaletwa.

Mhe. Spika, nitoe mfano. Mimi wakati kipindi hicho hicho nilipata malalamiko kutoka kwa Mhe. Raza, lakini risiti yake niliiona ndani ya barua iliyokuwepo. Kwa hivyo ilikuwa ni rahisi ku-*trace* kwamba fedha kweli shilingi milioni 20 ziliingia. Sasa ina maana utaratibu upo wa kuingiza fedha na risiti yake itaonekana. Kwa hivyo Wizara yangu ilipokea lakini katika mazingira kama hayo sidhani kama inastahiki kulaumiwa hasa baada ya kuona kwamba sisi ndio tuliofuatilia akaunti za benki za miaka mitatu iliyopita. Hilo ndio jibu lake Mheshimiwa. Najua kwamba mazungumzo yameshapita baina ya Mbunge wa Jimbo hili na Katibu Mkuu ili kuweza kuendeleza shughuli hiyo.

Mhe. Spika, baada ya hapo kwa kuwa mambo mengi yalizungumzwa na Mhe. Naibu Waziri, na mimi nilibakishiwa haya machache makubwa, naomba niwashukuru tena Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza. Na niwahakikishie kwamba kama alivyosema Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati madhumuni yake hapa si kujibu tu, lakini hasa ni kufanya utekelezaji wa yale ambayo Wajumbe walituelekeza. Kwa hivyo ningejibu tukaanza tu kujitetea hata ningefika mwakani, lakini yale yote ambayo Wajumbe wameyaona na yana kasoro sisi tunakubaliana nao na tutayatekeleza kadri ambavyo Mwenyezi Mungu atatujaalia uwezo wake. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Spika, naomba kwa mara nyengine tena kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu baada ya yote ambayo tulikuwa tunaendelea nayo katika jioni hii ya leo.

Mhe. Spika, baada ya majibu ya ufafanuzi ya Waheshimiwa Mawaziri pamoja na michango ya Wajumbe kwa ujumla, sina budi kuchukua dakika chache tu kuweza kuyajibu au kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya mambo mawili matatu, ili tuweze kwenda kujipanga na kuendelea na mengine.

Lakini kabla ya hapo napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wote waliochangia. Na kwa orodha yangu niliyonayo nina jumla ya Wajumbe 18 ambao walikuwa wamechangia. Ningeliomba kuwataja Wajumbe hawa ili wenyewe wajisikie na wajifariji.

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2. Mhe. Asha Bakari Makame
3. Mhe. Hamza Hassan Juma

4. Mhe. Mohammed Haji Khalid
5. Mhe. Saleh Nassor Juma
6. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
7. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
8. Mhe. Salmin Awadh Salmin
9. Mhe. Nassor Salim Ali
10. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
11. Mhe. Hassan Hamad Omar
12. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
13. Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati
14. Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano
15. Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano

Pia kuna waliochangia kwa maandishi nao ni:-

1. Mhe. Fatma Mbarouk Said
2. Mhe. Panya Ali Abdalla
3. Mhe. Marina Joel Thomas

Mhe. Spika, majibu na ufafanuzi umekwisha kutolewa na Mawaziri. Kubwa ninachowaomba Waheshimiwa Wajumbe wenzangu waende katika chumba cha *hansard* wakachukue Ripoti ya Mwenyekiti ambayo imesomwa hapa, ili waweze kufahamu zaidi kwa kadri ambavyo tulijaribu kutoa ufafanuzi juu ya mambo na hali halisi iliyokuwepo katika usimamizi wa Wizara hizi mbili ambazo Kamati yangu inasimamia.

Vile vile Mhe. Spika, ningependa kuelezea kwamba Kamati hii ya Mawasiliano na Ujenzi inafanya kazi zake kwa mujibu wa kanuni namba 111 kifungu cha kwanza (a) hadi (h) na tunakuwa tuko makini sana katika kutekeleza majukumu yetu, na sivyo kama vile baadhi ya watu wanavyoelewa.

Lakini pamoja na yote naomba kukariri eneo moja dogo sana ili kuweza kutoa ufafanuzi zaidi kwa yale ambayo yalikuwa yamejitokeza. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kusoma kipengele hicho.

"Mhe. Spika, kwa ujumla Kamati haipingani na maamuzi ya Serikali yaliyofikiwa ya kuendelea na ukarabati wa jengo, kwa kuwa inaamini kwamba imezingatia mambo muhimu na ya kimsingi. Hata hivyo, Kamati inaamini kwamba Serikali ingekuwa na maamuzi mazuri zaidi iwapo ingeuzingatia kwa makini sana ushauri wa Bodi ya Mamlaka ambao umetolewa kwa barua kwenda kwa Waziri. Ushauri ambao Kamati baada ya

kupata ufafanuzi wa kina inaona ni ushauri wenye nia nzuri ya kuendeleza uwanja huo na kuwezesha kuongeza mapato yake".

Vile vile Kamati ilitoa baadhi ya maelekezo. Lakini kwa kuendelea mbele zaidi kwa ujumla Bodi ya Mamlaka iliishauri Serikali kufuata pendekezo namba 2 (a) ambalo hata ushauri wa Mwelekezi umelitilia mkazo zaidi. Naomba kukomea hapo Mhe. Spika.

Baada ya hilo ningependa kutoa taarifa pale ambapo ilikuwa zinatolewa taarifa za malipo ya umeme. Baraza lako tukufu hili Mhe. Spika, nalo pia tumepata risiti yake limelipa katika mwezi wa Disemba shilingi milioni 20 na matumizi yake halisi yaani milioni 10 kwa mwezi.

Lakini vile vile nina barua ambayo ilikuwa ina hoja kamili ya Mhe. Kamal Basha Pandu, lakini kwa upande wetu kama Kamati tunasema kwamba maamuzi hayo kwa vile yalikuwa yamefikiwa na Baraza na utekelezaji ulifanywa na Serikali, na sisi kama Kamati tunalirejesha suala hilo katika Serikali au Baraza kwa maamuzi zaidi yanayofaa.

Baada ya hayo nachukua fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe wote waliopata nafasi ya kuchangia na waliokosa nafasi ya kuchangia, lakini wamechangia kutokana na mioyo yao kuwa iko pamoja nasi. Tunawashukuru sana na tunaomba kwa ujumla wao tujitahidi kutekeleza majukumu yaliyokuwa mbele yetu. Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, nashukuru sana na ahsanteni sana kwa kunisikiliza.

Mhe. Spika: Mhe. Mwenyekiti, tunakushukuru kwa kufanya majumuisho ya kiufundi ambayo umeyamaliza kwa muda wa dakika kama tatu nne tu hivi. Huo ni ufundi mkubwa.

Basi Waheshimiwa Wajumbe sasa kilichobaki ni kuwahoji kwamba wale wanaokubali kupokea na kukubali Ripoti za Utekelezaji za Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati pamoja na Miundombinu na Mawasiliano, na ile ya Mwenyekiti wa Kamati wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi kukushukuruni sana kwa mashirikiano makubwa ambayo tunapeana katika kuendesha shughuli zetu kwa ufanisi mkubwa.

Baada ya hayo basi Waheshimiwa Wajumbe sasa naakhirisha kikao hichi hadi kesho tarehe 04/02/2014 saa tatu barabara za asubuhi.

(Saa 1:50 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka
tarehe 04/02/2014 saa 3:00 asubuhi)